
# MAJI MAJI



TOLEO LA KISWAHILI

NA. 31 MEI 1977

**YALIYOMO**


UCHAMBUZI WA JUMUIA
KUADIMIKA KWA BIDHAA NCHINI
JUU YA SUALA LA DOLA
KUHUSU NCHI ZINAZONYONYWA
USHAIRI NA UKASUKU
UNYONYAJI WA WAFANYAKAZI CHINI YA UBEBERU
UJAMAA WA KINJOZI NA UJAMAA WA KISAYANSI



UMOJA WA VIJANA

WILAYA YA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

# M A J I M A J I

TOLEO NA. 31 MEI 1977

Hutolewa na: UMOJA WA VIJANA WA C.C.M.
Wilaya ya Chuo Kikuu
S.L.P. 35054,
DAR ES SALAAM.
Tanzania

****

Kamati ya Uhariri:

A.M. Moshi
F. Da Costa
L.A.M. Rugaikingira
A.J. Saffari
F.P. Shayo
E.T. Kisonga
N.N. Luanda
S.V. Lawa
A.S. Laiser
T.K. Ndibalema
Z.N.Z. Tumbo
S.S. Salehe
Maria Michael
I.L. Shirima

****

## Y A L I Y O M O

| | | Ukurasa |
|---|---|---|
| 1. | Tahariri | i |
| 2. | Uchambuzi wa Jumuia | 1 |
| 3. | Kuadimika kwa Bidhaa Nchini | 7 |
| 4. | Juu ya Suala la Dola | 9 |
| 5. | Kuhusu Nchi Zinazonyonywa Ulimwenguni | 21 |
| 6. | Ushairi na Ukasuku | 32 |
| 7. | Unyonyaji wa Wafanyakazi Chini ya Ubeberu | 52 |
| 8. | Ujamaa wa Kinjozi na Ujamaa wa Kisayansi | 57 |

****************

WAKULIMA NA WAFANYAKAZI ULIMWENGUNI,
UNGANENI!

HAMTAPOTEZA KITU ILA MINYORORO YENU

BALI ULIMWENGU WOTE UTAKUWA WENU

****************

MAWAZO YALIYOMO KATIKA MAKALA YALIYOCHAPWA KATIKA GAZETI HILI NI MAONI YA WAANDISHI WALA HAYAKUDHAMIRIWA KUWAKILISHA MAONI YA KAMATI YA WAHARIRI AU UMOJA WA VIJANA CHOU KIKUU

oooOOOoooo

## TAHARIRI

Katika makala ya Gazeti la Maji Maji Na. 30 tuliahidi kuendelea na uchambuzi wa falsafa ya kiyakinifu na falsafa ya kidhanifu katika kutanzua masuala ya jamii. Falsafa hizi mbili katika masuala ya uchambuzi huhitilafiana kata kata katika kubayinisha tafauti hizi itabidi kutoa mifano mbali mbali yenye kuhusu masuala ya jamii na kuona jinsi falsafa hizi mbili zinavyo kabili na kuchambua masuala hayo.

Moja ya suala la kitaifa linalokera wakulima na wafanyakazi wa nchi kama yetu ni umaskini wetu. Umaskini wetu unaelezeka katika tafauti kubwa ya mapato kati ya mkoa na mkoa; tafauti kubwa ya mapato kati ya tabaka na tabaka. Ingefaa kukumbuka hata mikoa yenye mapato madogo nayo ina "mamwinyi" wake. Jee falsafa za uchambuzi zinakabilije suala hili?

Mabingwa wa falsafa ya kidhanifu wangedakia suala hili kwa kusema kwamba Mungu ndiyo Muumba wa yote hivyo ameumba mikoa maskini na mikoa tajiri. Kadhalika Mungu kaumba tajiri na maskini. Wanakiri zaidi wa falsafa hii hueleza kwamba katika jamii ya watu wapo watu stadi, wajanja, waangalifu, wanaoona mbali, wanaojua kutengeneza hela" wakakusanya mapato haba na haba kisha baadaye wakatokea kuwa mamwinyi, matajiri wakubwa na "wazee wazito". Katika jamii hiyo hiyo wapo makachero, wapumbavu, wabadhirifu, walevi, wavivu, wazembe ambao hawaoni zaidi ya upeo wa pua zao ambao hula kila senti wanayopata bila ya kuelewa maana ya "haba na haba" wakaondokea kuwa maskini na makabwela mwaka nenda rudi hadi kiyama. Waledi wa falsafa hii husisitiza kwamba katika jamii mambo ndivyo yalivyo hivyo si shani kuweko na tabaka la matajiri na makabwela.

Katika uchambuzi wa falsafasa ya kidhanifu mabingwa wake husingizia suala la umaskini kwa kulihusianisha na mambo ya Mungu au mizimu au "hirizi". Kadhalika suala la umaskini hulihusinisha na tafauti za upeo wa bongo za binadamu au tafauti za asili za mwenendo na tabia za binadamu. Hukamilisha uchambuzi wao kwa kusema kwamba matajiri ni matajiri na makabwela ni maskini kwa kuwa hivyo ndivyo ilivyo! Jee huku si kukwepa ukweli wa mambo!

Je mabingwa wa falsafa ya kiyakinifu husema je kuhusu suala hili la umaskini? Falsafa ya kiyakinifu haihusianishi suala la kitaifa la umaskini na mambo ya Mungu au mizimu kwani suala hili hutokana na mfumo wa jamii tuliyonayo katika nchi kama yetu. Ipo hatari ya kuhusianisha masuala ya jamii na masuala ya Mungu au mizimu ambayo yanahusu zaidi "imani ya mtu binafsi". Kwa mfano kwa mtizamo huu tungeeleza suala la utumwa, ukoloni, ubeberu, unyonyaji na umaskini katika jamii kuwa ni masuala ya Mungu na mizimu. Hivyo kupambana na masuala haya ya udhalimu ni uasi kwa Mungu na Mizimu ambayo imani zetu binafsi zinakataza! Mtizamo wa aina hii unahalalisha utumwa, ukoloni, ubeberu, unyonyaji na umaskini.

Ni kwa sababu hii ambayo kwayo mtizamo wa kiyakinifu hubatilisha kata kata mtizamo wa kidhanifu. Hufanya hivyo kwanza kwa kuona kwamba suala la umaskini katika nchi kama yetu linaweza kuelezeka kutokana na hali halisi ya mfumo wa jamii katika siasa, uchumi na utamaduni.

Kwa ufafanuzi zaidi tunaona kwamba, mfumo wa uchumi wa taifa umenasishwa au umekwamishwa katika mfumo wa uchumi wa mataifa ya kibepari kwa kutumia soko la dunia la mabepari. Wakulima na wafanyakazi wa Tanzania mwaka hata mwaka huzalisha mali ili kuiwezesha jamii kuendelea, lakini sehemu kubwa ya utajiri hiporwa na mabeberu kwa kutuuzia nyenzo za uzalishaji mali kwa bei wanayotaka; kudai ruzuku na riba wanayotaka kwa mikopo wanayotupa; kulipa mishahara ya wataalamu tunaoazima kutoka kwao; kulipa ada za alama za biashara k.m. "Coca Cola". Kulipa ada kwa kupewa ruhusa kutumia muundo kutengeneza bidhaa fulani. Kulipa ada za "ushauri wa Kitaalamu" kutoka nje na gharama za usafiri wanazozitaka kwa kutumia vyombo vya mabepari kwa kusafirishia bidhaa zetu. Katika kiwango cha kimataifa umaskini wetu unasababishwa na unyonyaji wa kibeberu unaoendeshwa na mataifa yote ya kibepari ambao hupora sehemu ya utajiri unaozalishwa na wakulima na wafanyakazi mwaka hata mwaka.

Kulingana na mfumo wetu wa uchumi ndani ya taifa ugawanyaji wa ziada izalishwayo na jasho la wakulima na wafanyakazi kila mwaka hutegemea mamlaka na uwezo wa matabaka wa kuamua nani apate sehemu gani kulingana na ni nani anayemiliki njia kuu za uchumi, na nani anayeongoza mipango ya uzalishaji mali. Kulingana na kanuni ya uchumi, lile tabaka linalomiliki na kuongoza uzalishaji mali ndilo lenye uwezo wa kuamua mfumo wa ugawanyaji wa mapato ya taifa.

Kwa hiyo mfumo wa ugawanyaji mapato kama hauwapi wazalishaji mali uwezo wa kusimamia na kuongoza shughuli za uzalishaji pamoja na mfumo wa ugawanyaji wa mapato ndiyo chanzo kikubwa cha umaskini kwa matabaka ya wakulima na wafanyakazi ndani ya uchumi wa taifa lolote. Kwa mfano kama taifa linapanga kutumia sehemu kubwa ya mapato yake kustarehe badala ya kutumia mapato hayo kuendeleza viwanda ambavyo vinaongeza bidhaa za kuzalisha mali na bidhaa za matumizi ya kila siku ya tabaka la wakulima na wafanyakazi basi wakulima na wafanyakazi wanaweza kusakamwa na umaskini japo hata wakichapa kazi kwa juhudi kubwa.

Kwa ufupi ndivyo mtizamo wa falsafa ya kiyakinifu ungalilichambua suala la umaskini katika taifa liloonewa na kunyanyaswa na ubeberu kama letu. Ni katika kutambua tofauti hizi halisi ndipo tutakapoweza kuona ni falsafa gani itakayotuwezesha kuchambua jamii yetu ili tuweze kubayinisha njia za utatuzi wa matatizo hayo.

# UCHAMBUZI WA JUMUIA

## SEHEMU YA KWANZA : NGUVU ZA UZALISHAJI-MALI

### 1. Utangulizi

Jambo muhimu katika elimu ya siasa ni kujifunza ile misingi ambayo inatuwezesha kuchambua jumuia kisayansi. Sote tunajua kuwa jumuia zinatofautiana sana, jumuia ya Tanzania si sawa na jumuia ya China, au Marekani, au Afrika Kusini, n.k. wala jumuia ya Tanzania hii leo si sawa na Tanzania ya karne tatu zilizopita. Kuna mambo mengi yaliyo tofauti kati ya jumuia ya Watanzania na jumuia nyinginezo; utamaduni, siasa, uchumi, desturi na kawaida, na kadhalika.

Dhahiri mtu ukiulizwa kueleza kinaganaga tofauti kati ya jumuia moja na nyingine huwezi kuorodhesha mambo yote yanayozitofautisha jumuia hizo mbili. Sawa kama ungeambiwa kueleza tofauti kati ya "ring frame" na "kifaru" katika somo la ufundi-nguo hungetaja kila jambo lililotofauti kati ya mashine hizo mbili. Bila shaka ungezungumzia mambo yale yaliyo muhimu katika mashine hizo: kwanza kazi zake ni tofauti, kwani mashine moja ni ya kusokota nyuzi ambapo kifaru hufuma nguo, pili muundo wake ni tofauti kutokana na kazi zenyewe kuwa tofauti, na kadhalika. Bila shaka mwalimu hatafurahi kama badala ya kufanya hivi ungeanza kueleza jinsi rangi za mashine hizo zilivyo tofauti, kelele zake, uzito, n.k. Ingawa kweli mambo haya yote ni tofauti katika mashine hizo mbili, mambo hayo si ya msingi. Mambo ya msingi katika mashine ya "ring frame" na "kifaru" ni shughuli zifanywazo na miundo ya mashine.

Kadhalika katika suala la jumuia, tukitaka kueleza kwa ufasaha tofauti kati ya jumuia mbili yatupasa kubagua mambo yale yaliyo ya msingi kuhusu jumuia. Tusifanye kosa la kuchukua vitu vya juu-juu, kama vile "Wachina ni wakali kuliko sisi" ni "sisi ni weusi ndiyo maana hatuendelei", n.k. Misemo ya namna hii inafaa kilabuni tu; tukitaka maelezo murua itapasa tufanye uchambuzi wa kimsingi.

### 2. Uzalishaji-mali

Sasa ni mambo gani basi yaliyo ya msingi katika jumuia? Ingawa katika jumuia kama tulivyoona, kuna mambo mengi, kitendo kilicho cha msingi kabisa ni uzalishaji-mali. Hakuna jumuia inayoweza kuishi bila uzalishaji-mali. Jumuia yaweza kuwepo bila dini, bila ndoa, bila mchezo wa mpira, bila vyama vya siasa, n.k. Haya yote si ya msingi. Lakini uzalishaji-mali ndiyo hasa uti wa mgongo wa kila jumuia.

Kwa hiyo basi tukitaka kuielezea jumuia yoyote ile itatupasa tuliangalie kwanza kabisa suala la uzalishaji-mali. Huu ndio ufunguo wa kuelewa mambo mengine yote; bila kulielewa vyema suala hili hatuwezi kamwe kuyaelewa mambo mengine yaliyo katika jumuia.

Bila shaka ni dhahiri kwa nini uzalishaji-mali ni msingi wa kila jumuia. Binadamu hawezi kuishi bila kupata mahitaji fulani-fulani, hasa yale mahitaji ya lazima kabisa: makazi, mavazi, na chakula. Na sote tunajua kuwa mahitaji haya hayapatikani bila kazi - yaani vitu vinavyotosheleza mahitaji haya yote lazima vizalishwe kwa kazi. Ndiyo maana kabla ya kufanya jambo lolote lile jingine (k.m. kujishughulisha na siasa, utamaduni, dini, n.k.) binadamu lazima kwanza ajishughulishe na uzalishaji-mali. Baada ya kushiba, kuvaa, na kupata pahali pa kujisitiri ndipo atafikiria kusimama jukwaani kupiga siasa, au kuhutubia kuhusu uzuri wa kwenda mbinguni, na kadhalika.

Kwa hiyo basi, tukitaka kulinganisha jumuia mbili, au tukitaka tu kuichambua jumuia fulani, itatupasa kulizingatia swala la uzalishaji-mali.

3. Nguvu za Uzalishaji-mali

Uzalishaji-mali ni maingiliano kati ya binadamu na mazingira kwa jinsi ambayo binadamu huyakabili mazingira hayo ili yaweze kutosheleza mahitaji yaki. Ili kupata chungu cha kupikia, k.m., binadamu huubadili udongo (mazingira) hadi ukawa chombo kiitwacho chungu. Kadhalika hubadili pamba ikawa shati la kuvaa, hubadili majani ya mhogo yakawa kisanfu cha kula, hubadili ngozi ikawa viatu vya kuvaa, na kadhalika. Kitendo cha uzalishaji-mali ni kitendo ambapo binadamu hubadili mazingira yake na matokeo ni kitu chenye mafao.

Katika kuyabadili mazingira, aghalabu binadamu hutumia kifaa fulani. Ili kugeuza majani ya mhogo yawe kisanfu, mtu hutumia mwiko (pamoja na vifaa vingine); ili kuigeuza pamba iwe nyuzi mtu hutumia "spindles", na kadhalika. Vifaa vyote ambavyo binadamu huvitumia katika kuyabadili mazingira ili yaweze kutosheleza mahitaji yake tunaviita ZANA ZA KAZI.

Dhahiri, zana za kazi hutofautiana sana katika maendeleo yake. Mvuvi ni mvuvi, lakini mvuvi mwenye ndoano si sawa na mvuvi mwenye nyavu, ambaye naye si sawa na mvuvi mwenye meli maalum iliyoundwa kwa ajili ya kuvulia samaki. Ufanisi wa wavuvi hawa utatofautiana sana, yule mwenye zana za kisasa zaidi atapata mazao mengi zaidi kuliko yule atumiaye zana zisizoendelea. Mwenye jembe la mkono ni mkulima sawa na yule mwenye trekta, lakini mazao wazalishayo wakulima hao wawili ni tofauti sana.

Kwa hiyo basi, jumuia itumiayo zana za kisasa katika uzalishaji-mali haiwezi kuwa sawa na jumuia itumiayo zana za enzi za kale. Nchi ambayo watu wake ni wakulima watumiao majembe ya mkono si sawa na nchi ambayo watu wake ni wakulima sawia lakini watumiao trekta na mashine nyingine za kisasa. Kutokana na ufanisi kuwa tofauti, mambo mengine mengi ya kiuchumi na kijamii yatakuwa tofauti baina ya jumuia hizo mbili. Baadaye tutafafanua jinsi mambo hayo mengine yanavyotofautiana kutokana na zana za kazi kuwa tofauti.

Licha ya zana za kazi, jambo jingine linaloweza kutofautisha jumuia mbili katika uzalishaji-mali ni IDADI YA WAFANYAKAZI waliopo katika kila jumuia. Hata kama sis na majirani zetu sote hutumia majembe ya mkono, lakini sisi katika nchi yetu watu wawezao kufanya kazi ni elfu tano tu na majirani zetu ni milioni tano, uwezo wetu wa kazi hauwezi kuwa sawa na ule wa majirani zetu. Wao kutokana na idadi yao kubwa wana wasaa mkubwa zaidi wa kugawiana kazi, kushirikiana katika makundi makubwa, kupeana mawazo, na kadhalika.

Ni wazi kuwa tunapozungumza kuhusu idadi ya wafanyakazi tunamaanisha jumla ya wale wote wenye uwezo wa kuzalisha mali. Huwezi ukasema idadi ya wafanyakazi Tanzania ni milioni 15, ambapo idadi hiyo ni pamoja na watoto mamilioni wasiozalisha chochote. Kwa hivi, jumuia ambayo ina sehemu kubwa zaidi ya watoto miongoni mwa wananchi wake haiwezi ikawa na uwezo sawa wa kuzalisha na jumuia ambayo ingawa idadi ya wananchi ni ile ile, asilimia ya watoto ni ndogo.

Jambo kuu la tatu ni UJUZI. Mbali ya zana za kazi na idadi ya wafanyakazi, ujuzi nao huweza kutofautisha sana hali ya uzalishaji-mali - na hivyo kutofautisha jumuia moja hadi nyingine. Pahali ambapo wananchi wana ujuzi mwingi

hapawezi kuwa sawa na pahali ambapo wananchi hawana ujuzi wowote - hata kama idadi zao ni sawa na zana watumiazo ni sawa vile vile.

Suala la ujuzi linaambatana sana na suala la zana za kazi. Kama zana zilizopo katika jumuia ni za kisasa, basi ujuzi nao utalingana na matumizi ya zana hizo. Haiwezekani kukawa na ujuzi wa matumizi ya mashine za kisasa kama mashine hizo bado hazipatikani - kama ujuzi huo umeenea katika jumuia basi ni kwa kuwa zana zinazohusika nazo zimeenea katika jumuia hiyo.

Kwa ufupi basi, mambo haya matatu; zana za kazi, idadi ya wafanyakazi na ujuzi uliopo katika jumuia ndiyo hasa kitovu cha kila jumuia. Mambo haya matatu kwa pamoja huitwa NGUVU ZA UZALISHAJI-MALI.

Jumuia hutofautiana hasa kutokana na maendeleo ya nguvu za uzalishaji-mali. Na maendeleo ya kweli ni maendeleo ya nguvu za uzalishaji-mali. Kwa hivi tukitaka kuchambua jumuia yoyote ile jambo la kwanza ambalo yatupasa kuchunguza ni kiwango kilichofikiwa na nguvu za uzalishaji-mali na jinsi nguvu hizo zinavyozidi kusonga mbele (yaani ni kwa kiasi au pole pole, n.k.)

4. Mwisho

Kama ungeambiwa kuelezea hali halisi ya Tanzania na ukaamua kufuata ufafanuzi wa kisayansi kwa kuanza na suala la uzalishaji-mali, na hivyo kuchunguza kwanza njia za uzalishaji-mali, bila shaka hungeweza kutaja zana zote zinazotumika hapa nchini. Jukumu lako ingekuwa kuelezea hali ya wastani ilivyo kijumla kuhusu nguvu za uzalishaji-mali. Kama ungemweleza mtu kuwa hapa nchini kuna mitambo, matrekta, maplau, majembe, mashoka, misumeno, n.k. hangepata sura kamili ya nchi hii ~~kuweza~~ kuitofautisha na nchi nyingine.

Maelezo yako yangemwelea zaidi kama ungesema hapa nchini kuna kiasi cha watu milioni sita wawezao kufanya kazi, na walio wengi kati yao (kiasi cha asilimia 75) ni wakulima wadogo-wadogo watumiao majembe ya mkono bila ujuzi wa hali ya juu kwani walio wengi hata kusoma na kuandika hawajui. Kuna wakulima wachache ambao wana plau na trekta, lakini zana za kisasa kama hizi zinapatikana katika mashamba ya mabepari au ya serikali tu. Mijini kuna viwanda vichache vidogo-vidogo vitengenezavyo bidhaa za matumizi ya kila siku, navyo hutumia zana ziagizwazo ng'ambo. Ujuzi wa wafanyakazi viwandani vile vile bado mdogo na hivyo ufanisi bado katika ngazi ya chini.

Maelezo haya si kamili na ungeweza kuyapanua zaidi. Lakini angalau yanampa mtu picha ya jumla ya jumuia unayoizungumzia kabla hajaanza kukuuliza maswali mengine.

Kwa kumalizia sehemu hii basi, tukumbuke kuwa katika jumuia kuna mambo mengi lakini baadhi yake ni muhimu zaidi. Wajibu wetu ni kuyafafanua hayo yaliyo muhimu na kuacha pembeni yasiyo muhimu. Suala la uzalishaji-mali ndiyo la kwanza, na hivyo lazima tulichambue kwanza suala hilo kila tunapoangalia jumuia yoyote ile.

## SEHEMU YA PILI : MAHUSIANO YA KIUCHUMI

1. Ziada

Katika sehemu ya kwanza tumeona kuwa uzalishaji-mali ndiyo hasa kiini cha jumuia ya binadamu, na hivyo tukasema ikiwa tunataka kuichambua au kuielewa jumuia yoyote ile sharti tuchunguze kwanza suala hili la uzalishaji-mali. Kisha tukaonyesha kuwa katika kulichunguza suala la uzalishaji-mali jambo la kwanza la kuangalia ni hali ya nguvu za uzalishaji-mali katika jumuia - yaani kiwango cha maendeleo

[illegible]

[illegible]

[illegible]

[illegible]

[illegible] [illegible]

[illegible]

[illegible]

[illegible]

[illegible]

kazi. Kama ardhi na vifaa vya kilimo vitamilikiwa na kikundi fulani basi kikundi hicho kinaweza kuishi bila kufanya kazi na kikundi kingine cha watu wasiokuwa na njia hizo kitapaswa kutumia hizi zinazomilikiwa, na hapo kwa ajili ya kuzalisha kwa kutumia njia zilizo miliki ya wengine watu wafanyao kazi wawaachie ziada itakayopatikana hao wenye njia za uzalishaji-mali.

Huu ndio msingi wa MATABAKA katika jumuia. Matabaka ni makundi makubwa ya watu ambayo yanahitilafiana katika uhusiano wake na njia za uzalishaji-mali kwa jinsi ambavyo kundi moja linamiliki njia za uzalishaji-mali ambazo zinatumiwa na kundi la pili na kwa ziada inayozalishwa na kundi la pili inachukuliwa na kundi lile la kwanza.

Matabaka huweza kujengeka wakati ule tu jumuia imepata uwezo wa kuzalisha ziada, kabla ya hapo yanawezekana kuwa na tofauti mbali mbali baina ya watu lakini haziwezi kuwa tofauti za kitabaka. Suala la matabaka ni suala la uzalishaji-mali, suala la umilikaji njia za uzalishaji-mali na kutomiliki njia za uzalishaji-mali. Hivyo tusilichukulie kama tofauti za kipato wafanyakazi wawili wanaweza kutofautiana ujira, hii haimanishi wao ni matabaka mawili la hasha! Mradi wote wawili ni wazalishaji katika njia za uzalishaji wasizomiliki, basi wako katika tabaka moja, tabaka la wafanyakazi. Ndivyo ilivyo kwa mabepari; huyu aweza kuwa anachota ziada ya shilingi milioni moja kwa mwezi, na mwingine anachukua elfu kumi kwa mwezi. Ingawa wanatofautiana katika kipato, kwa kuwa wote wawili kipato chao ni ziada waichukuayo kwa ajili ya kumiliki kwao njia za uzalishaji-mali basi wote wako katika tabaka moja: tabaka la mabepari.

3. Unyonyaji

Pindi ikiwezekana kikundi kimoja kuishi kwa kutegemea ziada inayozalishwa na kikundi kingine kwa ajili ya kumiliki njia za uzalishaji-mali basi hapo ndipo panakuwapo UNYONYAJI: Unyonyaji ni kile kitendo cha tabaka moja kuondosha ziada inayozalishwa na tabaka jingine kwa kumiliki njia za uzalishaji-mali zinazotumiwa na tabaka linalozalisha. Mitaani neno hili "UNYONYAJI" hutumiwa bila misingi - kisayansi unyonyaji ni suala la kitabaka, mfanyakazi hawezi kumnyonya mfanyakazi kwani mfanyakazi hamiliki njia za uzalishaji-mali na hivyo kutorosha ziada.

Ni kweli mtu aweza kumpunja au kumtegea mwenzie, lakini tunapozungumza kuhusu suala la unyonyaji sharti tuchukue maana fasaha ya kisayansi. Tabaka limilikalo njia za uzalishaji-mali ndilo liwezalo kunyonya tabaka lisilomiliki njia hizo ingawa linazitumia katika kazi. Ndiyo kusema haiwezekani wafanyakazi wakawanyonya mabepari, kwani chochote wachukuacho wafanyakazi (hata kama kikiwa kikubwa namna gani) hutokana na kazi yao wenyewe, na chochote wachukuacho mabepari (hata kama kikiwa kidogo namna gani) lazima ni ziada iliyozalishwa na wafanyakazi.

Wala haiwezekani matabaka yakawapo bila unyonyaji kuwepo, au unyonyaji ukawepo bila matabaka kuwepo pia. Kama tulivyokwisha kuona, kuzalishwa kwa ziada ni ufunguo wa kuzaliwa kwa matabaka, na matabaka hayawezi kuwepo bila tabaka moja kutorosha ziada inayozalishwa na tabaka jingine. Hivyo matabaka na unyonyaji ni kama pande mbili za kitu kile kile kimoja, matabaka hayafutiki kama unyonyaji upo na unyonyaji hauwezi kuondoshwa kama matabaka yapo.

4. Mahusiano katika Jumuia

Suala hili la matabaka na unyonyaji ni muhimu sana, na hivyo katika somo lingine tutalizungumzia kwa kirefu zaidi ili tuweze kuyaelewa vyema mapana na marefu ya suala zima. Pindi jumuia ikisha kugawanyika katika matabaka, basi jumuia nzima inabadilika kwani vipengele vingi sana vinabadilika. Kadhalika, kufuatana na aina za matabaka zilizopo katika jumuia yoyote ile ndivyo hali za maisha zinavyokuwa tofauti. Mahusiano waliyo nayo watu katika jumuia hufuatia suala la umilikaji wa njia za uzalishaji-mali na ugawaji wa ziada.

Tulielezea pale kwanza kuwa matabaka ni makundi yanayotofautiana katika uhusiano wake na njia za uzalishaji-mali: wamilikaji wa njia hizo (ambao ndio watoroshaji wa ziada) na wasiomiliki njia hizo lakini huzifanyia kazi (ambao ndio wazalishaji wa ziada). Mahusiano yaliyopo miongoni mwa watu kufuatia suala la njia za uzalishaji-mali na suala la ziada yanaitwa MAHUSIANO YA KIUCHUMI.

Tunajua kuwa miongoni mwa watu kuna mahusiano mengi mbali mbali na hivyo kuna makundi mengi mbali mbali. Kuna makundi ya kisiasa, kiutamaduni, kifamilia, kidini na kadhalika, haya yote ni makundi yanayowakilisha mahusiano ya kisiasa, kiutamaduni, kifamilia, kidini na kadhalika. Lakini haya yote kwa pamoja yana msingi wake, nao ni mahusiano ya kiuchumi au mgawanyiko katika makundi kufuatia suala la njia za uzalishaji-mali na ziada. Mahusiano ya kiuchumi ndicho kitako cha kila jumuia, yakibadilika mahusiano mengine yote nayo hubadilika.

Ndiyo maana kuna mifumo mbali mbali ya kisiasa, kiutamaduni, na kijamii kufuatia tofauti zilizopo katika mahusiano ya kiuchumi. Siasa au utamaduni katika jumuia ya kibepari haviwezi kuwa sawa na siasa au utamaduni katika jumuia isiyo ya kibepari. Katika somo lingine tutaelezea kwa mifano jinsi mahusiano ya kiuchumi yanapobadilika mahusiano mengine hayo yana badilika - jinsi mgawanyo wa matabaka unavyobadilika na mgawanyo wa makundi ya siasa, utamaduni, na kadhalika, unabadilika nao.

Kwa kweli si mahusiano ya watu tu ndiyo yanayobadilika kufuatana na mahusiano ya kiuchumi yaliyopo, bali hata fikra na imani za watu hutegemea sana mahusiano ya kiuchumi. Fikra na imani za watu katika jumuia yenye matabaka haziwezi kuwa sawa na fikra na imani za watu katika jumuia isiyojua matabaka; kadhalika fikra na imani za watu katika jumuia yenye matabaka ya aina fulani haziwezi kuwa sawa na fikra na imani za watu katika jumuia yenye matabaka tofauti.

Kwa hiyo basi, mahusiano ya kiuchumi ndiyo hasa kitako cha kila jumuia. Katika sehemu ya kwanza tulisema kuwa jambo la kwanza inatupasa kuliangalia tukitaka kuchambua jumuia ni nguvu za uzalishaji-mali. Katika sehemu hii ya pili tumeona kuwa jambo la pili ni mahusiano ya kiuchumi. Kwa kuchunguza mambo haya mawili tutakuwa tumeanza kuielewa jumuia yoyote ile kwa misingi ya sayansi.

*********************

# KUADIMIKA KWA BIDHAA NCHINI

## (HII NI TAFSIRI YA MAKALA YALIYOCHAPISHWA KATIKA GAZETI LA DAILY NEWS)

Ni kawaida kwamba matatizo mbali mbali ya kijamii, kisiasa na kiuchumi huwaangukia watu wa jumuia moja kwa vishindo tofauti kufuatana na sehemu walizoko. Upungufu wa bidhaa za matumizi ya kawaida, kwa mfano, hauwezi ukawahusu watu wote kwa njia ile ile - wengine wataumia zaidi, wengine wataumia kidogo tu, na wengine hata wanaweza wakanufaika kutokana na upungufu huo. Katika makala haya hatujaribu kuchunguza sababu ziletazo upungufu na kuadimika kwa vitu bali tutajaribu kuangalia jinsi kuadimika huko kunavyoyahusu makundi tofauti ya watu.

Kwanza lazima tutofautishe baina ya aina mbili za upungufu wa bidhaa. Kuna uadimikaji wa bidhaa za anasa ambazo hutumiwa na matajiri na pili kuna uadimikaji wa bidhaa za matumizi ya lazima ambazo hutumiwa na wananchi wa kawaida. Mathalan, kwa miaka kadhaa magari madogo, radio gram, friji, vinywaji vikali vitokavyo Ng'ambo, mashine za kunasia sauti, n.k., vimekuwa vikizidi kuadimika kutokana na hali mbaya ya kiuchumi inayohusiana na upatikanaji wa fedha za kigeni. Hii haimanishi kuwa matabaka ya watu tajiri hayapati bidhaa hizo. Kutokana na uwezo wao, wao wanaweza kabisa kupata bidhaa hizi hata kama kibiashara haziletwi kwa wingi au zimezuiwa kabisa.

Watu wakubwa katika pilika-pilika zao za kwenda na kurudi kwenye mikutano, semina, n.k. huko Ng'ambo wanaweza kurudi na bidhaa kemkem na anasa zisizopatikana hapa nchini. Tena vitu hivyo huviingiza nchini bila hata ya msukosuko wa ushuru kwani au ni watu wenye madaraka au wana fedha za kulipa hongo kwa maafisa wanaohusika. Kadhalika hivi majuzi kumezuka njia nyingine tena ya kupatia bidhaa za anasa zisizo madukani: bidhaa hizo huletwa na watumishi wa kigeni ambao pindi wakimaliza mikataba yao huviuza vitu hivyo kwa wakazi wa hapa kwa bei aghari zinazonunuliwa na watu wakubwa tu au wafanya-biashara wenye utajiri mkubwa. Ukiangalia kurasa za gazeti la "Daily News" huwezi kukosa kuona matangazo ya uuzaji vitu vya aina hii.

Kwa hivi wakubwa kwa kweli hawana habari na suala la upungufu au kuadimika kwa bidhaa, pamoja na bidhaa za anasa. Ni wananchi wa kawaida ndio wasumbukao na uhaba wa bidhaa mbali mbali. Kwa hivi suala la upungufu wa vitu ni suala la kitabaka, inategemea wewe uko tabaka gani ndipo utateseka au hutateseka na tatizo hili la upungufu wa bidhaa.

Hebu sasa tuangalie swala la uadimikaji wa bidhaa za lazima katika jumuia. Katika muda wa zaidi ya miaka minne sasa, upungufu wa bidhaa za lazima kwa maisha ya wananchi umekuwa ukongezeka siku hata siku. Mara kwa mara kumekuwa kukitokea upungufu wa vitu kama sukari, mafuta ya kupikia na ya taa, sabuni zakufulia na kuogea, n.k. Hii ni hali ambayo mtu analazimika kuishi nayo siku hizi. Tatizo la sukari kwa mfano, lilianza kama mzaha: wakati mwingine sukari ipo, wakati mwingine haipo, na vivyo hivyo. Wakati mwingine sukari ilipotea kabisa hata tukaambiwa kuwa imeagizwa Ng'ambo, kwa ghafla tukaona imejaa madukani kisha ikatoweka tena na baada ya wiki mbili - tatu ikazuka tena kwa ghafla vile vile.

Hata katika kipindi hiki ambapo sukari huwa haionekani, ni wananchi ndio wanaosumbuka. Wakubwa wao huipata bila shida. Wao hawajipangi foleni, kwa kutimia fedha na madaraka yao huwekewa sukari, au nyama au mafuta, n.k. kwa kiasi cha chote wapendacho.

Njia moja ambayo hutumiwa na wakubwa kupunguza idadi ya wananchi wanaotumia bidhaa fulani ni kuongeza bei ya bidhaa hizo. Sukari yaweza kuuzwa kwa Shs. 2/50 kwa kilo, watu wengi wakawa wanainunua, ili kuhakikisha kuwa misururu inapungua wakubwa wanaweza wakapandisha bei hadi kufikia Shs. 5/- kwa kilo. Hapo sehemu fulani ya wananchi itapasa waache kutumia bidhaa hiyo na kuwaachia wakubwa fursa ya kupata sukari. Hizi ni mbinu za matabaka yote ya kinyonyaji kuwakomoa wananchi. Kwa kupandisha bei, wananchi hulazimika kupunguza matumizi ya bidhaa zinazohusika na kwa hivi kwa kweli huwa wamepunguza hali zao za maisha na kuwa za chini zaidi, kitu ambacho dhahiri hatuwezi kukiita cha kimaendeleo - ni hatua ya kipinga-maendeleo.

Kama tulivyoona, wanaohusika na kupungua huku kwa hali za maisha ni wale K.C.C. (Kima Cha Chini) kama wanavyoitwa siku hizi, wakubwa hawapunguzi matumizi ya sukari kwa kuwa imepanda bei - watatafuta njia za kuongeza kipato chao au hata za kuipata sukari hiyo bure. Lakini wananchi wa kawaida itapasa wapunguze matumizi hayo, na mara nyingine kuacha kabisa. Na watu wakiacha kutumia sukari, au nyama, n.k. dhahiri miili yao inakosa vitamini muhimu - ndiyo maana baada ya miezi michache wanaanza kumiminika hospitali wakiwa wanaumwa maradhi chungu nzima. Huko hospitali nako watakuta upungufu wa dawa, vitanda, chakula, n.k. ambapo wakubwa wakiungua watapata huduma kemkem bila shida.

Sasa tunapozungumza kuhusu wananchi kupata taabu tunamaanisha nani hasa? Matabaka yanayohusika katika kundi hili la "Wananchi" kwanza kabisa ni wafanyakazi (yaani wale wanaouza nguvu zao za kazi kwa ujira si pamoja na wale wanaopata mishahara kutokana na madaraka yao dhidi ya wale wafanyao kazi), wakulima, na vibwenyenye vya ngazi ya chini (mathalan makarani, wapiga-chapa, n.k.). Hawa wote ndio "Wananchi", na ndio wanaoteseka kutokana na upungufu wa bidhaa muhimu za maisha. Maafisa ambao siku hizi hujiita 'wafanyakazi', jambo ambalo si la kweli, hawapati shida hizi - wao hata kama nyama ikiadimika wanaweza kuifuata hata Kibaha kwa gari la serikali na dreva (mfanyakazi) wa serikali.

Hapo zamani watu walikuwa wanajaa sana katika hoteli za chips na samaki wakati wa mchana, siku hizi ni maafisa ndio waendao huko kila mara. Wananchi huenda magengeni au kuzurura tu kusubiri saa ya kurudi kazini. Makarani walizoea kula nyama, siku hizi utakuta vipande vya mbatata na punje za maharage. Hii ndiyo milo yao ya sasa.

Kisha, siku hizi vile vile kumekuwa na upungufu wa nguo - hasa khanga na vitenge, japo inajulikana kuwa bidhaa hizo zinauzwa Ng'ambo. Ni mambo yatokanayo katika ubeberu ndipo bidhaa zitengenezwazo nchini huweza kuadimika humo nchini na zikapatikana Ng'ambo kwa urahisi au zile zinazobakia nchini zikawa ni zile hafifu na nzuri zote wakapelekewa watu wa nje. Wakati mwingine khanga nzuri hubidi ziingizwe nchini magendo huku zimetengenezwa hapa hapa nchini.

Kwa ufupi basi, jambo tunalosisitiza ni kwamba upungufu wa bidhaa si tatizo la "Kitaifa" au la "nchi", ni tatizo la kitabaka: linatokana na unyonyaji wa tabaka moja dhidi ya tabaka jingine. Kwa hiyo tukitaka kulielewa vizuri, sharti tuchunguze jinsi harakati za kitabaka zinavyokwenda katika jumuia yetu. Vitu vinaweza kuwa vichache kwa watu wa tabaka fulani na wakati huo huo vikawa ni vingi sana kwa watu wa tabaka jingine.

# JUU YA SUALA LA DOLA

Na: K. KUJALI

## Mwanzo wa dola*

Katika jamii wa kisasa, dola si jambo ambalo linazungumzwa sana au linapiga mshangao wowote kwa sababu tunachukulia dola kama ni kitu cha kawaida ambacho lazima kiwe miongoni mwa jamii yoyote ile. Hii inaonyesha jinsi mtazamo na falsafa ya kibwenyenye - ambayo ni mojawapo ya mitazamo muhimu miwili inayotawala ulimwenguni kimawazo - ulivyoenea katika badhi ya watu ulimwenguni. Mtazamo wa kibwenyenye huchukulia utaratibu na mfumo wa kibwenyenye kama ni mfumo ambao umekwepo tangu zamani za kale na utaendelea milele na milele. Ukweli ni kwamba hayo ni mawazo ya kitabaka pekee na ya kiitikadi wala siyo sahihi kisayansi hata kidogo. Kwa sababu tukichambua jamii za kale tutatambua kwamba mwanzo wa dola unaambatana na mwanzo wa mgawanyiko wa jamii katika matabaka. Ni wazi kwamba katika jamii nyingi za kale ambazo zilikuwa bado hazijawa na matabaka, dola halikuwepo wala halikuhitajika. Mgawanyiko katika matabaka ya kihasama kwa mara ya kwanza inaweka mazingira ambayo ni lazima kuwa na dola.

Jamii iliyogawanyika katika matabaka yanayozalisha mali na yale yasiyozalisha mali ni jamii iliyokabiliwa na migongano ya kihasama. Tabaka (au matabaka) linalojinufaisha kutokana na mgawanyiko huu, yaani linolonyonya haliwezi kuaachia migongano hii ivuruge utaratibu wa unyonyaji. Kwa hiyo tabaka hilo linafanya njama zote na linachukua hatua zote za kukusanya <u>NGUVU</u> na uwezo wa nguvu zote katika chombo kimoja - na chombo hicho ni dola. Dola linakuwa ni chombo ambamo zimekusanyika nguvu zote za ukandamizaji wa wale wanaonyonywa. Kwa mara ya kwanza matumuzi ya nguvu yanakuwa marufuku kwa mwananchi yeyote yule ila ni dola tu. Naiyo kusema dola lililokomaa linamiliki silaha n.k. kwa niaba ya tabaka linalotawala dhidi ya matabaka yanayotawaliwa na pia dhidi ya matabaka mengine maadui kutoka nchi za nje. Isitoshe, matumizi ya nguvu dhidi ya mtu binafsi pia yanakuwa ni uwezo wa dola tu - na vyombo vyake - na ni marufuku kwa mtu ye yote mwingine.

Kwa ufupi, tumeona kwamba dola ni matokeo ya jamii iliyogawanyika katika matabaka na wala halikuwepo tangu zama za kale wala halitaendelea kuwepo milele na milele. Dola ni chombo ambamo zimekusanyika nguvu zote kwa niaba ya tabaka linalonyonya dhidi ya matabaka yanayonyonywa.

Kwa hiyo, tukiangalia historia, tunaona kwamba mifumo ya kitabaka kama utumwa na ubepari ndio mifumo ambayo yote imekuwa na dola kwa sababu mifumo hii yote imegawanyika katika matabaka ya kihasama.

Dola la kibwenyenye ambalo ndilo la aina iliyopo katika nchi nyingi za ulimwengu leo, ni matokeo ya historia ndefu. Ni dhahiri kwamba muundo wa dola umendelea kukuwa tangu enzi za ut.. hadi leo. Dola katika enzi ya utumwa na ukabaila ulikuwa bado kitu changa. Chini ya ukabaila, kwa mfano, vilikuwepo vijidola vidogo vidogo vikitumikiwa na mamwinyi mbali mbali. Ni mapinduzi ya kibwenyenye dhidi ya utawala wa kikabaila katika nchi za Ulaya Magharibi ndiyo uliyojenga kwa mara ya kwanza dola kuu moja la kitaifa. Dola la kibwenyenye ni dola la hali ya juu kabisa lililokuwa na nguvu kupita madola yote ya hapo awali. Ni dola la aina hii linatukabili ulimwenguni leo; ndio maana ni muhimu sana kuzieleza sifa za dola la kibwenyenye.

* Kuhusu maelezo ya maneno 'dola','nchi', 'taifa' na 'serikali', angalia uk. 20

II. Dola la kibwanyenye

Nchi za Ulaya Magharibi, Uingereza na Amerika Kaskazini ni nchi zenye ubepari ulioendelea. Nchi za 'dunia ya tatu' yaani Afrika, Asia na Amerika Kusini ndizo nchi za ubepari uliovia. Na nchi hizo za pande mbili pamoja ndizo zinaunda mfumo wa kibepari ulimwenguni.*

Kurahisisha maelezo vangu juu ya suala la dola la kibwanyenye, nitazungumzia dola la kibwanyenye kinadharia (nadharia iliyotokana na historia halisi ya madola haya ya kibwanyenye) na sio dola hasa ya nchi maalum. Hata hivyo tunaweza kusema kwamba madola ya nchi hizo za ubepari ulioendelea yana sifa zote kuu za dola la kibwanyenye nitakaloelezea ingawa sifa za kisiasa za madola hayo zinatofuatiana.

Katika nchi ya kibepari halisi yapo matabaka mawili makuu - mabwenyenye na maproletari. Tabaka la kibwanyenye ndilo lina-miliki njia za uzalishaji mali. Mabwenyenye ndio huajiri wafanyakazi katika viwanda na mashirika yao. Kufuatana na utaratibu wa kibepari, ujira anaopata mfanyakazi ni kiasi cha kutosheleza mahitaji yake ya lazima tu. Lakini mfanyakazi huzalisha bidhaa ambazo zina thamani zaidi ya mahitaji yake. Hiyo inamaanisha kwamba sehemu ya kazi aliyofanya mfanyakazi hailipiwi na ndio chanzo cha faida ya bepari. Kitu ambacho huuzwa na mfanyakazi anapo ajiriwa na bepari sio kazi lakini uwezo wake wa kazi. Ndio maana bepari anaweza kumfanyisha kazi zaidi ya ile ambayo ni ya lazima kutosheleza mahitaji ya mfanyakazi mwenyewe kwa sababu amenunua uwezo na sio kazi ya mfanyakazi. Kwa mfano, bepari ameajiri mfanyakazi kwa masaa manane kwa ujira wa shillingi 200/=. Hii inamaanisha kwamba mfanyakazi huyu ameuza uwezo wake au nguvu zake za kazi kwa masaa manane. Lakini kazi ambayo ni lazima afanye kutosheleza mahitaji yake labda inatakiwa masaa manne (4) tu. Sasa ujira anaopewa unatosha kwa mahitaji yake tu. Na kama nilivyokwisha sema, mahitaji haya ni sawa na kazi ya masaa manne. Kwa kifupi, matokeo ya uhusiano huu ni kwamba mfanyakazi anafanyakazi kwa masaa manane (8) lakini anapewa ujira wa masaa manne (4) tu. Kwa hivyo kazi ya masaa manne mengine ni ziada ambayo inachukuliwa na bepari. Ziada ya aina hii huitwa THAMANI-ZIADA. Ni wazi kwamba katika mfumo huo wa ubepari mfanyakazi ni mzalishaji ziada na bepari ni myonyaji. Ndiyo maana utaratibu huo kamwe hauwezi kuwa na usawa.

Licha ya matabaka hayo mawili katika mfumo huo wa kibepari, pia kuna matabaka na vijitabaka vingine. Lakini matabaka mawili niliyotaja ndiyo hasa msingi maalum wa jamii ya kibepari. Kwa hiyo basi katika jamii hii dola linadhihirisha mahitaji ya tabaka la kibwenyenye kwa jumla. Ndiyo kusema dola si chombo cha jamii kwa jumla au cha umma kwa sababu jamii yenyewe imegawanyika katika matabaka. Yapo matabaka yanayonyonywa na yale yanayonyonya na kutawala kisiasa. Tabaka (au matabaka) linalotawala ndilo linalotumia dola kujinufaisha lenyewe. Katika jamii ya kibepari, ni tabaka la mabwanyenye ndilo linalotawala kiuchumi na kisiasa na hushika nguvu za kidola. Kwa hiyo ni dhahiri kwamba katika jamii ya kitabaka dola silo kitu ambacho hakifungamani na tabaka lolote. Pia dola hali hudumii wananchi wote kwa usawa kwa sababu jamii yenyewe ni jamii ya kutokuwa na usawa - jamii ya kitabaka.

Hebu tuangalie sasa ni nini kazi mbalimbali za dola ambazo zinakuza mfumo wa kibepari.

* Hapo hatuhesabu nchi za kikomunisti.

Kwanza kabisa ni lazima jamii ya kibepari kuwepo utaratibu maalum wa kiuchumi na wa kisheria kuhakikisha kwamba unyonyaji wa kibepari unaendelea bila matatizo na mvurugo. Kwa mfano, kama tulivyokwishaona kiini cha ubepari ni uhusiano kati ya mfanyakazi na bepari. Ni mfanyakazi ambaye ni mzalishaji thamani-ziada ambayo inachukuliwa na bepari. Kulinda, kuimarisha na kuendeleza uhusiano huu ni kazi mojawapo muhimu ya dola. Hiyo maana dola linaweka sheria kadha wa kadha, kama sheria za kazi, za mkataba n.k. Kwa hiyo, wakati mfanyakazi anapoajiriwa na bepari, kisheria wamefanya mkataba wa kazi na ni kinyume cha sheria kuwa upande wowote kuvunja mkataba huo. Hapo linakuja swali, Je, kama dola ni chombo cha mabepari, vipi bepari pia, ikawa amevunja mkataba tunaozungumzia anaweza kuchukuliwa hatua za kisheria na kufikishwa mahakamani? Sio haya tu, lakini ikionekana kwamba ana hatia, anaweza kuhukumiwa na kupewa adhabu kama mwananchi mwingine. Ni kweli kwamba hii inawezekana na hata kama sio mara nyingi mabepari kama watu binafsi huadhibiwa na vyombo vya dola. Je, hiyo inamaanisha kwamba dola si chombo cha mabepari? La, hasha! Kwa sababu, dola si chombo cha bepari kama mtu binafsi bali ni chombo cha tabaka la mabepari kwa jumla. Kwa kweli, ni kazi mojawapo ya dola kuhakikisha kwamba mabepari wenyewe hawaibiani wao kwa wao na wanatatua hitilafu miongoni mwao kwa utaratibu uliopangwa bila mvurugo mkubwa. Mvurugo mkubwa unaweza kuhatarisha utawala wa tabaka la mabwenyenye kwa jumla na huenda hata kupatia nafasi tabaka la wafanyakazi kujaribu kufanya mapinduzi. Isitoshe, kama nilivyoeleza hapo juu, kazi mojawapo ya dola ni kupanga utaratibu wa uchumi wa kibepari kuhakikisha kwamba mfumo wa ubepari kwa jumla unaendelea na unafanya kazi bila vipingamizi vikubwa na vikwazo. Kwa mfano, mikataba ya kazi na mikataba mingine ya uuzaji na ununuaji wa bidhaa n.k. ifuatwe. Bila hayo, uzalishaji na uuzaji wa bidhaa ambao ni lazima katika utaratibu wa unyonyaji hautafanya kazi. Hii inaonyesha kwamba ni jukumu la dola kupanga, kuimarisha na kulinda mfumo wa kibepari kwa jumla ambamo tabaka la mabepari ndilo linalofaidika.

Hebu nirudie suala la uhusiano baina ya dola na tabaka ambalo ni suala muhimu sana kulielewa. Kurahisisha maelezo tunaweza kusema kwamba uhusiano baina ya dola na mtu binafsi (mwananchi binafsi) - awe yeye ni mfanyakazi au bepari - siu sawa na uhusiano kati ya dola na tabaka la mabepari au la wafanyakazi. Dola linatekeleza mahitaji na maslahi ya tabaka zima la mabepari na sio bepari mmoja mmoja wala sio vijitabaka vya mabwanyenye. Na papo hapo dola hulinda tabaka zima la mabwanyenye dhidi ya tabaka la wafanyakazi. Labda itakuwa rahisi kuelewa jambo hilo nikitoa mfano wa korokoroni, mlinzi wa usiku. Tuchukue mfano wa familia moja tajiri ambayo inaishi katika jumba kubwa na huko uani wanakaa watumishi wa nyumbani. Huyo korokoroni ambaye ameajiriwa na tajiri bila shaka amepewa mafunzo ya ulinzi na amepewa silaha kumwezesha kufanya kazi yake barabara. Kazi yake hasa ni kuilinda familia nzima ya bwana mkubwa na nyumba nzima dhidi ya wezi kutoka nje. Lakini huyu mlinzi hana uwezo wowote kuingilia mambo ya ndani, yaani ugomvi au mizozo miongoni mwa familia. Ikiwa bwana mkubwa amegombana na mkwee au na mwanawe, huyo mlinzi hana haki ya kuingilia kati isipokuwa kama ugomvi huo ni mkubwa mno na unaweza ikahatarisha usalama wa familia na nyumba nzima ya tajiri wake: Tuseme katika ugomvi wao, wameacha milango wazi au kwa hasira mmoja wao amewasha moto. Hapo ni jukuma la mlinzi huyo kuingilia kwa sababu mzozo huo umekwenda mbali na unaweza kuhatarisha maisha ya familia. Hata hivyo anaingilia ugomvi wa aina hii kwa nia ya kusulihisha wala hana uwezo, kwa mfano, wa kumwadhibu yule aliyetenda kosa. Lakini kazi za mlinzi huyo na jukuma lake ni tofauti kabisa ukichukuwa uhusiano baina ya tajiri na wale wafanyakazi wa nyumbani. Hapo, ikiwa kuna ugomvi mkali, jukumu lake ni kumlinda tajiri wake daima na kukomesha upinzani wa wale wafanyakazi hata kama ikibidi atumie silaha yaani mabavu.

Vile vile dola. Dola ni kama yule mlinzi na familia tajiri ni kama tabaka la mabwenyenye. Kama yule mlinzi, dola huwa haliingilii ugomvi na mizozo ya vijitabaka vya mabwenyenye bali huweka utarati' na vyombo (k.m. Bunge) vya kusuluhisha mizozo hiyo. (pia linaweka vyomba na utaratibu mbali-[illegible] li ku[illegible] [illegible] ya kawaida ya kila siku miongoni mwa wanainchi). Kwa hiyo, kuhusu migongano kati ya wananchi binafsi au vijitabaka vya mabwanyenye tunaweza kusema kwamba dola halifungamani na upande wowote lakini sio ilivyo ikiwa migongano ni migongano na mapambano ya kitabaka baina ya wafanyakazi na mabepari. Katika mapambano hayo ya kitabaka daraka la dola ni kulinda na kupigania upande wa tabaka la mabwenyenye kama yule mlinzi wa usiku ambaye anapigania upande wa tajiri wake.

Tofauti kati ya jinsi dola linavyoingilia kati migongano ya kawaida na migongano ya kitabaka litaeleweka kwa ufasaha zaidi tukichukuwa mfano mwingine. Kama tujuavyo kuna sheria mbalimbali za kuilinda mali (sheria kuhusu wizi). Kwa kuwa katika jamii ya kibepari wale wenye mali nyingi ni mabepari, sheria hizo kwa jumla zinanufaisha mabepari. Chini ya sheria hizo iwapo mfanyakazi ameiba mali ya bepari, huwa anachukuliwa hatua za kisheria: kukamatwa na polisi, kufikishwa mahakamani ni kuadhibiwa ikiwa amepatikana na hatia. Iwapo inaonekana kwamba yeye hana hatia, annachiliwa huru. Vilevile, ikiwa bepari anamwibia mwenzie (k.m. kuandika hundi ya bandia au hata anamwibia mfanyakazi (k.m. kumpunja ujira wake) anachukuliwa hatua zile zile za kisheria na hata kufungwa jela. Hapo ndipo tunaona vyema dalili za dola: kwa kweli hakuna tofauti kubwa jinsi vyombo vya dola - polisi, mahakama, magereza n.k. - vinavyomtendea mfanyakazi mhalifu au bepari mhalifu. Je, tunaweza kusema kwamba hapo dola limempendelea bepari na limemnyanyasa mfanyakazi, Mbona basi hao wote wawili wanaadhibiwa chini ya sheria hizo hizo na wala haukuwepo ubaguzi wowote? Je, mfano huo hauthibitishi kwamba kuna usawa, na vyombo vya dola havifungamani upande wowote?

La hasha! Tukiangalia juu juu inaonekana kwamba dola halina ubaguzi na ni chombo cha jamii lakini tukichambua kiini cha mahusiano ya kijamii tutaona hayo sio kweli hata kidogo. Nitathibitisha usemi wangu kwa njia ya maswali:

- Je, nani kwa uwingi wanakabiliwa na mashtaka ya jinai - walewaliona mali au wale wasiona mali? Ni wazi kwamba wale wasiona mali. Na, ni nani wasiona mali katika jamii ya kibepari, mabepari au wafanyakazi? Wafanyakazi. Kwa hiyo ni dhahiri kwamba wafanyakazi ndio kwa uwingi, siku nenda siku rudi, wanateswa na sheria hizo za jinai.

- Je, kati ya mfanyakazi na bepari nani ana uwezo zaidi wa kujitetea kisheria huko mahakamani? Ni wazi kwamba ni bepari. Kufuatana na hali yake ya kiuchumi ana uwezo wa kuajiri wakili na kupigania upande wake kuliko mfanyakazi. Mara nyingi jinsi sheria za kibwenyenye zizopo, mfanyakazi "maskini" anatiwa ndani kwa sababu ya kutojitetea vizuri. Isitoshe, kama tuelewavyo mara nyingi mapolisi na mahakimu huwa wanahongwa ili wapitishe hukumu ya upendeleo Je nani - mfanyakazi au bepari - ana uwezo wa kuhonga hawa waheshimiwa? Ni wazi, bepari.

Kwa haya yote, ni wazi kwamba mfanyakazi ana nafasi ndogo sana ya kutendewa haki na vyombo vya dola la kibwenyenye. Wafanyakazi wengi wanaelewa ukweli huu bila kuambiwa kwa sababu wao ndio hukandamizwa na upendeleo wa taasisi za kidola.

Labda watetezi wa ubepari watatoa dai kusema kwamba hayo yote yaliyotajwa juu yanaonyesha hitilafu tu na sio sifa maalum za mfumo wa kibepari. Kwa hiyo, yanayohitajika ni marekebisho wala sio mapinduzi ya mfumo kwa jumla. Lakini ukweli ni kwamba haya sio makosa yanayofanywa na watu binafsi bali yanaambatana kabisa na mfumo wa kibepari na hayawezi kurekebishwa bila kupindua kabisa mfumo nzima. Hata hivyo, tukubali kwamba "hitilafu" hizi zinaweza kurekebishwa, na zikarekebishwa, je, dola litabadilika kuwa chombo cha jamii zima na kutenda haki kwa pande zote bila kujali tabaka? Haiwezekani kabisa, ikiwa jamii bado ni jamii ya kitabaka. Dola, kama nilivyokwisha sema, daima ni chombo cha tabaka linalotawala. Ukweli huu unathibitishwa kabisa na mfano niliotoa hapo awali. Hebu turudie mfano ule.

Tuliona kwamba mwananchi ye yote yule - akiwa mfanyakazi au bepari - ikiwa anakabiliwa na hatia ya wezi anaweza kuhukumiwa adhabu chini ya sheria ile ile bila kujali tabaka lake. Tukubali hayo hata kama siyo sahihi kabisa katika hali halisi ya jamii kama tulivyokwishaona. Sasa badala ya mfanyakazi mmoja ambaye ameiba mali ya bepari, tuseme kikundi cha wafanyakazi kimegoma kazi. Mzozo huo sio wa aina ambayo bepari anaweza kuipuuza wala dola halichukuli jambo hilo kama jambo lepesi kwa sababu mgomo ni aina mmoja wapo ya harakati za kitabaka. Wanapogoma wafanyakazi kwa kweli wanakataa kunyonywa hata kama hawasemi wala hawafikiri hivyo - ndivyo ilivyo. Hapo basi utaona vyombo vya dola hufanya juu chini kuwarudisha wafanyakazi kazini na vikishindwa kabisa, huweza hata kutumia nguvu sio tu za kawaida za polisi bali hata za jeshi (au za kikundi maalum cha kijeshi kama kile cha F.F.U.) kulazimisha wafanyakazi kurudi kazini.

Ni dhahiri kwamba kuna tofauti kubwa kati ya yule mfanyakazi mmoja mhalifu ambaye aliiba na hicho kikundi cha wafanyakazi ambacho kinagoma. Wizi wa aina ya kwanza ni tukio la kila siku na mabepari wala dola huwa hawajali sana. Lakini tukio kama mgomo lina uwezo wa kuhatarisha mfumo wenyewe ndio maana halipuuzwi na dola. Walakini hata migomo siyo kitu kibaya sana kwa mabepari kwa sababu dola linatumia njia mbalimbali kusuluhisha na kurudisha wafanyakazi kazini.

Hebu tufikirie kitendo cha hali ya juu kabisa kwa upande wa wafanyakazi - yaani kitendo cha kuunda chama cha kisiasa cha kiproletari. Tuseme chama hiki ni chama halisi cha kiproletari na kinafuata itikadi ya kiproletari ya mapinduzi. Kwa hiyo lengo na shabaha yake ni kutayarisha wafanyakazi kisiasa kupambana na dola la mabwanyenye na hatimaye kuleta mapinduzi ya kijamii. Ndiyo kusema, upinzani wa chama hiki ni dhidi ya mfumo nzima wa kibepari na tabaka zima la mabwenyenye. Lengo ambalo linaliongoza chama hicho ni kuleta mabadiliko ya kimsingi ya kisiasa, kiuchumi na kijamii- kuweka mfumo wa kisoshalisti na utawala wa kiproletari. Chama kama hicho kina dhihirisha kuwa baadhi ya wafanyakazi wamefikia mwamko wa juu sana wa kitabaka na wameungana pamoja kuiendeleza harakati za kitabaka. Ni wazi kwamba mwamko huo ni wa hali ya juu zaidi kupita hata mwamko wa migomo wa kupigania haki za kiuchumi(k.m. nyongeza ya ujira; hali bora ya kufanyia kazi n.k.). Hali ya mwamko kama huu inahatarisha mfumo wa kibepari wenyewe. Ndiyo maana dola ambalo lina jukumu kubwa la kulinda mfumo huo kwa niaba ya tabaka la mabepari linatumia nguvu za kitabaka - hasa nguvu za kijeshi - dhidhi ya chama hicho. Wala halijali sheria tena. Wala hakuna kukamatwa na polisi, kufikishwa mahakamani n.k. Hali kama hii inatangazwa kama hali ya hatari; sheria zote zinawekwa kando na jeshi lenyewe (sio polisi tena) linajichukulia mikononi mwake uwezo wote wa kupigana na kukomesha upinzani wa wafanyakazi. Hii ni hali ya juu ya harakati za kitabaka. Katika harakati hizo dola linashindwa kuficha ukweli wake kama chombo pekee cha mabwenyenye. Ule uongo wa kujifanya dola kama chombo kinachotenda haki bila ubaguzi, chombo kinacholinda uhuru wa mwananchi n.k: Uongo wote huo wa kibwanyenye unaelewa wazi; na umma, kwa mara ya kwanza unaelewa

kwamba dola si mlinzi wa hali yao wala kamwe halipiganii ukombozi wao bali ni mlinzi wa wakandamizaji wa umma - mabwanyenye:- ni chombo cha ukandamizaji.

.........................

Kwa kifupi basi tunaweza kusema:

(1) Dola si chombo cha jamii nzima bali ni chombo cha tabaka linalotawala na linalojinufaisha kutokana na mfumo wa kibepari.

(2) Dola la kibwanyenye ni chombo cha tabaka zima la mabwanyenye na wala si la vijitabaka vya kibwanyenye au la mabepari kama watu binafsi.

(3) Dola lililokomaa ni chombo ambacho huhodhi nguvu zote za kisilaha na matumizi ya nguvu yanakuwa halali kwa dola tu na si kwa wengine.

(4) Kazi muhimu za dola la kibwanyenye ni kuimarisha, kukuza na kulinda mfumo wa kibepari. Kazi hizo huwa linalifanya kwa:-

(a) Kupanga utaratibu wa kiuchumi na wa kisheria ambao unawezesha unyonyaji kuendelea bila vikwazo na kuhakikisha kwamba utaratibu huo unafuatwa na wananchi wote. Mpinzani au mhalifu yeyote yule wa utaratibu huo anaweza kuadhibiwa na vyombo vya dola ambavyo vina uwezo wa kutumia mabavu.

(b) Kuunda tawala maalum na kufundisha kikundi cha kitaalamu cha warasimu kuendesha shughuli za utawala za kila siku.

(c) Kuweka vyombo - mbalimbali (k.m. baraza, n.k.) vya kusuluhisha migongano ya kila siku na migongano miongoni mwa tabaka linalotawala.

(d) Kulinda mfumo wa kibepari, yaani tabaka zima la mabepari dhidhi ya maadui ya nje na dhidhi ya matabaka yanayotawaliwa. Ndio maana chombo kama jeshi ni sehemu muhimu sana ya dola.

................


Sasa tutazungumzia kwa ufupi muundo wa dola, yaani sehemu na vyombo mbalimbali vya dola.

Muundo wa Dola

Dola la kibwanyenye la kawaida huwa limegawanyika katika sehemu na vyombo mbalimbali kutekeleza kazi na shughuli za kidola nilizozitaja hapo juu. Kielelezo (u.k. ) kinaelezea sehemu na vyombo vya dola la kibwanyenye.

Kama nilivyokwisha kusema sifa pekee ya dola ni kwamba hiki ni chombo ambacho kinahodhi nguvu zote za mabavu na ni chombo pekee ambacho kina uwezo wa kutumia nguvu katika jamii ya kibwanyenye. Kwa hivyo, sehemu mojawapo ya dola ni ile ambayo itumiayo mabavu bila kificho. Tunaweza kugawanya matumizi ya mabavu katika aina mbili kuu: (a) matumizi ya mabavu dhidi ya mtu binafsi (mhalifu); na (b) matumizi ya mabavu ya kitabaka dhidi ya matabaka yanayotawaliwa na dhidi ya maadui kutoka nje. (Ni dhahiri kwamba aina hizi haziwezi kutenganishwa kabisa na kuna maingiliano kati zao). Na vipo vyombo mbalimbali ambayo hushughulikia matumizi ya mabavu ya aina mbili hizo. Kwa mfano, polisi, mahakama, magereza, n.k. hushughulikia mzozo na migongano ihusikayo mtu

MUUNDO WA DOLA LA KIBWENYENYE



binafsi. Kwa upande mwingine, Jeshi ambalo ni chombo pekee kinacho dhihirishe wazi wazi sifa ya kitabaka ya dola hutumika kulinda mfumo mzima; yaani tabaka linalotawala dhidi ya matabaka maadui ya ndani na ya nje, Jeshi hushughulikia matumizi ya nguvu dhidi ya mizozo na migongano ya kitabaka k.m. kukomesha migomo, ghasia, upinzani dhidi ya serikali ikiwa unahatarisha utawala wa kibwanyenye na kupambana na maadui wa tabaka linalotawala kutoka nchi za nje. Ndiyo maana Jeshi ni chombo muhimu sana cha dola na huthaminiwa sana katika nchi za kibwanyenye. Tabaka linalotawala hutegemea jeshi kulinda mfumo wa kijamii ambao unaoleta faida kwa mabwanyenye. Jeshi kwa kawaida lina utaratibu wa kipekee na wanajeshi hawahesabiwi kama raia wa kawaida. Pia wanajeshi wanapewa mafunzo ya kitaalam katika matumizi ya silaha; wanafundishwa kutii amri daima bila swali na bila fikra. Hayo ni ya lazima kwa jeshi la kibwanyenye kwa kuwa wengi wa wanajeshi hutoka matabaka ya wafanyakazi na wakulima na hutumikiwa kama vibaraka vya tabaka la kibwanyenye dhidi ya matabaka ya wafanyakazi na wakulima. Ndiyo maana wanapewa mafunzo ya kiitikadi kamili, kutowa upendeleo wowote ambao wanaweza kuwa nao kwa upande wa matabaka yanayokandamizwa. Mafunzo ya kutii amri daima na ya nidhamu ni muhimu ili kuwafanya hawa wanajeshi watumikie mabwana yao bila usaliti. Ndiyo maana nidhamu inatiliwa mkazo sana katika jeshi. Nidhamu ya kijeshi la kibwanyenye ni nidhamu ya kitabaka ya kukandamiza na ya kutesa.

Sehemu ya pili ya dola ni ile ya utawala. Dola la kibwanyenye lina kikundi maalum cha watu waitwao <u>warasimu</u>. Hao ndio wataalamu wa kitawala. Kama wanajeshi hao pia hutenganishwa na raia wa kawaida sio hasa kwa nidhamu lakini zaidi kwa utalaam na hali ya maisha yao. Hao ndio wanaoendesha shughuli za kawaida za dola na hutumikia tabaka linalotawala kisiasa: "watumishi watiifu" wa dola la kibwanyenye!

Katika sehemu hii ya utawala zipo shughuli nyingi, nyingine ambazo lazihusu dola, kama vile uendeshaji wa mabaraza, kamati, n.k. kusulu hisha migongano mbalimbali; shughuli nyingine za kiuchumi na za kitaalamu kama ule utafiti, n.k.

Sehemu ya tatu kuu ya dola ni ile ya siasa - hasa Bunge na Serikali. Bunge, kwa kweli, linaweza kulinganishwa na baraza kuu la usuluhishaji migongano miongoni mwa mabwanyenye wenyewe. Ni kweli kwamba kitabaka, mtazamo wa mabwanyenye ni mmoja na mahitaji yao ya muda mrefu hayatofautiani. Lakini, matakwa yao ya kila siku na ya haraka yanatofautiana na mara nyingine hata kuhitilifiana sana. Ndiyo maana vijitabaka vya kibwanyenye hugombana vyenyewe kwa vyenyewe. Hitilafu hizi husababishwa na hali halisi ya uchumi wa kibepari. Vijitabaka mbalimbali vya mabwanyenye hushughulika na sehemu mbalimbali za uchumi ambamo maslahi yao hugongana mara kwa mara. Migongano hii inakuwa ni migongano ya kisiasa pia. Bunge ndilo chombo cha kusuluhisha kisiasa migongano hii. Kama tunavyoelewa wote, vijitabaka hivyo huwakilishwa Bungeni na vyama vya kisiasa. Kila chama cha kibwanyenye kinawakilisha kijitabaka maalum na maslahi yake. Usuluhishaji wa migongano kati ya vijitabaka vya kibwanyenye kwa njia ya majadiliano katika Bunge huitwa "demokrasi" na "usawa". Ni wazi kwamba demokrasi ya aina hii ni demokrasi ya kibwanyenye kwa sababu ni demokrasi miongoni mwa tabaka la mabwanyenye lakini ni "utawala wa kidikteta" dhidi ya matabaka yanayotawaliwa. Ndiyo maana ni vigumu sana kwa chama halisi cha kiproletari kushika hatamu za kisiasa kwa kupitia njia ya uchaguzi. Ikitokea ghafla kuwa chama cha kiproletari kimeshinda uchaguzi, kamwe hakiwezi kuchukua utawala wa dola na bila shaka kitapinduliwa. Kwa sababu hizo Kamaradi Lenin alitia mkazo sana suala la jukumu la chama cha kiproletari kuvunjilia mbali kabisa dola la kibwanyenye na kuunda dola jipya la kiproletari katika mapinduzi halisi ya kiproletari.

Kwa hiyo Bunge, kama dola, si chombo ambacho hakifungamani upande wowote bali ni chombo ambacho kazi zake ni kurahisisha

usuluhishaji wa migongano miongoni mwa vijitabaka vya mabwanyenye. Papo hapo uchaguzi kila miaka mitano; majadiliano makali Bungeni n.k. yanasaidia mabwanyenye kimawazo kwani yanapotosha mawazo ya wanaokandamizwa kuhusu ukweli wa mambo. Bunge na vyombo vingine vya dola, licha ya kuwa na kazi nilizotaja hapo juu, vinasaidia kueneza na kukuza itikadi ya uwongo ya mabwanyenye kuhusu haki, usawa, demokrasi n.k. katika fikra za umma kwa jumla.

Ule uchaguzi wa kila miaka mitano, kwa kweli, unachagua chama cha kijitabaka kimoja kuunda serikali na kushughulikia kazi mbalimbali za dola kwa muda ule wa miaka mitano. Serikali ya "Labour" au "Conservatives" huko Uingereza; au serikali ya "Republican" au Democrats" huko Marekani haibadilishi hata chembe moja sifa za kibwanyenye za dola. Dola linabakia hivyo hivyo, uwe utawala wa chama hiki au kile. Kinacho badili, ikiwa, kwa mfano, chama cha "Labour" kikishinda uchaguzi, ni muundo tu wa serikali - ndio kusema mawaziri, waziri mkuu n.k. - wala si dola. Matamshi ya Marx juu ya uchaguzi ni ya busara tupu. Marx alieleza kuwa uchaguzi kila miaka mitano ni nafasi tuinayowapa wafanyakazi (na wale wengine wanaonyonywa) kuchagua kijitabaka kipi cha kibwanyenye kitakachowakandamiza kwa miaka mitano ijayo. Ni kubadilisha kikundi kimoja cha wakandamizaji kwa kingine. Hii ndiyo demokrasi katika jamii ya kibwanyenye! Uchaguzi chini ya mfumo wa kibepari kamwe hauwezi kuleta utawala halisi wa wafanyakazi.

Sehemu ya nne kuu ya dola ni ile ya itikadi. Mara nyingi dola humiliki njia za kutangaza habari na kueneza itikadi ya kibwanyenye kama redio, magazeti, telivisheni, sinema n.k. Vilevile mara nyingi dola huendesha shughuli za kielimu - mashule, vyuo n.k. - ambazo hutayarisha wataalam kwa ajili ya uchumi wa kibepari na wakati huo huo kueneza itikadi ya kibwanyenye.

..............

Hizo basi ndizo sehemu kubwa mbalimbali za dola la kibwanyenye. Dola katika nchi moja ya kibepari hutofautiana na dola lingine pengine kwa muundo lakini madola yote haya katika nchi za kibepari yana sifa zote za kibwanyenye tulizozungumzia.

Ni muhimu pia kuelewa kwamba kufuatana na hali halisi ya jamii dola la kibwanyenye linaweza kuwa na aina mbalimbali za kisiasa kama ile ya kifalme, au ya demokrasi ya kibwanyenye (yaani kuwa na Bunge, uchaguzi n.k.) au ya kijeshi. Kiini cha aina hizo zote ni utawala wa kibwanyenye. Aina za kisiasa za dola zinategemea historia, hali halisi ya kijamii na nguvu za kitabaka katika kila nchi.

Kuanzia miaka ya mwisho ya karne ya 19, madola ya kibwanyenye yalishambulia nchi zingine za ng'ambo na kuweka utawala wake huko. Huu ndio ulikuwa mwanzo wa ubeberu na ukoloni. Kwa hiyo, madola ya kibepari ya nchi zilizoendelea ni vile vile madola ya kibeberu. Jambo hilo tutaligusia hapa chini.

## III. <u>Dola la Kibeberu</u>

Matokeo ya migongano ya kiuchumi wa kibepari huko nchi za Ulaya yalikuwa ni kuwafanya mabwanyenye wa nchi hizo kuvuka mipaka ya nchi zao kutafuta faida zaidi nchi nyingine. Mabepari wa nchi za Ulaya walihitaji mazao awali (Yahitajikayo katika viwanda, k.m. pamba, ngozi, n.k.) na masoko ya bidhaa zilizotengenezwa katika viwanda vyao. Hayo mawili yangewasaidia kuhamishia migongano ya jamii zao katika nchi zingine; migongano iliyotokana na hali ya uchumi wa kibepari na upingamizi wa wafanyakazi. Sababu hizo ndizo zilizofanya mabepari hao kusafirisha rasilmali nchi za nje kujipatia mazao awali na masoko. Walakini, rasilmali inahitaji kulindwa. Licha ya hiyo, ilikuwa ni muhimu sana kwa viwanda vya nchi hizo kujipatia mazao awali bila vikwazo vyo vyote. Kwa sababu hizo mabepari walivamia nchi

za "dunia ya tatu" na kuweka utawala wao wenyewe kwa njia ya dola la kikoloni. Ndiyo kusema dola la kikoloni lilikuwa kama mlinzi wa maslahi ya matabaka hayo ya kibwenyenye ya nchi za Ulaya. Kufika mwaka wa 1914, hizo nchi za kibepari zilikuwa zinatawala karibu nchi nyingine zote za Afrika na Asia kama makoloni. Katika juhudi zao za kuweka utawala wao na kunyonya mali yao, madola ya kibeberu yaligongana wenyewe kwa wenyewe mara kwa mara, hata kupigana vita kama vile vita viwili vya ulimwengu. Ukweli ni kuwa vita hivyo vilikuwa ni matokeo tu ya migongano miongoni mwa nchi za kibepari ingawa watu wengi wa nchi za Afrika na Asia ambao hawakuwa na uhusiano wowote na ugomvi huo walipigana na kuuawa. Kama kawaida, wakigombana mabwinyi, wanaoumia zaidi ni watwana.

Vita hivyo na migongano miongoni mwao ilifanya madola hayo ya kibwenyenye yapanuke sana kijeshi mpaka leo kama tunavyoona jinsi sayansi ya kivita na hii usanyiko ya zana za vita yanahatarisha maisha ya dunia zima. Muhimu zaidi kupita migongano miongoni mwao wenyewe ni migongano kati ya ubeberu kwa upande mmoja, na nchi za kisoshalisti, nchi ambazo zinapigania uhuru wao - (yaani vyama vya ukombozi) kwa upande mwingine kama ilionekana wazi katika vita vya Vietnam, Msumbiji, n.k.

Hayo yote yamefanya madola ya kibeberu kufumbua na kutengeneza zana za vita mpya kila siku - yaani kuendeleza vyombo vya kuulia. Hata hivyo, nchi za kibepari zimepigwa na kushindwa vibaya na nguvu za ukombozi na kisoshalisti kote duniani. Enzi hii ni enzi ya kisoshalisti na wala si ya ubeberu na ubepari. Kwa jumla, ubeberu unapigwa vita na umma wa watu ulimwenguni kote. Nchi zinataka na zinapigania uhuru; mataifa yanapigania ukombozi na watu (umma) wanapigania mapinduzi. Hayo ndiyo maelekeo katika ulimwengu mzima. Mara ya kwanza katika historia ya wanadamu, mamilioni ya watu wameanza kusimama imara dhidi ya ubeberu na ubepari na kusema: Tumenyonywa na kuteswa kadiri ya kutosha; sasa tutaungana zote pamoja na kufanya mapinduzi halisi ya umma chini ya uongozi na nguvu za kiproletari kuleta ukombozi halisi wa binadamu. Huu ndio mwito wa kisasa na kilio cha kivita cha umma.

## IV. Dola la ukoloni mambo-leo

Katika mapambano yake na nguvu za ukombozi, ubeberu ulifanya (na unaendelea kufanya) kila njama ya kushinda na kuendelea na ubeberu. Njama mojawapo ilikuwa kutoa uhuru wa bendera kwa nchi za Afrika na Asia. Baada ya uhuru kama huo, ubeberu uliendelea kunyonya uchumi wa nchi hizo kwa njia mbalimbali ambazo huwa unabadilisha kufuatana na mabadiliko katika mazingira ya nchi hizo na hali ya mapambano katika ulimwengu.

Wakati wa ukoloni, "dola la kikoloni" lilikuwa, tuseme, ni kama idara" au sehemu tu ya dola la kibwenyenye la nchi ambayo ilikuwa inaitawala. "Dola la kikoloni" lilikuwa linaendeshwa na watumishi wa tabaka la kibwenyenye. Kwa mfano, chini ya ukoloni wa Kiingereza, "dola la kikoloni" katika Tanganyika lilikuwa ni sehemu tu ya dola la Uingereza na lilikuwa linaendeshwa na watumishi - Gavana, D.C., polisi n.k. - wa mabwenyenye wa Uingereza. Tabaka lililokuwa linatawala, linaishi huko Uingereza. Wakati huu basi nchi zetu zilikuwa zina tawaliwa na tabaka la kigeni la kibwenyenye na dola pia tuseme lilikuwa dola la kigeni. Tabaka lenyewe lilibaki huko Uingereza na liliwakilishwa humo nchini na "dola la kikoloni." Baada ya uhuru, kwa mara ya kwanza kitabaka kizalendo cha hapa hapa nchini - tabaka la vibwenyenye - lilishika hatamu za kidola japokuwa liliendelea kuwa kibaraka cha mabwenyenye wa ulimwengu.

Ni muhimu sana kuchambua sifa za madola katika nchi hizi za ukoloni - mamboleo; tabaka au matabaka ya ndani ambayo yanatawala na mahusiano ya kiuchumi na kisiasa kati ya madola na ubeberu. Jambo hilo haliwezi kuzungumziwa kwa jumla tu bila uchambuzi maalum wa nchi au jamii tunazozungumzia. Walakini tunaweza kuonyesha hili tu, kwamba uhuru (hata wa bendera) kwa mara ya kwanza ulifanya tabaka la kizalendo kushika hatamu za kidola iwapo chini ya mfumo wa ubepari wa ulimwengu.

Ndiyo maana tunasema kuwa wafanyakazi na wakulima - yaani umma - wa nchi hizo za ubepari uliovia wananyonywa na tabaka la ndani na tabaka la nje. Unyonywaji wa wafanyakazi na wakulima wetu una sura mbili - ule wa kibepari na vilevile wa kibeberu. Ndiyo maana harakati ya wafanyakazi na wakulima dhidi ya dola la kikoloni-mamboleo ni harakati pia dhidi ya ubeberu ambao unastawisha dola hilo - kiuchumi, kisiasa na kijeshi.

Je, jinsi gani mapambano hayo ya wafanyakazi na wakulima wa 'dunia ya tatu' yanaweza kupata ushindi na kujenga jamii ya kimapinduzi halisi kwa manufaa yao wenyewe? Kuweza kuendeleza mapinduzi hayo wanamapinduzi wanapaswa kuelewa maana ya dola na kulichambua kisayansi dola katika jamii yao. Kwa hiyo, maelezo haya, ingawa ni mafupi mno, kuhusu dola la kibwanyenye ni mwanzo tu.

Makala haya yatakuwa na upungufu ikiwa sitagusia jambo moja muhimu kwa mwanamapinduzi ye yote na jambo hilo ni suala la chama cha kiproletari.

## V. <u>Mapinduzi ya kiproletari: Suala la chama na dola.</u>

Maelezo niliyotoa hapa juu yanaonyesha kwa ufasaha kwamba nguvu za matabaka yanayotawala zinatokana na nguvu za kidola; kwamba dola ni chombo ambamo inakusanyika migongano yote ya kitabaka. Vilevile ni dola ambalo ndilo linasimamia na kuwakilisha *umoja* wa tabaka la kibwanyenye dhidi ya tabaka la wafanyakazi. Kwa hivyo ni wazi kuwa tabaka la kibwanyenye lina chombo chake pekee cha kukimarisha tabaka hilo; ambacho pia kinakuza na kulinda daima utaratibu na mfumo wa kibepari ambao unawanufaisha waheshimiwa hao. Je, wafanyakazi ambao wananyonywa na kuteswa chini ya mfumo huu, wana chombo gani kitachopigania ukombozi wao? Je, jinsi gani wafanyakazi watatekeleza jukumu lao la kihistoria kuipindua mfumo huu wa ubepari na kutupilia mbali utaratibu wa unyonyaji na badala yake kuijenga mfumo wa kisoshalisti? Dhahiri, mapinduzi ya kiproletari hayawezi kushinda bila mapambano makali dhidi ya dola la kibwenyenye; ni dhahiri pia kwamba mapambano hayo hayawezi kuendelezwa kuelekea kwenye ushindi bila ya uongozi wa kisiasa wa chombo cha wafanyakazi wenyewe - yaani chama chao. Chombo cha mabwenyenye ni dola; chombo cha wafanyakazi kimo chama ambacho kinaongozwa na itikadi ya kisayansi inayowakilisha maslahi halisi ya wafanyakazi - yaani itikadi ya Marx na Lenin, na hiki ndicho chama cha kiproletari. Sawasawa na dola ambalo linawakilisha umoja wa mabwanyenye, chama cha kiproletari kinaunganisha wafanyakazi na kuleta mwamko wa kitabaka kwao.

Lenin ametufundisha kwamba chama hicho hakiwezi kuwa cha upuuzi tu kama vyama vya kibwanyenye. Wanachama wa chama hicho wanakuwa wanamapinduzi - wafanyakazi na wengine - ambao wana msimamo madhubuti na wanajitolea maisha yao kupigania mapinduzi ya kiproletari. Sio mtu ye yote yule ambaye anakubaliwa kuwa mwanachama eti kwa sababu ametowa ushuru, anakubaliana na ahadi za chama na amekatisha kadi. La sivyo! Mwanachama wa chama cha kiproletari ni "kada" - ni mwanamapinduzi ambaye kazi yake daima ni kuendeleza mapinduzi. Kwake yeye vitu vingine vyote vya maisha ya kawaida ni haramu ila mapinduzi.

Hiyo haimaanisha kwamba chama kama hicho ni chama cha wateule bali ni chama cha wafanyakazi na wengine ambao wamefikia kiwango cha juu sana cha mwamko wa kiproletari. Uhusiano baina ya wanachama hao na umma kwa jumla ni sawa na uhusiano wa samaki na maji ya bahari. Kamaradi Lenin alieleza kuwa bila chama cha aina hiyo itakuwa vigumu mno kuleta umoja wa kitabaka kwa wafanyakazi na kusisimua mwamko wa kisiasa miongoni mwao. Bila chama kama hicho dola la kibwanyenye litaendelea daima kutenganisha wafanyakazi. Bila mwamko na umoja, wafanyakazi hawataweza kamwe kulipindua na kulibomolea mbali dola la kibwenyenye na kujenga jamii ya kisoshalisti.

Kwa jeshi la kibaraka la mabwanyenye, wafanyakazi (na wakulima) wawe na jeshi lao la wanamapinduzi; kwa silaha zao za kisasa, wafanyakazi wawe na silaha yao kubwa kupita zote na hiyo ni itikadi ya kiproletari; kwa chombo chao cha dola, wafanyakazi wawe na chama chenye nguvu na umoja chama ambacho kinaongozwa na nadharia ya kisayansi ya Marx na Lenin.

Mwito mkuu wa Lenin ulikuwa:

> "SISI MAMILIONI YA WAFANYAKAZI TUMEVUNJA MIGONGO YETU KWA MUDA MWINGI SANA! TUMEWAFANYIA KAZI MATAJIRI NA KUBAKI MASKINI KWA MUDA MWINGI SANA! TUMEWAACHIA WATUIBIE KWA MUDA MREFU SANA.......
> TUNATAKA KUUNGANA: KUUNGANA KATIKA CHAMA CHA WAPROLETARI NA KWA PAMOJA TUPIGANIE MAISHA MEMA.....
> SI MATESO WALA SI JELA, WALA SI UHAMISHAJI WALA SI KIFUNGO CHA ADHABU, WALA SI MAUTI, YOTE HAYA HAYAWEZI KUTUTISHA.....TUTASHINDA JAPO KUNA MATESO"

Naam! hicho ndicho kilio cha kivita cha wanamapinduzi.

********************

## NYONGEZA

Hapo nitaeleza maana ya maneno, maneno ambayo mara nyingi hutafsiriwa vibaya katika maandishi ya kibwenyenye. Maneno haya ni:

'nchi', 'taifa', 'dola' na 'serikali'.

NCHI: inamaanisha eneo maalum la ulimwengu, yaani sehemu ya ardhi yenye mipaka yake ambamo wanaishi watu na linatawaliwa na dola maalum.

TAIFA: inamaanisha jamii ya watu iliyo wenye nchi yao wenyewe, lugha, utamaduni na uchumi. Kwa kawaida, huwa jamii kama hii huishi katika sehemu maalum ya ulimwengu, yaani katika nchi yao.

DOLA: Dola ni chombo cha tabaka linalotawala katika jamii au taifa maalum. Ni chombo ambacho kinahodhi njia za upiganaji kwa niaba ya tabaka maalum. Kwa kawaida, mipaka ya nchi ndiyo inadhihirisha eneo la utawala wa dola maalum. Lakini maneno 'dola' na 'taifa' hayana maana moja.

SERIKALI: Serikali ni sehemu moja ya dola. Tunaweza kusema kwamba serikali ndio inashika hatamu za kisiasa za dola. Serikali inaweza kubadilika bila dola kubadilika, kama nilivyoeleza katika makala.

Ifuatayo ni tafsiri ya sehemu tu ya Sura ya Tano ya Taarifa iliyotolewa na Kiongozi wa Chama cha Kikomunisti cha nchi ya Albania kwenye Kikao cha Saba cha Mkutano Mkuu wa Chama hicho. Tunasikitika imepasa tutoe sehemu ndogo tu ya Taarifa hiyo muhimu kwa kukosa nafasi katika gazeti hili. Sura ya Tano inahusu hali ya ulimwengu ilivyo na siasa ya nchi za nje ya Albania - hata sura hii haikuwezekana kuitafsiri yote, badala yake tumetafsiri sehemu fulani-fulani tu.

Kusudi la kuchapisha tafsiri hii kwanza kabisa ni kuwatambulisha kwa wasomaji wetu nchi ya Albania na msimamo wake wa kisiasa; pili ni kuanzisha mjadala kuhusu suala la nchi zinazonyonywa na kukandamizwa - nchi ambazo siku hizi zinaitwa "dunia ya tatu". Kuna hatari kwamba msemo wa "dunia ya tatu" huenda ukaficha ukweli kwamba nchi hizi kwa kweli si "dunia" pekee bali ni sehemu tu ya ile "dunia" ya kibepari, na kwamba si kweli kwamba nchi hizi zinapinga ubeberu kwani ni matabaka fulani tu ndiyo yawezayo kupinga ubeberu - baadhi ya matabaka katika nchi hizi, yaani matabaka yanayotawala, ndiyo nguzo ya ubeberu katika nchi hizi. Kwa hivi kuna umuhimu kuwa na msimamo wa kisayansi kuhusu suala hili. Tunatumaini tafsiri hii ya sehemu ya Taarifa ya Kamaradi Hoxha itasaidia katika kufafanua msimamo sahihi.

MHARIRI.

## KUHUSU NCHI ZINAZONYONYWA ULIMWENGUNI

## NA

## ENVER HOXHA

Ujenzi wa ujamaa wa kisaynsi nchini Albania, pamoja na harakati za watu wetu ili kuimarisha utawala wa kifanyakazi na ulinzi wa nchi yetu, na jitihada zao za kujenga hali madhubuti kwa vizavi vijavyo - haya yote ni mambo ambayo kamwe hayawezi kutenganishwa na hali ya ulimwengu mzima wa leo, yaani suala zima la maendeleo ya jumla ya historia ya ulimwengu kama ylivyo hivi sasa.

Chama chetu kimekuwa kikifuatia kwa makini na kuyachambua matukio na matendo ya kila hali mpya, na mwelekeo na nia ya makundi mbali mbali ya kisiasa ambayo yanajishughulisha kuhusu hili na lile hapa ulimwenguni, na daima

kimeshikilia msimamo sahihi wenye misingi thabiti kufuatana na mafundisho ya ujamaa wa kisayansi, na kufuatana na maslahi ya taifa letu, mapinduzi yetu, na ukombozi wa wananchi.

Kwa ujumla, hali ya ulimwengu hivi sasa inaonekana kuwa ya kutatanisha sana, imejaa migongano na mikabiliano ambayo sasa imeenea dunianzima na katika pande zote za maisha ya watu. Dhidi ya ubeberu, ubeberu-jamii na vitendo vyake viovu vya kivamizi, dhidi ya mabeberu, makampuni-hodhi ya kimataifa na unyonyaji wake wa kishenzi, dhidi ya wapinga-maendeleo pamoja na hujuma zao za kimabavu - dhidi ya mambo yote haya ndiyo kuna wafanyakazi na wana-mapinduzi shupavu wa ulimwengu mzima ambao nguvu zao zinazidi kukua kila siku, watu ambao wanapigania uhuru na demokrasi, wanapigania ujamaa wa kisayansi. Ulimwengu umefikia hatua ambapo suala la mapinduzi na ukombozi wa kitaifa wa wananchi si jambo la kutumainiwa tu kwa siku za usoni bali limekuwa suala la kushughulikiwa sasa hivi..........

Siku hata siku vuguvugu la ukombozi miongomi mwa watu pote duniani linazidi kusonga mbele. Ushindi wa kihistoria na ulio maarufu sana waliopata wananchi wa Vietnam, Cambodia na Laos - ushindi ambao haukuwa dhidi ya mabeberu wa Kimarekani peke yao bali pia dhidi ya hila, njama navitimbi vya kila aina vya mabeberu-jamii wa Urusi, umethibitisha kuwa hizi nchi mbili za kimabavu - pamoja na uwezo wake mkubwa kuhusu vita na utajiri wake mwingi - kamwe haziwezi kuzikandamiza nchi nyingine hata zikiwa ndogo namna gani, kama nchi hizi nyingine zikijitoa mhanga kupigana hadi mwisho na kujitolea kwa kila hali. Ushindi huu umethibitisha ukweli kwamba uhuru na ukombozi ni vitu ambavyo huweza kupatikana na kulindwa kwa bunduki, kwa mapambano, na kwamba msimamo wa kuanzisha vita vya umma vyenye lengo la kuleta ukombozi wa kitaifa ndiyo msimamo uwezao kuleta ushindi wa hakika.

Hivi leo makontinenti ya Asia, Afrika na Marekani-Kusini yamekuwa ni ngao pana ya mapambano dhidi ya ubeberu wa Kimarekani, mabeberu-jamii wa Urusi, na mabeberu wengineo. Wananchi katika makontinenti haya wanafanya jitihada kubwa na za pamoja kudumisha uhuru wao, kuondoa ukoloni na ukoloni-mamboleo. Sisi sote tumeshuhudia jitihada hizi za watu wa Afrika kujipatiaukoombozi halisi baada ya kukaa katika hali ya utumwa kwa karne nyingi. Kupatikana kwa uhuru katika nchi ambazo hivi majuzi tu zilikuwa chini ya ukoloni wa Kireno kumeharakisha zaidi mapambano dhidi ya ubaguzi wa rangi huko Zimbabwe na Afrika Kusini.

Mapambano ya watu wa kimaendeleo na wa kidemokrasi dhidi ya wafashisti na wapinga-maendeleo vile vile yamezidi kusonga mbele na kutanuka. Kuangushwa kwa serikali za kidikteta katika nchi kadhaa, na mapambano ya wazalendo wa Brazil, Bolivia, Thailand na Malaysia, pamoja na mapambano ya kujikinga ya wananchi wa Chile, Argentina na Indonesia dhidi ya serikali za kifashisti za nchi hizo yamekuwa ni pigo kubwa kwa wapinga-maendeleo na mabwana zao wa kibeberu. Wananchi wa ukanda za Bahari ya Hindi, wa Asia ya Kusini-Mashariki na pwani ya Afrika wanapigana kutwa kucha ili waweze kuviondoa vituo vya kijeshi na vituo vya meli za kivita vilivyowekwa katika sehemu hizo na nchi mbili za kimabavu za Marekani na Urusi. Kila pahali wananchi wanazidi kuamka na kutambua hatari inayoletwa kao na siasa ya uchochezi, uvamizi na ukandamizaji inayotekelezwa katika sehemu hizo na mabeberu wa Kimarekani na mabeberu-jamii wa Kirusi.

Nchi zile ambazo zinatekeleza kwa dhati ujamaa wa kisayansi ndiyo nguzo madhubuti ya kusaidia wananchi walio katika harakati za mapinduzi na ukombozi. Nchi hizo ni muhimu sana katika suala zima la kufaulu kwa mapinduzi. Albania, nchi yenye ujamaa wa kisayansi, inaona fahari kuwa miongoni mwa nchi kama hizo - tunesimama bega kwa bega na wafanyakazi na wananchi kwa ujumla katikamapambano yao makubwa - mapambano ya kuleta ujamaa wa kisayansi, ukombozi na uhuru. Kwa kujibidisha zaidi katika ujenzi wa maisha mapya kwa kuvunjilia mbali mashambulio ya mabeberu, wabadilifu wa kisasa, na mabwanyenye wapinga-ukomunisti, nchi yetu imetoa mchango na bado inaendelea kutoa mchango wake katika jitihada za kulinga na kuendeleza lengo la ujamaa wa kweli.

Ni kudumishwa huku kwa harakati za wafanyakazi kukua kwa juhudi za kutafuta ukombozi, ushindi uliopatikana katika ujenzi wa ujamaa wa kisayansi- haya yote ndiyo kwa pamoja yamedhoofisha zaidi ubeberu na ubeberu-jamii, yamefanya migongano katika mfumo wa ubepari iwe mikali zaidi hati kuutikisa mfumo huo hadi kwenye mizizi yake.........

Chama chetu kinafikiri kuwa hali ya ulimwengu hivi leo ni yenye mshindo mkubwa, na hivyo hakuna nafasi ya mtu kulegalega. Ni sharti tuchambue na kupina siasa na vitendo vya mabwanyenye wa kibeberu na nchi zote mbili za kimabavu, na papo hapo tuwe na msimamo thabiti wa kitabaka kuhusu siasa na vitendo hivyo. Jambo hili ni muhimu sana katika hali ya sasa kwa wana-mapinduzi wote, mataifa yote na wananchi wote wanaopigania ukombozi na uhuru, amani na usalama miongoni mwa mataifa. Msimamo wa kimsingi kuhusu suala hili muhimu ndiyo njia pekee iliyo sahihi ya kupata strateji na mbinu za kimapinduzi kweli kweli, na ndiyo kipimo cha kutambua ni watu gani walio wa kimaendeleo na hivyo kuweza kuwatambulisha kutoka kwa wapinga-maendeleo.

Tukiangalia hali thabiti - mambo kama yalivyo na vitendo vitendavyo - tunaona kuwa hapa ulimwenguni hivi leo nchi zile mbili za kimabavu, Marekani na Urusi, ndizo adui mkubwa zaidi, wa hatari zaidi, na chochezi zaidi kuliko mabeberu wengine ambao wamewahi kuwepo katika historia ya ulimwengu. Kama ni kwa pamoja au pweke-pweke, nchi hizo mbili ndizo adui mkuu wa ujamaa wa kisayansi, adui wa uhuru na ukombozi wa mataifa, kinga kubwa ya wakandamizaji na wanyonyaji, na ndizo zinazofanya daima kuwe na hatari ya kutokea vita kuu ya tatu. Wala hatuwezi kusema kuwa nchi mojawapo kati ya hizo mbili ni afadhali, zote ziko katika mstari mmoja.

Walimwengu bado wanaendelea kukumbana na uchokozi na uvamizi wa mabeberu wa Kimarekani. Tangu vita kuu ya pili imalizike, mabeberu wa Kimarekani wamekuwa wakifuata siasa ya kiovu na kutenda vitendo vya kifedhuli dhidi ya wakomunisti, wapenda-uhuru na ukombozi. Ni mabeberu wa Marekani ndio walioanzisha uchokozi wa kinyama huko Korea na Vietnam, na kutenda vitendo vya kinyama ambavyo vilikuwa havijajulikana katika historia ya binadamu. Ni mabeberu wa Marekani ndio waliojiingiza huko Congo, ndio walioyazimisha mapinduzi ya Dominika, ndio walioeneza vita hadi huko Laos na Cambodia, ndio waliowasha moto katika Mashariki ya Kati na kuchochea kuzuka kwa serikali za kifashisti huko Chile na Argentina.

Kufuatia hali yao ya kibeberu, mabeberu wa Marekani wamezidi kueneza mirija yao kwenye makontinenti yote na wanazidi kudumisha mizizi yao kila pahali na kwa kila njia - kama vile kwa kutumia "misaada" watoayo, kwa mikopo izifanyazo nchi zinazoipokea zikabwe zaidi na zaidi, kwa mikataba mbali mbali, kwa vituo vya kijeshi walivyoweka katika nchi nyingi, kwa kuingilia kati kikatili katika mambo ya ndani ya nchi nyingine, na hata kwa kuvamia nchi nyingine kwa silaha. Haya yote ndiyo matendo maovu ya mabeberu wa kinyama wa Marekani.

Kadhalika, tabia ya kukubali na kufuata siasa ya Marekani bila kufuata misingi yoyote ambayo Krushev na wafuasi wake wamekuwa wakiendeleza haikuwafanya mabeberu wa Marekani wawe na huruma zaidi. Bado Marekani ndiyo makao makuu ya ubepari kiuchumi na kisiasa, ndiyo mlinzi mkubwa wa ukoloni na ukoloni-mamboleo, ndiyo kiini cha ubaguzi wa rangi na mwenezaji mkubwa wa vitendo vya kipinga mapinduzi pote duniani. Chama chetu daima kinashikilia msimamo kwamba mabeberu wa Marekani ni wachokozi na wataendelea kuwa wachokozi mradi wana uwezo wowote wa kuchokoza nchi nyingine.

Kutokana na mapambano ya kimapinduzi na ya ukombozi na vile vile kutokana na hali yake kuzidi kuwa mbaya zaidi na zaidi na migongano yake kuwa mikali zaidi na zaidi, ubeberu umeshindwa pahali pengi sana. Inatosha tukitaja tu jinsi ukoloni ulivyotokomezwa hadi nchi nyingi zikapata uhuru wake. Katika siku za usoni ubeberu utaendelea kushindwa vile vile. Lakini wakati huo huo mabeberu - hasa mabeberu wa Marekani - watazidi kuongeza juhudi zai kujaribu kupokonya tena kile walichonyang'anywa na kutwaa sehemu nyingine mpya. Hivi ndivyo ubeberu unavyojieneza na kufifia wakati ule ule. Hivyo, hivi sasa kama ilivyokuwa katika siku zilizopita, swala la kufichua na kupinga mipango yote ya kichochezi ya mabeberu wakiongozwa na mabeberu wa Marekani ni suala la lazima kabisa kama tunataka kweli kulindauhuru na ujamaa wa kisayansi, na kama kweli tunataka mapinduzi na ukombozi vifaulu.

Watu wa ulimwenguni vile vile wanapingana vita vikali dhidi ya yule adui wa pili, ubeberu-jamii wa Urusi - adui ambaye ni mwenye hatari na unyama kama yule wa kwanza tu. Siasa ya wabadilifu wa Urusi hakika ni siasa ya uchochezi wa kikoloni na kikoloni-mamboleo ambayo msingi wake ni mabavu ya mtaji na silaha. Harakati ambazo Urusi inaendesha hivi leo kutaka kushika sehemu muhimu katika Mashariki ya Kati, kujieneza kwake katika Bahari ya Mediteranea, Bahari ya Atlantiki, na Bahari ya Hindi, kujiingiza kwake katika nchi za Kiafrika na za Marekani-Kusini, vitisho vyake kwa nchi za Ulaya na uchokozi wake katika nchi za Asia - vitendo vyote hivi vinadhihirisha siasa hii ya Urusi. Kama mabeberu wa Marekani, mabeberu-jamii wa Urusi wanajitahidi sana kila pahali kuzimisha moto wa mapinduzi na ukombozi uliowashwa na wananchi.

Katika mashindano yao na mabeberu wa Marekani, mabeberu-jamii wa Urusi wamekuwa wakila njama za kupinga mapinduzi dhidi ya wananchi, wamekuwa wakichochea magomvi na chuki miongoni mwa mataifa, na wamekuwa wakijitahidi kujigamba wanadume kila pahali. Chama chetu daima kimekuwa kikisisitiza kuwa ndoto zozote au kulegalega kokote katika msimamo kuhusu Urusi ya leo lazima kutaleta madhara kwa wale wote wanaoendelea kuamini uongo na maneno matupu yanayotoka Moscow.

Ili kutekeleza siasa yao ya kukandamiza wengine na kujiingiza katika sehemu zisizowahusu, mabeberu, mabeberu-jamii, na mabepari wa ulimwenguni kwa ujumla wameunda taasisi na

vyombo kemkem vya kijeshi, kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni, n.k, ambavyo hivi leo ndiyo silaha na njia kuu za kukandamizia wananchi wa ulimwengu mzima. Wakati huo huo wametunga msululu nadharia, dhana na tasnifu ambazo wanazitumia katika kuwalaghai na kuwatishia wananchi na kuhalalisha dhuluma na ukandamizaji wao, na papo hapo kuwavuruga akili watu ili waweze kuwa na mwelekeo watakao wao mabeberu. Uchokozi wa kijeshi kujiingiza katika uchumi wa nchi nyingine na uvamizi wa kiitikadi - hayo yote ndiyo kwa pamoja msingi wa siasa inayofuatwa na maadui hawa, siasa ambayo lengo lake ni kuvunjilia mbali ujamaa wa kisayansi, kufyekelea mbali mapinduzi, na kuendeleza mfumo wa kitumwa uliopo hivi sasa.

Katika hali hii wajibu wa wana-mapinduzi na wananchi kwa ujumla ni kuimarisha nguzo za mapambano ya pamoja na madhubuti ili kuweza kupambana na maadui hawa katika pande zote wanazoijia tulizozitaja hapo juu - kufichua na kuteketeza silaha zao na vituo vyao vyote, silaha za kisiasa, kiuchumi, kijeshi na kiitikadi.

Hivi sasa, kama ilivyokuwa hapo zamani, nguzo kuu za siasa ya kichokozi na kikandamizaji ya nchi mbili za kimabavu, yaani ngao kuu zinazotumiwa na nchi hizi katika kulinda mifumo yake ya kibeberu - ngano ambazo ndiyo silaha zao muhimu katika magomvi yao na kujiandaa kwao kwa ajili ya vita - ni NATO (Shirika la Kijeshi la Kujihami la Nchi za Magharibi) na WARSAW TREATY (Shirikala Kijeshi la Kujihami la Nchi za Mashariki), kisha mikataba mbali mbali ya kisiasa na kijeshi iliyowekwa na nchi za kibepari na za kibadilifu pamoja na vituo vyao vya kijeshi na majeshi yenyewe yaliyoko katika nchi nyingi za kigeni.

NATO na WARSAW TREATY, pamoja na majeshi ya kibepari na ya kibadilifu ya nchi zilizo wanachama katika mashirika hayo mawili ndiyo kinga kuu ya ubepari na ubadilifu, na ndiyo jeshi kuu ambalo kazi yake ni kushambulia mapinduzi na ujamaa wa kisayansi, kushambulia uhuru na ukombozi wa wananchi. Mikataba ya kijeshi baina ya nchi mbali mbali ndiyo kinga ya wapinga-mapinduzi na wapinga-uzalendo walioko ndani ya nchi hizo - makundi ya watu ambao wanaziuza nchi zao na kuzifanya zikandamizwe na wageni na hivyo kutokomeza kabisa uhuru wa nchi hizo. NATO na WARSAW TREATY daima vimekuwa na vinaendelea kuwa ni vyombo vya kuandaa na kuanzisha vita............

Mfumo wa kibepari ambao wakati huu unakabiliwa na matatizo ambayo yanazidi kuuzorotesha kama ilivyotabiriwa na akina Marx, Engels, Lenin na Stalin, sasa hivi umefikia ngazi ya ubeberu na ambayo ni hatua yake ya mwisho. Ili uweze kudumu muda mrefu zaidi ubepari umeanzisha njia mbali mbali za kuwanyonya wananchi - sio tu kitaifa bali ulimwenguni pote - umeunda ukoloni-mamboleo ambao ni njia ya pekee na ya hali ya juu sana katika kupora mali ya nchi, umeanzisha mahusiano ya kifedha na mikataba ya kiuchumi na kijeshi ambayo yote kwa pamoja yana nia ya kuzidi kudumisha umaskini wa mataifa mengi yajulikanayo kwa majina ya "dunia ya tatu", "dunia ya pili", "nchi zisizofungamana na siasa ya upande wowote", au "nchi zinazoendelea". Majina yote haya ambayo yanajaribu kutafsiri mitindo mbali mbali ya kisiasa iliyopo hapa duniani sasa hivi, yanaficha na hayafichui hali halisi ya kitabaka na ya kisiasa iliyomo katika nchi hizi, migongano mikuu ya nyakati zetu, suala la kimsingi linalokabili mataifa na ulimwengu mzima - yaani mapambano makali kati ya mabwanyenye wa kibeberu kwa upande

pamoja na ujamaa wa kisayansi, wafanyakazi wa ulimwenguni na marafiki zao kwa upande mwingine.

[illegible] wa majina kama haya hapa juu unatuonyesha [illegible] kiwango kilichofikiwa na [illegible] - wa kitaifa na wa kimataifa - na jinsi [illegible] ya mataifa mbali mbali na [illegible] ulimwenguni. Majina haya pia yanaweza yakatuonyesha kiwango cha [illegible] na [illegible] wa [illegible] na ubeberu na ubeberu-jamii, na vile vile yanaweza kutuonyesha hali iliyopo miongoni mwa watu ya kutaka kujikomboa na kuwa huru kutoka kwa nchi za kibeberu. Kwa kuliangalia suala hili kitabaka - tofauti zilizopo hapa na pale - tutaona kuwa, katika mataifa haya yenye matabaka ya [illegible] na unyanyasaji wa mtu na mtu, na kwamba wafanyakazi pamoja na [illegible] wengine wanakandamizwa na kudhulumiwa na mabwanyenye katika hali mbali mbali. Ujamaa wa kisayansi unatufundisha kuwa katika ulimwengu wa leo nchi zimegawanyika kufuatana na mfumo ya kiuchumi iliyopo katika nchi hizo, yaani nchi zakibepari na nchi za kijamaa (ujamaa wa kisayansi). Nadharia kama ile ihimizayo "njia ya kati isiyo ya kibepari wala kijamaa" ni miongoni mwa nadharia ambazo zimekuwa zikienezwa na wafuasi wa ubadilifu wa Krushov, na nia ya nadharia hizi ni kuhujumu ujamaa wa kisayansi katika nchi hizi na kuleta [illegible] ya kiitikadi miongoni mwa watu na pia kuharibu mapambano ya wapenda amani.

Hali kadhalika kuhusu uchambuzi wa siasa inayofuatwa na mataifa au serikali mbali mbali, wana-ujamaa wa kisayansi hufanya uchambuzi kama huo kitabaka - yaani hutazama msimamo wa serikali na mataifa haya kuhusu ubeberu na ujamaa wa kisayansi, msimamo wao kuhusu umma ulioko nchini na wapinga-mapinduzi.

Kwa kutumia misingi hii, vuguvugu la kimapinduzi na wafanyakazi huweza kujenga strateji na mbinu zao, huweza kupata marafiki wao wa kweli na kuungana nao ili kuendesha mapambano dhidi ya ubeberu, ubepari na upinga-maendeleo. Maneno kama "dunia ya tatu", "nchi zisizofungamana na siasa ya upande wowote", "nchi changa", au "nchi zinazoendelea" huwapumbaza wananchi wanaopigania ukombozi wa kitaifa na kijamii katika kufikiri kwamba wako chini ya paa linalowakinga kutoka vitisho vya nchi za kimabavu. Maneno haya yanaficha hali halisi ya mambo yalivyo katika nchi hizi ambazo kwa ujumla - kisiasa, kiitikadi na kiuchumi zimefungamana na kutegemea nchi mbili za kimabavu na vile vile kufungamana na wakoloni wa zamani.

Wafuasi wa ubadilifu wa Yugoslavia wako katika mstari wa mbele katika kueneza rai ya "nchi zisizofungamana upande wowote". Wanavyoelewa wao ni kuwa "nchi zisizofungamana upande wowote" ni zile zote ambazo hazina mikataba ya kijeshi na mabeberu wakubwa na mabeberu-jamii, hasa mikataba na NATO na WARSAW TREATY. Lakini hata kama hazina mikataba maalum ya kijeshi na mabeberu hawa kwa njia ya NATO na WARSAW TREATY nchi nyingi hizi zimefungamana kabisa na nchi za kimabavu na nchi za kibepari kwa misululu ya mikataba na mapatano mbali mbali kiasi kwamba kule kuziita "nchi zisizofungamana upande wowote" inakuwa ni upuuzi mtupu.

Msimamo halisi wa nchi hizi "zisizofungamana na upande wowote" ulionekana kwenye Mkutano wa Colombo. Kwa taabu kubwa sana jumuia hii ya nchi "zisizofungamana na upande wowote ilifanikiwa kuficha tofauti na migawanyiko ya kisiasa iliyopo na inayoendeshwa miongoni mwa kila nchi

na makundi ya mataifayaliyohudhuria mkutano huo. Katika mkutano huo hakuna hata mmoja aliyeishutumu au kuishambulia bila kuficha Marekani au Urusi na kupinga tabia yao ya uchochezi na uzushi wa vita. Badala yake waliona ni afadhali kuishambulia Ufaransa.

Mataifa mengi yanayojifanya eti hayafungamani na siasa ya upande wowote yanatiliana mikataba ya ulinzi na ya kijeshi miongoni mwao na ambayo mataifa ya kibeberu yanashiriki pia. Na hakuna hata taifa moja lililokataa mikataba hii. Ubeberu-jamii wa Kirusi unajaribu kuanzisha "Asian Security Treaty" (Mkataba wa Kijeshi wa Nchi za Asia), na punde si punde tutashuhudia mkataba kama huo katika bara la Afrika - "African Security Treaty" (Mkataba wa Kijeshi wa Nchi za Kiafrika), n.k. Hivi vyote ni vyombo mbali mbali vyenye shabaha ya kuifanya nchi "isiyofungamana na siasa ya upande wowote" iendelee kukandamizwa kwa kila hali.

Msemo wa "nchi zisizofungamana na siasa ya upande wowote" ni msemo unaodanganya na unaojaribu kuonyesha kuwa jumuia ya nchi ambazo ina uwezo wa kupambana na ngome ya nchi za kimabavu imeundwa. Mtu anaweza ukafikiri kuwa nchi zote hizo - bila ya kuacha hata nchi moja zinapinga ubeberu, zinapinga vita, zinapinga udikteta, na kwamba ni nchi zinazofuata demokrasi na siasa ya ujamaa wa kisayansi. Hii inasaidia kudumisha ufisadi na demokrasi ya uwongo iliyomo katika baadhi ya nchi hizi "zisizofungamana na siasa ya upande wowote" na vile vile msemo huu unasaidia kuwafanya watu katika nchi hizi waamini kwamba viongozi wa nchi zao wanapoanzisha au kuvunja mahusiano yale ya aina yoyote na mabeberu na mabeberu-jamii kwa njia ya siri au bila kuficha wanafanya hivyo siyo tu kama wawakilishi wa "serikali za wananchi" lakini pia kama jumuia ya mataifa ambayo haiwezi kuchezewa hata nchi za kimabavu.

Chama chetu kinafikiri kuwa wananchi ni lazima waelezwe ukweli wa hali ya mambo bila kuficha kitu chochote, kwani ni kwa kufanya hivi tu ndipo umoja thabiti - umoja wa mataifa na serikali zipendazo maendeleo dhidi ya ubeberu - unaweza kuimarishwa. Ili kuweza kuunganisha umma katika kupigania uhuru na maendeleo ya kijamii dhidi ya ukandamizaji na unyonyaji unaofanywa na yeyote yule, ni muhimu kwanza kuweka mstari na kufafanua adui halisi ambaye wananchi watapambana naye na vile vile kufafanua yule rafiki ambaye wananchi wataungana naye.

Adui wa wananchi ni ubeberu, ubeberu-jamii na mabwanyenye wakubwa wa ulimwengu ambao kwa ujumla wanafuata siasa ya upanuzi na unyonyaji katika nchi za Asia, Afrika na Marekani-Kusini. Nchi za kimabavu na mtaji wa kimabavu wana shabaha ya kudumisha vyombo na taasisi zote za kitaifa zilizoundwa wakati wa ukoloni. Itokeapo kwamba maslahi yao yako hatarini, angalau kidogo tu, kama vile kupanda kwa bei ya mafuta na malighafi nyingine, basi watakuja juu na wako tayari hata kuzusha vita dhidi ya wananchi wanaotaka milki kamili juu ya mali yao na wanaopigania haki na usawa katika masuala ya kibiashara na uchumi wa ulimwengu.

Hata hivyo, hali hii ya wizi na unyonyaji wa kinyama haiwezi ikaendelea milele. Wakati huu vita vya kutaka uchumi uwe mikononi mwa wananchi ni vita vilivyopo kila mahali na hakuna hata mtu mmoja atakayeweza kuzuia vuguvugu hili la kimapinduzi lililoenea ulimwenguni kote. Wananchi wana haki ya kuwa na milki kamili juu ya mali ya

asili ya nchi zao na pia wana haki ya kuitaifisha mali hiyo. Vita na ulipizaji kisasi unaofanywa na mabeberu dhidi ya haki hii ya wananchi ni vita kali sana, lakini hata viwe vikali na virefu namna gani, vita hivi haviwezi kamwe kuzuia kupatikana kwa haki hii. Hakuna kitu kitakachozuia mapambano ya wananchi katika jitihada yao ya kutafuta usawa katika biashara ya kimataifa na katika kuhakikisha kuwa mapato yatokanayo na uuzaji wa malighafi yanatumika kukuza viwanda na utamaduni na kuinua hali yao ya maisha. .......

Kwa njia ya biashara ya zana za kivita, mataifa ya kimabavu yanaongoza ushindani wa kununua zana hizi miongoni mwa mataifa madogo, na hii huwa ndiyo kiini cha magomvi na nchi za jirani na baadaye kusababisha vita kati yao kitu ambacho huleteleza kuingilia kati na ukandamizaji wa Marekani na Urusi. Kwa uuzaji wa zana za kivita, pamoja na matisho ya vita - ambayo ndiyo propaganda kubwa inayotumiwa - mataifa haya mawili ya kimabavu yanajaribu kujipenyeza katika Afrika, Mashariki ya Kati, Marekani-Kusini, na Asia.

Katika nchi hizi, Marekani na Urusi zinashindana katika kujipenyeza. Kusudi yaweze kukandamiza baadhi ya nchi katika kanda hizi, mataifa mawili haya ya kimabavu huanzisha na huunda serikali za vibaraka yakisingizia kwamba yanaleta ukombozi na baadaye kuwachonganisha wakitumia kanuni ya "kutenganisha na halafu utawale". Kusema kweli, uwe ni ubeberu wa Kimarekani - ambao ni wa kimacho-macho na wa kinyama - au ubeberu-jamii wa Kirusi ambao vile vile ni wa kinyama ila tu unajificha kwa propaganda ya kusema Urusi yenyewe ni nchi ya kijamaa - lakini nchi zote mbili kwa pamoja zinahatarisha amani, zinachochea na kutia moto migongano miongoni mwa wananchi kwa manufaa ya nchi hizo mbili zenyewe, zinajenga vituo vya meli za kivita katika baadhi ya nchi, zinaanzisha mikataba ya kijeshi, zinaanzisha mikataba ya kibiashara inayokandamiza, n.k.

Moja kati ya mifano inayodhihirisha siasa ya nchi hizi mbili za kimabavu ni Mashariki ya Kati - ambapo suala kuu ni la mafuta. Uhasama uliopo kati ya wananchi Waarabu na Uyahudi, hali yenyewe ilivyo kati ya Waarabu wenyewe - ambao wamegawanyika na kutoelewana kati yao (hali ambayo inadumishwa na kuzoroteshwa kwa njama za Marekani na Urusi) ni matokeo ya suala hili: nchi hizi mbili za kimabavu zinajitahidi sana kutaka kupora mafuta. Damu ya wananchi wa Kiarabu imekuwa ikimwagika na inaendelea kumwagika kwa sababu ya mali hii. Ubeberu wa Kimarekani unaisaidia Uyahudi kimacho-macho ili nchi za Kiarabu ziendelee kutengana. Urusi inajifanya eti kuwasaidia wananchi wa Kiarabu kwa kuwauzia silaha hali wakati huo huo inasafirisha idadi kubwa ya Warusi wenye dini ya Kiyuda huko Uyahudi ambako wanatumiwa katika mapambano dhidi ya wananchi wa Kiarabu.

Wakati huo huo mataifa ya kimabavu yanashindana menyewe kwa menyewe. Licha ya kuwa rafiki mpenzi wa Uyahudi, ubeberu wa Kimarekani umeweza sio tu kudumisha "urafiki" wake na Saudi Arabia na Umoja wa Falme za Kiarabu, lakini umeweza pia kuzorotesha nafasi ya Urusi katika eneo hili. Kuvunjika kwa mkataba kati ya Urusi na Misri pamoja na kufukuzwa kwa meli za kivita za kichochezi za Urusi kutoka bandari za Misri ni pigo kubwa, si ushindi kwa ubeberu-jamii wa Kirusi.

Kwa sasa, Marekani ndiyo inaonekana kufanikiwa katika kuongoza mipango yao katika eneo hili. Hapana shaka, ubeberu-jamii wa Kirusi haukai kimya tu na kukunja mikono yake. Warusi wanajaribu kuziba pengo lililotokea nchini Misri kwa kushikilia zaidi na zaidi nchi zile za Kiarabu ambapo tayari wanao uhusiano au kwa kutafuta sehemu mpya au vilevile kwa kujishikiza na "marafiki" wapya.

Katika Bara la Afrika, mapambano kati ya nchi mbili hizi za kimabavu hivi sasa ndiyo yameanza na mapambano haya hayatakwisha hivi karibuni. Ubeberu wa Kimarekani umekwisha kujenga mizizi yake katika Bara hili tangu siku nyingi. Maslahi ya ubeberu huu yanawiana na maslahi ya nchi za Ulaya-Magharibi - ambapo kwa pamoja ni kipingamizi kikubwa kwa Urusi ambayo inataka kujipenyeza katika Bara hili.

Mambo yanayotokea Angola yanachukuliwa kama ni "ushindi" mkubwa kwa Urusi - kwani ni kitu ambacho kinasaidia kuufanya ubeberu-jamii uonekana kama ni mkombozi wa wananchi. Vile vile Urusi inasaidia ubeberu wa Kimarekani na ubepari kwa ujumla kuchochea hofu na vita dhidi ya ukomunisti, ingawa matokeo ya Angola hayana uhusiano wowote na ukomunisti. Mapambano ya sasa ya wananchi wa Afrika ni mapambano dhidi ya siasa ya kuingilia kati katika mambo yasiyowahusu inayo-fuatwa na nchi mbili hizi za kimabavu pamoja na unyonyaji wa nchi hizo.

Mataifa makubwa ya kibeberu yanatumia kwa manufaa yao hali mbaya ya kiuchumi na kijamii iliyopo katika nchi za Kiafrika kwa kufanya hila na njama zisizo na kipimo. Njama hizi zisizokwisha zina madhumuni ya kudumisha Bara kubwa kama hili lenye idadi kubwa ya watu ambao wameishi katika umaskini kwa karne nyingi lakini ambao wana utamaduni wa kijadi, na nguvu mpya ambazo ubeberu, ubeberu-jamii na mtaji wa ulimwengu haviruhusu kutumika katika njia sahihi ya kuleta maendeleo, uhuru, demokrasi na uhuru kamili, na umilikaji mali ulio wa manufaa kwa mataifa haya.

Chama chetu kinaamini kuwa itokeapo kwamba mataifa ya kimabavu au yanaungana au kugombana, wanaoumia daima ni wengine. Kuungana na kugombana kati ya mataifa ya kimabavu ni sura mbili za mgongano thabiti - ni ishara ya strateji moja ya ubeberu, yaani kuzuia uhuru wa wananchi na kukandamiza ulimwengu mzima. Yote haya yana hatari moja, kwa hivyo nchi hizi mbili za kimabavu ndizo adui mkubwa na wa kwanza kwa wananchi. Ndiyo sababu mtu asije hata mara moja kutegemea ubeberu wa nchi mojawapo kupigana au kutengana na ubeberu wa nchi ya pili.

Kuna baadhi ya mataifa ambayo, ingawa yanaelewa hatari iletwayo na moja kati ya nchi hizi mbili au kuelewa hatari ya nchi zote mbili za kimabavu, lakini bado yanategemea ulinzi wake kutoka Marekani au Urusi. Ukweli ni kwamba ulinzi kutoka kwenye mataifa ya kimabavu ni ndoto tu kwa sababu shabaha ya ulinzi kama huo ni kuifanya nchi "inayo-lindwa" kuwa koloni. "Ulinzi" kutoka mataifa ya kimabavu kila mara unaambatana na udunishaji wa kisiasa na kiuchumi - yaani kudunisha uwezo wa taifa kumiliki mali ya taifa na pia kuweka vikwazo katika kujiamulia wao wenyewe maswala ya kitaifa na ya ulimwengu.

Wananchi wasipumbazwe na "upinzani dhidi ya ubeberu" ambao unaenezwa na mabeberu-jamii wa Kirusi ambao shabaha yake ni kuwaunganisha wale wote wanaopinga ubeberu wa Kimarekani na kuupiga vita. Kwani kuungana na "upinzani"

huu ni kutoa mhanga maslahi ya nchi yako, kuhatarisha maisha ya wananchi na pia kuwa kibaraka wa mabeberu-jamii na vile vile kuwa chombo cha kukingia hulka zao. Migongano kati ya Urusi na Marekani si migongano baina ya ujamaa wa kisayansi na ubepari kama tunavyoelezwa na Moscow, bali ni migongano kati ya mataifa mawili ya kibeberu.

Wakati tunashutumu uongo na mbinu za uongo za "upinzani dhidi ya ubeberu" zinazoenezwa na wabadilifu wa Kirusi ni muhimu vile vile kushutumu "upinzani dhidi ya ubeberu-jamii" unaoenezwa na Marekani na mabepari hodhi wa ulimwenguni. Wananchi hawawezi kamwe kukubali kuumia wakati Marekani na Urusi wanapogongana na kuwa vyombo vinavyotumiwa na mabeberu katika njama zao za kibeberu........

Ujamaa wa kisayansi unatufundisha kuwa ubeberu na wachochezi wa vita watadhoofishwa kwa harakati za kimapinduzi na ukombozi wa wananchi. Iwapo vita vya uchochezi vya kibeberu haviwezi kuzuiwa, basi, ni jukumu la wana-mapinduzi na wafanyakazi kuvifanya vita hivyo kuwa vita vya ukombozi.

Ni muhimu wananchi kuelezwa kuwa maadui wa mapinduzi na wafanyakazi wa ulimwengu mzima, maadui wa uhuru na watu wote wanaokandamizwa, wachochezi na chanzo cha vita ni ubeberu wa Kimarekani, ubeberu-jamii wa Kirusi na mabwanyenye wapinga-mapinduzi wa kila nchi. Mataifa haya ndiyo yanayowakilisha mfumo wa kinyama wa kibepari na ambao kiini na shina la nguvu zake ni unyonyaji wa kinyama wa wananchi. Mapambano makali na marefu ni lazima yafanywe dhidi ya mataifa hayo ya kinyama, dhidi ya itikadi zao za aina mbali mbali zitolewazo toka vyama vya kisiasa, makampuni hodhi ya ulimwengu na vyombo vidogo vidogo vya kitaifa na vya ulimwengu mzima; toka kwenye mabenki na miungano ya kisiasa na ya kijeshi na majeshi yenyewe -- hadi mwishowe kuvunjwa kwa nguvu za kidogo na kung'olewa kwa mizizi yake.

Hali ya mambo kama ilivyo sasa inaonyesha kuwa vita hivi vikali ni lazima vipigwe na wananchi wote wa ulimwengu mzima, na watu wote wapenda amani ambao wana moyo wa kizalendo wa nchi zao na ambao uendeshaji wa harakati hizi ndilo jukumu kubwa maishani mwao. Iwapo harakati hizi zitaongozwa na wafanyakazi wa ulimwenguni chini ya Chama cha kikomunisti ambacho kinaongozwa na nadharia sahihi ya ujamaa wa kisayansi, basi harakati hizi zitakuwa ngumu, kali na kubwa.

Mabeberu na mabeberu-jamii wana wapenzi wao, nao ni mabepari wapinga-mapinduzi waliomo katika kila nchi wanamotawala. Mabeberu hawa wanawatumia mabepari hawa katika njama zao na ndio wanaokandamiza wananchi kwa niaba yao. Kwa hivyo huwalisha na kuwahami mabepari hawa ili wawe imara katika machafuko ya ulimwengu na pia waweze kuwa ngome kubwa dhidi ya wananchi pindi wanaposimama na kufanya mapinduzi dhidi ya wakandamizaji waliomo ndani ya nchi na walio nje ya nchi. Kwa hiyo mabeberu wa nje na wawakilishi wao waliomo ndani hawawezi wakatenganishwa. Bila ya kupambana na yule aliyemo ndani, huwezi ukapambana na yule aliyeko nje; bila ya kupambana na yule aliye ndani hadi kumpindua - huwezi ukapambana na yule aliyeko nje. Kwa maana nyingine, haiwezekani kuzuia vita. Ni muhimu kuvunjilia mbali kila aina ya vituo vilivyoenezwa na mataifa ya kimabavu katika kila nchi; kwani kwa kufanya hivyo unaweza kudunisha na kuvunjilia mbali ueneaji na uwezo wao ambao mizizi yake inatokana na ukandamizaji wa wananchi.

Ni lazima tutegemee uandalizi thabiti wa wananchi na umoja wa wale wote wanaopinga minyororo ya mabeberu na mabeberu-jamii. Tunazingatia umoja wa wafanyakazi wa ulimwengu na wote ambao ni wapinga-ubeberu na wapenda amani ambao kutokana na harakati zao siku moja wataweza kuvunjilia mbali njama za kichochezi za mabeberu na mabeberu-jamii.

Kikizingatia ujamaa wa kisayansi, Chama cha Wafanyakazi cha Albania pamoja na wananchi wa Albania wamekuwa na wanaendelea kuendeleza upinzani dhidi ya mataifa mawili ya kimabavu, dhidi ya vita vya kibeberu, dhidi ya mabepari hodhi na wapinga-mapinduzi wa ulimwengu. Kwa hivyo hata katika siku za usoni hawatalega-lega katika jitihada yao na wataendelea kupigana vita bega kwa bega na wananchi wote wapinga-ubeberu na ubeberu-jamii, bega kwa bega na vyama vyote vya kisiasa vya wafanyakazi, wanamapinduzi na wafanyakazi wa ulimwenguni na wale wote wapenda maendeleo ili waweze kufichua njama za maadui na ili kuhakikisha kuwa juhudi za kutafuta uhuru na amani kwa wananchi zimefanikiwa.

Kila wakati nchi yetu itasimama bega kwa bega na wananchi wowote wale ambao uhuru wao unahatarishwa na ambao haki zao zinanyang'anywa. Tunatamka msimamo huu kila mara na sio tu katika nyakati za baraka bali hata katika siku za dhiki. Wananchi kote ulimwenguni wanahakikishiwa kuwa nchi ya kijamaa ya Albania iko nao bega kwa bega na haigopi kutoa misaada ya aina yoyote ile.

****** ******

USHAIRI NA UKASUKU

(Uchambuzi wa Mashairi ya Miaka Kumi ya Azimio la Arusha)
(Kiliçhotungwa na Kuchapishwa na UKUTA)

M.M. MULOKOZI

Ili kuadhimisha miaka kumi ya Azimio la Arusha, chama cha Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania (UKUTA) mwaka 1977 kimetoa kijitabu cha Mashairi ya Miaka Kumi ya Azimio la Arusha. Mhariri wa mkusanyo huu wa mashairi thelathini na mane ni Abdilatif Abdalla, mtungaji wa Utenzi wa Maisha ya Adam na Hawaa[1] na ile diwani maarufu ya mashairi ya mapambano, Sauti ya Dhiki.[2] Kutokana na mashairi na maandishi yake mengine tunajua kuwa Abdilatif ni mshairi mwenye ubingwa mkubwa kisanaa na mtazamo wa kimaendeleo kisiasa. Bali hii haina maana kwamba hata mashairi haya aliyoyahariri ni mazuri kisanaa na kwamba ni ya kimaendeleo kimaudhui; kwani mashairi haya hayawakilishi msimamo wa mhariri bali yanawakilisha msimamo wa UKUTA na wa washairi wenyewe walioyaandika.

Huu si mkusanyo wa kwanza wa mashairi yahusuyo Azimio. Mkusanyo wa kwanza, Mashairi ya Azimio la Arusha,[4] ulichapishwa mwaka 1971. Diwani hiyo ilikusanywa wakati wa shamra shamra za kushangilia kuzaliwa kwa Azimio, maana washairi wengi waliliona Azimio kuwa lilikuwa ni ushindi mkubwa wa 'wakulima na wafanyakazi' wa Tanzania dhidi ya wanyonyaji, hasa mabepari wa kigeni.

Diwani hii ya sasa imekusanywa baada ya shamra shamra hizo kupoa na watu kuanza kutafakari kwa undani na makini zaidi maana, ubora na upungufu wa Azimio kinadharia na kiutekelezaji. Kwa namna fulani diwani hii ni kigezo cha maendeleo ya miaka kumi katika uwanja wa fikira na fasihi ya kijamaa. Hivyo, ili kuyapima kwa usahihi mafanikio hayo itatubidi kwanza kuipitia kwa ufupi diwani ya Mashairi ya Azimio la Arusha iliyotolewa mwaka 1971.

Mtu asomapo Mashairi ya Azimio la Arusha jambo lidhihirikalo upesi ni ule msisimko wa furaha iliyosababishwa na kutangazwa kwa Azimio. Furaha hiyo ya 'ushindi' na matumaini makubwa inajitokeza dhahiri katika beti zifuatazo:

Matanga yamebetuka, chombo kina mteleo
Wala hakitapinduka, chenda Bara na Mwambao
Wenyewe twachekacheka, nje mwabaga kilio.....
(Said M. Nurru, uk. 3)

Nimesikia kelele, mayowe mengi ya watu
Wakimtaja Nyerere, Mwalimu Rais wetu
Lele lele lele, karudisha mali zetu.....

Tupige vigelegele, huu ndio mwaka wetu
Azimio lile lile, litatuvika viatu
Tuwakanyagie wale, wanyonyaji wa damu zetu......
(Yohana Mwanishi (Vurugu) uk. 20)

......../2

Mshairi, Said Nurru, hashangilii tu Azimio bali anaeleza imani yake kuwa litafaulu: 'chombo kina mteleo'; haki kwenda mrama. Beti za Yohana Mwanishi zinaonyesha shangwe tupu: 'lele lele.... tupige vigelegele'. Kina cha le kinakaririwa ili kuleta taathira ya hoi hoi na furaha iliyokuwa imeenea mchini kote wakati huo.

Washairi hawa na wengine ambao mashairi yao yamo katika diwani hiyo waliamini kwamba Azimio limewakomoa mabepari - hasa wa kigeni - na sasa uchumi uko mikononi mwa wananchi wenyewe: maendeleo na mafanikio makubwa yako usoni; ujamaa utafaulu.

Pamoja na kuliimbia 'haleluya' Azimio, washairi wengi walikisifu chama cha TANU kuwashangilia viongozi kwa kufanya uamuzi huo wa kujenga ujamaa. Mshairi, Mamba Maghaile, alieleza mawazo na hisi za washairi wengi alipomsifia Rais Nyerere hivi:

Kiongozi kama huyu, ni wapi atatokea?
Mwenye nyingi taghamuyu, ishangazayo dunia
Ya Rabi mlinde huyu, nyota ya Watanzania
Ni wapi atatokea, kiongozi kama huyu?
(Mamba Maghaila, uk. 113)

Shairi hili linaonyesha mambo mawili: Kwanza linaonyesha kuwa mshairi huyo na wote anaowawakilisha waliliafiki na kuliunga mkono Azimio. Yaani waliikubali siasa ya ujamaa kama ilivyoelezwa katika Azimio la Arusha. Pili, ubeti huu unadhihirisha upungufu wa kinadharia wa washairi wengi waliolisifia Azimio--wengi waliamini kuwa ujamaa huletwa na viongozi (au unaweza kuletwa na viongozi), yaani huanzia juu na kutelemka chini kwa watu kama 'neema' ya miungu au watawala. Mtazamo huu mpotofu ulisababishwa na hali halisi ya kihistoria kama ilivyoonekana kijuujuu, maana ni kweli kuwa uamuzi wa kujenga ujamaa haukutokana na harakati za watu wa tabaka la chini kukamata dola, bali ulitangazwa na viongozi huko Arusha. Jambo ambalo washairi wengi hawakuliona ni kwamba viongozi hawakufanya uamuzi huo kwa hiari na imani yao tu, bali palikuwa na msukumo wa kisiasa na kiuchumi kutoka chini, miongoni mwa wafanyakazi, wakulima na wanafunzi ambao hawakuridhika na mkondo wa maendeleo yetu baada ya uhuru.[5]

Msisimko wa kisiasa uliolikumba taifa uliwazindua hata waliokuwa hawajapata kutunga mashairi katika maisha yao, wakajikuta wanapagawa na 'buruhani' ya ujamaa. Bi Tatu Rashid Malenda ni mmoja wa washairi ambao usanifu wao ulizinduliwa na Azimio. Anakiri kuwa:

Maisha sijaandika, kulituma gazetini
Mwaka huu kuandika, yamenikuna moyoni.....
(Tatu Rashid Malenda, uk. 47)

........./3

Habari njema za ujamaa 'zilimkuna moyoni' Bi. Tatu Rashidi M...., na akaamua kuuhama mji kurejea kwao Rufiji kulima:

> .......Msako utapofika, mami nimo safarini
> Nakwenda kwetu Rufiji, kulima mpunga na pamba

Sawa; lakini je, ujamaa utamsaidia vipi mwanamke katika mapambano yake ya kujitoa katika unyonge; utamkomba au atabakia tu kuwa mtumwa wa suala hilo, madhali yu mwanamke, haoni ubaya wa mgawanyo wa kazi unaomweka jikoni daima;

> Beti tisa kituoni, edita kaka saini,
> Bi Nuru nipe ...., nakimbilia jikoni...(mkazo ni wa mhakiki)

Pamoja na kukunwa moyoni, Bi Tatu bado hali yake haijabadilika: anakimbilia jikoni!

Si mashairi yote katika mkusanyo wa kwanza yalikuwa ni ya kushangilia na kukaribisha tu Azimio. Mengi mengine yalikiuka kiwango hicho na kuhimiza hatua kali zaidi zichukuliwe kuimarisha na kuendeleza ujamaa. Iliwadhihirikia baadhi ya washairi kuwa kutaifisha mabenki tu kulikuwa hakutoshi kuleta ujamaa; hivyo ndivyo alivyosema mshairi Himaka:

> Mirija tumeikata, matawi yamesalia
> Matawi yana matata, kama tusipochungua
> Yafaa kuyatafuta, au tutaangamia
> Wananchi tushikane, tuyakusanye matawi
> (H.S.Himaka (Sitaki Matata, uk. 82)

'Matawi' ni mirija ya ndani ambayo, japo ilikuwa imenyang'anywa --kwa kiasi fulani-- mhimili wake wa kimataifa, lakini ilikuwa bado ina uwezo wa kukwamisha mapinduzi.

Washairi wengine walielewa kuwa kutangaza ujamaa ni mwanzo tu wa mapambano makali ya kiujenzi, kiulinzi na kitabaka. Kwa wengi, ujenzi maana yake ulikuwa ni uendelezaji wa kilimo. Hawa mawazo yao yalilingana ya yale ya Azimio; hawakuelewa ya kuwa haiwezekani kujenga ujamaa bila ya kuwa na viwanda vikubwa vya kuuwezesha uchumi kujitosheleza na kujitegemea.

> Babu walikusanyika, shambani kujilimia
> Na sisi tukiishika, njia waliyopitia
> Nchi itasafishika, nuru itatuenea.....
> (Khalfani Ramadhani, uk. 56)

Madhali babu zetu walikuwa wakulima, basi nasi pia tutaendelea kwa kutegemea kilimo tu! Huu ni mtazamo finyu usiokuwa wa kisayansi, unaotukuza kila jambo la kale na kuwania kuirudisha historia nyuma, jambo ambalo haliwezekani. Ni kweli kuwa babu zetu walikuwa wakulima, na labda ndio maana mfumo wao wa jamii ulianguka kwa urahisi mara tu ulipogongana na mfumo ulioendelea zaidi wa ubepari wa viwanda. Ili kuushinda ubepari huo uliotutiisha mwishoni mwa karne iliyopita, inatubidi kuasisi mfumo ulioendelea zaidi kuliko ukulima wa babu zetu na ubepari wa Kimagharibi

............/4

Wapo washairi wachache waliopendekeza viwanda vikubwa viimarishwe, ili vikasaidiane na kilimo, kujenga uchumi wa kijamaa unaojitegemea. A.M. Pazi alisema:

Kama hoja ya kuchuma, na ndio huu msingi
Pato huja kwa kulima, na kuunda vitu vingi.......
(<u>A.M. Pazi</u>, uk. 75)

Pamoja na kujenga, lazima kile kinachojengwa kilindwe; alihimiza Yasini Ndevumbili:

Majeshi yawe imara, tusivamiwe ghafla
Yalinde pwani na bara, au popote mahala.......

na akatahadharisha kuwa majeshi ya polisi yasitumike kukandamiza watu:

.....Na yapunguze bakora, kupiga walio jela
Tuzingatie ahadi, za kujenga ujamaa
(<u>Sh. Y.Ndevumbili</u>, uk. 92)

Jambo ambalo Ndevumbili hakulielewa sawa sawa ni kwamba jeshi ni chombo cha kikandamizi cha dola, na dola ni mwakilishi wa tabaka linalotawala. Jeshi linatimiza tu wajibu wake kwa tabaka lililoliajiri. Kwa hiyo si ajabu kuwa katika nchi nyingi za Afrika polisi bado wanatandika watu viboko (sio watu waliofungwa tu, bali hata raia 'huru').

Mashairi mengi katika <u>Mashairi ya Azimio la Arusha</u> yalirudia mambo yale yale yaliyosemwa katika Azimio lenyewe, ila yaliyasema kisanaa zaidi kwa vina na mizani. Yapo baadhi ya mashairi ambayo yalikiuka mipaka ya itikadi ya Azimio ya kuleta mapinduzi ya jamii kwa njia za amani. Haya yalisisitiza harakati za kitabaka na kuwaonya wanyonyaji kuwa tabaka la wafanyakazi,na wakulima li tayari kutumia mabavu dhidi ya maadui zake. Abdu Lugude Mkumbu alimshauri Rais hivi:

Wanyonyaji uwanyonge, twakuomba wana wako
Uwanyang'anye matonge, warudi watokeako....

Haitoshi kukata mirija ya wadhalimu--sharti wanyongwe, waangamizwe kabisa. Mlio wa vina vya <u>nge</u> na <u>ko</u> unatilia nguvu maudhui hayo yahusuyo matumizi ya mabavu katika harakati. Mshairi aliendelea:

Hii mijitu ya lana, irudishe itokako
Ufanye haraka sana, uichape na viboko....
(<u>A.L. Mkimbu</u>, uk. 39)

Kuchapa viboko maana yake ni kuwakandamiza wakandamizaji, siyo kuwahurumia na kuwalipa fidia.

Katika shairi jingine, "Usihofu Vibaraka", Mkimbu aliiendeleza fikra hiyo ya matumizi ya mabavu dhidi ya wapinzani wa ujamaa:

Hii sasa dola yako, kakujalia Rabuka
Usihofu vifumoko, wasopenda ushirika
Yafaa wachape mboko, heshima wasipoweka
Usihofu vibaraka, timiza wajibu wako
(<u>A.L. Mkimbu</u>, uk. 53)

....../5

Rai hii iliungwa mkono na Saidi M. Nurru ambaye alisema:

> Tupo imara kabwela, kwa mapanga twawasheta
> Hatuna tena kulala, japo mvua kunyonyata
> Japo mkifanya hila, sisi tutazikung'uta
> Asemae hatuwezi, huyo anajidanganya........
>
> (Said Nurru, uk. 47)

Mkimbu na Said Nurru ni washairi wenye fikira za kimaendeleo. Tunaweza kuwalinganisha na mshairi wa kijamaa wa Kirusi, Vladimir Mayakovsky (1893-1930).[6] Mshairi huyo aliliona suala la harakati za kitabaka kuwa ndilo kiini na nyezo kuu ya vuguvugu la kujenga ujamaa. Hata hivyo mtazamo wa kidini uliyaathiri mashairi ya Mkimbu na Nurru. Mathalan Mkimbu anafikiri dola ' ya kijamaa' hutoka kwa Mungu: "Hii sasa dola yako, kakujalia Rabuka". Hii si kweli, dola yoyote ile ni matokeo ya mapambano baina ya matabaka ya watu hapa hapa duniani-dola ni chombo cha utekelezaji wa madaraka ya tabaka linalotawala. Vivyo hivyo kwa kiasi kikubwa dini ni chombo cha kuendeleza itikadi ya tabaka linalotawala.

Pamoja na dosari zake zote, Mashairi ya Azimio la Arusha ni mkusanyo wa kwanza wa mashairi ya kimaendeleo kiasi hicho katika fasihi ya Kiswahili. Mengi ya mashairi yaliyomo yaliwakilisha fikira na hisi za kweli za umma wa wakulima na wafanyakazi wa Tanzania wa miaka ya 1967-1971. Kulingana na hali ya wakati huo, ilikuwa ni vigumu sana kwa washairi hao kukiuka kiwango cha itikadi ya Azimio la Arusha na kuweza kuona mbele zaidi, kutambua matatizo na ugumu wa kujenga ujamaa, na kuzibainisha nguvu za kitabaka zilizokuwapo katika jamii yetu. Sasa, baada ya miaka kumi, ni rahisi zaidi kuyaona matatizo hayo, na hivyo ni rahisi zaidi kukata tamaa na kufikiri kuwa ujamaa hauwezekani kujengwa Afrika. Hatutarajii mshairi wa leo, ambaye si mnafiki, kushangilia tu 'mafanikio' ya miaka kumi ya Azimio bila kuonyesha matatizo halisi ambayo yameikabili Tanzania katika miaka hiyo kumi.

Namna itakavyokuwa, kiuchambuzi na kiitikadi, kama si kwa fani, tungetarajia mkusanyo wa Mashairi ya Miaka Kumi ya Azimio la Arusha uwe bora zaidi ya ule wa kwanza. Lakini hivyo sivyo ilivyo. Kwa nini?

Labda sababu mojawapo iliyoudumisha mkusanyo huu wa pili ni kwamba washairi wameandika kutokana na wito maalumu wa chama chao cha UKUTA; hawakuandika kutokana na musuko tu wa moyoni, au chambilecho mshairi Tatu Rashidi Malenda, hawakuandika kwa kuwa mafanikio ya miaka kumi ya Azimio yalikuwa 'yamewakuna moyoni'. Kwa upande mwingine, mashairi ya diwani ya kwanza hayakuandikwa kutokana na wito wa mtu yoyote, bali yalikusanywa kutoka katika magazeti ya Uhuru na Ngurumo; washairi waliyatunga kwa hiari yao tu bila kushawishiwa au kuombwa na mtu yoyote. Kwa vyovyote vile kosa haliwezi kuwa limetokana na mhariri wa diwani hii, Abdilatif Abdalla, maana utangulizi wake

mwenyewe unaonyesha kuwa hakuyachagua mashairi aliyoyachagua kwa kuwa yalikuwa bora sana bali kwa kuwa ndiyo yaliyokuwa mazuri zaidi miongoni mwa yale aliyoletewa. Kwa hakika, utangulizi wa mhariri unayakejeli mashairi yaliyomo kitabuni, licha ya kuwa umepevuka zaidi kifikira na kiitikadi kuliko mashairi yenyewe. Kama kuna sababu yoyote ya kukinunua kitabu hiki cha Mashairi ya Miaka Kumiya Azimio la Arusha zaidi ni kwa ajili ya utangulizi wake kuliko yale yaliyomo.

Katika utangulizi, Abdilatif anatupa tahakiki kamili ya mashairi yaliyomo katika kitabu alichokihariri; na anawapa rai washairi wa Kiswahili, rai ambayo lau wakiifuata wanaweza wakaunufaisha ushairi wao.

Kwa vile diwani hii imetolewa kuadhimisha miaka kumi ya Azimio la Arusha, mhariri katika utangulizi anaanza kwa kutueleza maana ya siku hii: Azimio ni nini, lilianzaje na kwa nini tuliadhimishe. Tofauti na washairi wake, Abdilatif anatambua kwamba kutangazwa kwa Azimio hakukufuta matabaka wala hakukuondoa unyonge katika Tanzania. Abdilatif anasema, "Azimio la Arusha halikuifanya Tanzania kuwa ni nchi ya Ujamaa na Kujitegemea mujaribu tu wa kutangazwa kwake, Wala mpaka hivi leo, baada ya miaka kumi kupita, bado Tanzania haijalifikia lengo hilo....." (uk. 2). Huu ni ukweli ambao kutokuuelewa--ambako hasa ni kutokuelewa ujamaa ni kitu gani--ndiko kulikoyafanya baadhi ya mashairi katika diwani hii yawe ya kidhanifu, ya kusifia tu mafanikio ya ujamaa na kujidanganya kuwa hivi leo 'shida hakuna tena' (Tazama uhakiki wa shairi la Ndevumbili, uk. 00)

Hata hivyo, mhariri vile vile anateteraka kidogo kwa kusema kuwa "kabla ya uhuru kupatikana TANU ilikuwa imekwisha jua fika aina ya nchi iliyokuwa inataka kuijenga na ikawa tayari ishaweka misingi ya falsafa itakayofuatwa na nchi". (uk. 3). Ingawa ni kweli kuwa Rais Nyerere alianza kuzungumzia 'Ujamaa wa Kiafrika' tangu mwaka 1962, lakini 'ujamaa' huo haukuwa na maana sawa na ujamaa tunaouzungumzia. Kwa kweli 'ujamaa' huo haukukataa ubepari. Mwalimu alisema: "..... Katika Tanzania, vuguvugu la wananchi la miaka ya 1950 na miaka ya mwanzo ya 1960 lilikuwa ni la kudai uhuru. Tulipinga ukoloni, tulipinga kutawaliwa na wageni, bali hatukupinga ubepari, na wala hatukupigania ujamaa." 7

Jambo kubwa analolijadili mhariri katika utangulizi ni kuhusu wajibu wa mshairi (au mwandishi) kwa jamii yake. Abdilatif anaona kuwa wajibu mkubwa wa mshairi ni kuisaidia jamii yake kujikomboa, kuendelea, kujenga ujamaa. Na ili mshairi au mwandishi atimize dhima hii, sharti mshairi ajielimishe, aichambue jamii yake barabara na kuelewa nguvu za kitabaka na kihistoria zinazoisukuma mbele jamii hiyo, na aishi na watu na kushiriki kwa matendo katika maisha na harakati za wanyonge ambao anawatetea kwa kalamu yake.

unasisitiza kuwa fasihi imefungamana na migogoro na mahusiano ya kijamii, na lazima itoe picha ya kweli ya mambo hayo. Abdilatif anasema "fikira za jamii fulani kuwa zimezongeka katika minasaba ya uhusiano ya jamii hiyo; na kazi zote za fasihi (au tuseme sanaa yote kwa jumla) huwa hazijizukii tu vivi hivi kimiujizaujiza au hazizwi ni fikira za kipekee za watunzi hao ambao zatokana na saikolojia zao zisizoweza kueleweka....." (uk. 7)[8]

Huu ni mtazamo sahihi kabisa na ambao unatangua udhanifu ulioenea katika uwanja wa nadharia ya fasihi ya Kiswahili usemao ya kuwa fasihi ni 'hisi' au ni 'ufunuo' au 'buruhani' kutoka kwa Mungu au miungu.[9] Labda kidogo uyakinifu huu hauwi wa kidayalektiki kiasi cha kutosha, kwani mhariri anaongezea kuwa: "Fasihi yoyote huwa haina budi kulingana na mazingira na wakati inapoandikwa." (uk. 7). Kauli hii ni kweli kwa kiasi fulani tu. Kwa vile fasihi ni zao na kio cha jamii, mahali na wakati maalumu, ni wazi kuwa kwa kawaida italingana na mazingira na wakati inapoandikwa. Bali si sahihi kusema 'haina budi' kuwa hivyo, maana fasihi inaweza pia kuwa mbele ya wakati na mazingira inapoandikwa. Kwa kweli fasihi ambayo ni jamili, pevu na yenye manufaa ya kudumu ni ile ambayo maudhui yake na maono ya mtunzi wake yanakiuka wakati na mazingira finyu ya mwandishi huyo. Ndiyo maana hata leo watu bado wanasoma Utenzi wa Al-Inkishafi, mashairi ya Muyaka, tumthiliya za Shakespeare, Moliere; Biblia; ngano za kale za Wagiriki, n.k. Hata mashairi ya Abdilatif mwenyewe, na maandishi ya Shaaban Robert na Watunzi wengine wa leo huenda yatakuwa yanasomwa na kupendwa na watu hata karne mbili baada ya sasa, kwani maudhui na usanii wayo unakiuka mipaka ya jamii na karne ya leo.

Jambo la tatu ambalo Abdilatif analigusia katika utangulizi wake ni juu ya sanaa yenyewe ya ushairi, hasa kuhusu uhusiano kati ya fani na maudhui. Rai ya mhariri kwa washairi wenzie ni kwamba fani na maudhui ni pande mbili za kitu kimoja na kitu hicho hakikamiliki iwapo mojawapo kati ya hayo linakosekana na au halikuzingatiwa ipasavyo. Na hili ndilo tatizo kubwa la mashairi mengi ya katika diwani ya Mashairi ya Miaka Kumi ya Azimio la Arusha. Maana kwa kuzingatia maudhui tu na kupuuza fani washairi wengi wameuua usanifu wao na kupunguza athari na mvuto wa Mashairi yao. Abdilatif anawapinga wale wadaio kuwa wanaandika mashairi yao kwa lugha 'ya kawaida' au kwa fani 'duni' kwa kuwa ati wanataka 'kuwafikia' watu wengi. Anasema ni kosa 'kuudhania umma kuwa hauna mabongo' ya kuweza kuelewa mashairi mazito. Huko, anasema, ni 'kuudharau umma'.

Suala la kuwa kiwango gani cha fasihi kinasadifu 'umma' ni gumu na si rahisi kulipa jibu linalotosheleza. Jambo la kukumbuka ni kwamba viwango vya welewa vya watu mbalimbali miongoni mwa umma vinapitana.

Watu wote hawawezi kuielewa fasihi kwa kiwango kile-kile. Kadhalika welewa wa msomi aliyejifunza fasihi shuleni kwa miaka kumi ni tofauti na welewa wa mwananchi aliyehitimu elimu ya watu wazima tu. Tunapokuja upande wa fasihi ya Kiswahili, kuna suala la lugha. Kiswahili si lugha ya kwanza ya kila msomaji wa Kiswahili: kwa wengine ni ya kwanza na kwa wengine ni ya pili. Viwango vya welewa vya makundi haya mawili vinatofautiana kutegemea ujuzi wao wa lugha ya Kiswahili. Mathalan mashairi ya Abdilatif ambayo kwa kawaida ni mepesi kueleweka kwa wananchi wa kawaida wa pwani, hayaeleweki kwa wasomaji wengi wa bara, hata wale waliosoma hadi kidato cha nne! Na hawayaelewi kwa sababu lugha ya Kimvita iliyotumika hawaijui, ingawa ni Kiswahili -- Kiswahili chao ni kile cha shuleni 'kilichosanifiwa'. Hivyo kusema kwamba mashairi kadha hayaeleweki kwa watu si 'kuutukana umma' bali ni kueleza tatizo ambalo ni halisi, la kweli na gumu.

Tumeupitia kwa urefu utangulizi wa mhariri wa kitabu hiki, Abdilatif Abdalatif, sababu mawazo yanayosemwa humo ni ya msingi kabisa katika kujadili na kupanga namna ya kuendeleza fasihi yetu ya Kiswahili. Na kama tulivyosema awali, uzito na umuhimu wa kitabu hiki hauko katika mashairi yaliyomo, bali zaidi uko katika utangulizi.

Mhariri anamalizia utangulizi wake kwa kututahadharisha kuwa wakati tunashangilia miaka kumi ya Azimio, inatubidi tuyaone pia matatizo ya Azimio yanayotukabili; anasema:

.... Tucheze huku twapima, vyema tupime, miaka ilosabiki
Tujue tulipokwama, tupatizame, na kuving'oa visiki
Tulipovuka salama, tutie shime, alo na haja hachoki
Hapumui hadiriki
Hadi yalomkingama, ayaegemo, ajitoe kwenye dhiki......

Laiti kama washairi waliotoa mchango wa mashairi katika Mashairi ya Miaka Kumi ya Azimio la Arusha wangalifuata rai hii ya mhariri wao! Bali sivyo ilivyo. Idadi kubwa ya mashairi katika diwani hii yanatukuza na kushangilia tu 'mafanikio ya ujamaa' kana kwamba mambo yote leo ni sawa na ni shwari kabisa. Kwa mfano Sullimar anasema:

Tumekusanyika sote, tunaishi kijamaa
Kazi tunafanya sote, kwa furaha si nazaa
Mwenye hali na kiwete, leo wote wajamaa.....
Hakuna tatizo leo, japo kwanza yalijaa
Twakuza maendeleo, faida izidi zaa
Bila ya mapendeleo, twagawana kijamaa.....
(A.I. Sullimar, uk. 38)

Kutokana na maneno haya, mtu asiyeifahamu Tanzania anaweza kudhani kuwa Tanzania ya leo ni pepo ya ujamaa ambamo hamna tena matabaka, hamna wanyonyaji na wanyonywaji, mali yote twagawana sawa kwa sawa. "Hakuna tatizo leo"!

Nchi isiyokuwa na tatizo haiwezi kuendelea, itatumama; kwani maendeleo ni matokeo ya mashindano ya binadamu dhidi ya 'matatizo.' Kwa bahati mshairi anakiri mwishoni kuwa hajajua kutunga, bado anajifunza:

Ningali nasoma shule, ya utunzi wa sanaa
Kama kuna kosa mle, kwenu anaomba shufaa........

Kama mwandishi angekosea sanaa tu, angesamehewa. Lakini kosa lako ni kubwa zaidi, ni la kiitikadi; na kosa hilo halina msamaha. Mwandishi aseme kweli hata kama inauma!'

Kama washairi wenye ukasuku wangekuwa ni chipukizi tu, hatungekuwa na wasiwasi sana. Bali tunashtuka tuonapo washairi 'mahiri' wa zamani, waliokwisha kujipambanua katika kunga, wakifanya kosa hilo hilo. Ndevumbili anaimba:

Kwa faidaze twadara, viumbe ajimaina
Waliokuwa kachara, sasa tumevimbiana
Si uvimbe wa harara, ni dhiki hakuna tena
Haki limezikomboa, Azimio la Arusha
Watu tunataanasi, tumeodoa utwana.......
Kwa usawa wa maisha, sote twaafikiana

(Y.Ndevumbili, uk. 80)

Watanzania wote 'wanataanasi' --wanaishi kwa anasa na "kwa usawa wa maisha." Hakuna migogoro yoyote, kwani "sote twaafikiana"! Laiti kama mawazo haya ya Ndevumbili yangekuwa kweli, Tanzania ingekuwa pepo; ingekuwa ni nchi ya kwanza duniani kufikia ukomunisti --hatua ya juu kabisa ya ujamaa -- ambapo "dhiki hakuna tena" na wanyonge .. wote (walikuwa kachara) 'wamevimbiana' kwa shibe.

Ni kweli kuwa wapo walioneemeka katika miaka kumi ya Azimio, lakini si wote. Watanzania walio wengi bado wamekabiliwa na ukosefu wa chakula bora, malazi safi, mashule, n.k. Hatua ya kwanza ya kujikomboa ni kuona na kuukubali ukweli huu. Kuukanusha ukweli huu ni kukanusha haja ya kufanya ukombozi wa kuiondoa hali hii mbaya.

Mshairi Mayoka anamuunga mkono sahibu yake Ndevumbili na kusisitiza:

Azimio miyaka kumi, hako aliyefubaa
Nchi imejaa nyemi, Tanzania inang'aa...

Kwa sababu ya 'neema' zote hizo, Mayoka anamalizia:

Naombea utawala, usipatwe na fazaa !

(J.M. Mayoka, uk. 90)

Mtu huombea jambo ambalo limemnufaisha. Hivyo, kwa vile Mayoka kanufaika kutokana na dola iliyopo, ana haki ya kuiombea. Bali ni kosa kuuchukulia ufanisi wake binafsi kuwa ni ufanisi wa wote. Hivyo, ingawa mshairi Mayoka anasema "Ni kioo ujamaa, unajiona mwenyewe" lakini yaelekea yeye mwenyewe amejifanya ndiye 'kioo' na katika yeye anauona ujamaa; ufanisi wake, furaha yake na majonzi yake ndiyo ufanisi, furaha na majonzi ya ujamaa!

Kipimo kimojawapo cha kufaulu kwa Azimio la Arusha katika miaka kumi ya kwanza ya uhai wako ni mwamko wa kisiasa na kitabaka walionfikia wananchi katika muda huo. Vuguvugu la wafanyakazi la mwaka 1971-1973 lililozinduliwa na Mwongozo lilionyesha, kwa kiasi fulani, kuwa wafanyakazi wa Tanzania walikuwa wameanza kujitambua kitabaka na kuyaelewa maslahi ya tabaka lao. Bali si rahisi kupima mwamko wa wafanyakazi na wakulima, hasa wakati hali ya kijamii inapokuwa kijuujuu na vuguvugu limepoa. Wakati kama huo ni vigumu kupambanua kati ya mwanamapinduzi na mpinga mapinduzi. Njia mojawapo ya kukadiria mwamko wa umma ni kuchunguza sanaa zao, hasa nyimbo za fasihi simulizi, ushairi na hadithi.

Inavyoonyesha kutokana na diwani hii (na kwa kuchunguza mashairi mengi yachapishwayo katika magazeti ya Kiswahili) mwamko wa kisiasa wa wasahiri wengi haujaongezeka sana tangu mwaka 1967. Wengi bado wanakariri yale yaliyosemwa na washairi wa enzi hizo.

Mathalani mshairi Ngariba, kama washairi wengi, anaona kuwa fanikio kuu la Azimio ni kwamba limeikata kabisa mirija ya kigeni:

Faida zajulikana, tangu mirija kukata
Fedha haziendi tena, Ulaya kwa kina pita
Zatufaa sisi sana, uchumi tumekamata....

(K.O.N. Shaki (Ngariba) uk. 16)

Kukata mirija ya kigeni, kujinasua kutoka katika makucha ya ubepari wa kimataifa ndilo sharti la kwanza la ujenzi wa uchumi wa kijamaa. Bali kufyeka mirija ya kigeni si rahisi kama kutangaza Azimio. Hata kama baadhi ya vyombo vya kifedha vya kigeni, kwa mfano mabenki na makampuni ya bima, vimekwisha kutaifishwa, bado ziada yetu inanyonywa kwa kupitia njia tofauti, mpya na labda madhubuti zaidi. Kutaifisha mabenki na majumba hakutoshi kuutokomeza ubepari wa kimataifa. 10
Labda mshairi Shaki analitambua jambo hili anaposema:

Tuna vichache viwanda, hapa pwani pia Moshi
Kwa vitu tunavyounda, nchini havitutoshi
Mazao yetu yaenda, huko ng'ambo mafurushi

Ni kweli kuwa 'viwanda havitutoshi' (siyo pwani na Moshi tu, bali nchini kote) na hivyo uchumi wetu umepogoka (haujitegemei wala kujitosheleza kwa viwanda na bidhaa asilia). Iwapo mazao yetu 'yanasombwa kwa mafurushi' kupelekwa ng'ambo, haiwezekani tukawa wakati huo huo 'uchumi tumekamata'. Tatizo la mshairi huyu, kama ilivyo kwa washairi wengi waandikao magazetini, ni lile la kurudia kikasuku yale yasemwayo majukwaani na magazetini bila ya kuyaelewa wala kuyacheua sawa sawa. Mathalani pamoja na kutuonyesha baadhi ya matatizo yetu halisi, mshairi huyu anadiriki kutamka kuwa:

Mafanikio mazuri, Azimio Limeleta
Watu wana hali nzuri, waidhi bila matata
Pamoja na kwa fahari, huduma bora wapata .......

Sasa tushike lipi?

Ukasuku hauchujui maudhui tu, bali unaharibu hata usanifu. Maana kama maudhui hayatoki ndani ya moyo, hayawakilishi hisi za kweli za mshairi, hata fani yake itakuwa chapwa, ya kulazimisha. Ubeti ufuatao unadhihirisha wazi uchapwa tunaouzungumzia:

Haya nilokwisha soma, ndiyo maoni yangu
Nadhani mtayapima, pamoja na ya wenzangu
Mtachukua mema, na myapige mafungu
Azimio la Arusha, latimiza miaka kumi

(<u>K.O.M. Shaki</u>, uk. 17)

Ubeti huu hauna mvuto wowote wa kishairi, ni nathari tu katika umbo la vina na mizani. Na mifano ya 'mashairi' ya aina hii ni mingi ana katika kitabu cha <u>Mashairi ya Miaka Kumi ya Azmio la Arusha</u>. UKUTA haina budi kujiuliza kama kwa kuchapisha tungo za aina hii ihakuza au inaviza ushairi wa Kiswahili.

Mengi yaliyosemwa juu ya shairi la K.O.M. Shaki (Ngariba) yanasadifu pia shairi la Mohamed Sulemani (Mtu-Chake) ambalo ni la pili katika mkusanyo wa UKUTA. Mtu-Chake anaona kuwa Azimio limeleta mema matupu; matatizo yaliyopo ni ya kujitakia tu; yanasababishwa na uvivu, uzembo na utegaji:

Tatizo ni utendaji, mipango kukamilisha
Wengine ni wategaji, mambo huyakorofisha
Kwa hiyo waongozaji, wavivu huwatabisha
Azimio la Arusha, limenufaisha umma

(<u>Mohamed Sulemani</u>, uk. 19)

Aonavyo Mtu-Chake ni kwamba kipingamizi kikubwa cha ujenzi wa ujamaa nchini Tanzania ni watu 'wadogo', watu wa hali ya chini, wanaoongozwa. Hao ndio wazembe na ndio wategaji. Wanataa-bisha 'waongozaji', wakubwa, watawalamsonge, wazalendo. Huku si kutetea mapinduzi bali ni kuyapindua mapinduzi. Ni kushindwa kuielewa na kuieleza nafasi ya umma katika kujenga ujamaa. Iwapo wa hali ya chini ndio wavivu na wafisadi wa mipango ya kijamaa, uchumi wa nchi hii unazalishwa na nani? (Na viongozi?) Yawezekana kuwa baadhi ya wafanyakazi ni wavivu, bali kila lililopo lina kiini chake katika mfumo wenyewe wa jamii: Je, uvivu huo umesababishwa na nini? Kulijibu swali hili kungemlazimisha mshairi kuichambua jamii yake kisayansi badala ya kuieleza kijuujuu tu. Bali uchambuzi na ukasuku havitangamani.

Kwa bahati si washairi wote katika diwani hii wanaafiki kauli isemayo kuwa Azimio limesafisha kila waa na kila tatizo, kizingiti kikubwa kilichosalia ni ufisadi wa watu wa chini. A.I.Sullimar (shairi na. 3); Salim Ali Kibao (na.4) na J.M. Mnyibwe (na. 5) wanatuingiza ndani zaidi kiuchambuzi na kukanusha ile dhana ya kuwa hakuna matabaka katika nchi hii na unyonyaji wa ndani umekwisha. Sullimar anapatia anaposema:

......../12

Walizuka limbukeni, kutuletea ghasia
Wakapita chini chini, kuwashawishi raia
Waacho kutia kani, lengo tulilofikia
Huu ni ukweli wako, Azimio la Arusha

Pendekezo langu hapa, niwape watanzania
Tunoe visu kwa tupa, makali yalozidia
Tuwachinje mapapa, na vizazi vyao pia
Huu ni ukweli wako, Azimio la Arusha

(A.I. Sullimar (Mchunguzi) uk. 21)

'Limbukeni' anaowazungumzia Sullimar ni ndumilakuwili, wanafiki wanaotukuza ujamaa hadharani na kuupinga kichinichini. Ili kupambana na nyang'au wa aina hii, wenye kuwakilisha tabaka la wanyonyaji, itabidi pengine silaha na mabavu vitumike

Tunoe visu kwa tupa.......
Tuwachinjie mapapa .......

Neno 'mapapa' linaonyesha kwamba hawa si 'makabwela' bali ni majitu: ni watu wenye madaraka na wanyonyaji wakubwa. Tunapata picha ya bahari 'tesi' ambamo samaki wakubwa wanawameza samaki wadogo. Hii si bahari shwari, ni bahari yenye harakati. Na bahari hii ni Tanzania, ni Afrika ni ulimwengu mzima. Kukanusha au kuufumbia macho ukweli huu ni kufuata hiari ya moyo dhidi ya kauli ya historia ambayo haipingiki na haiwezi kutanguliwa.

Salim Ali Kibao anaungana na Sullimar ~~kutukanabahisha kuwa~~ mapambano yangali yanaendelea:

Miaka kumi imekwisha, na dunia imeona
Harakati hazijesha, na vijiji vinafana
Tutakapokamilisha, hapo tutatulizana.......

Swali ni je, harakati hizo ni za aina gani na ni dhidi ya nani? Ni za kupinga ubepari wa kimataifa tu au hata ubepari wa ndani? Kuna uhusiano gani kati ya mabepari wa ndani na wale wa kigeni? Kuhusu swali hili Kibao anatetereka na kuturejesha jukwaani. Analiona Azimio kuwa:

Ni kitu kilotingisha, mambo yalofichamana
Pia kuwaunganisha, wale wasiopatana
Fikra kuziamsha, za kuondoa ubwana
Ni faida kubwa sana, kuwa nalo Azimio (uk. 22)

Azimio la kujenga ujamaa haliwezi 'kuwaunganisha wale wasiopatana', kwani kufanya hivyo ni kuleta suluhu ya matabaka wakati nia ya ujamaa ni kuendeleza harakati za matabaka na hatimaye kulikomboa kabisa tabaka la wanyonyaji. Isitoshe, kuungana kwa matabaka ya ndani hakuwezi kuwakasirisha mabepari ya kigeni: 'Hilo likakasirisha, wageni wakanong'ona' bali matokeo yake yangekuwa ni kuwafurahisha wanyonyaji wa kigeni. Kutoungana kwa matabaka ya ndani yenye maslahi tofauti ndiko hasa kungewaghadhibisha mabepari hao, kwani wangekosa kipenyo cha kuingilia uchumi na siasa ya nchi (tabaka la ndani linalowakilisha mabepari wa kigeni lingetengwa, kukandamizwa na kuangamizwa kabisa).

Bali swala hili litaeleweka kwa wale tu wanaokubali kuwa baina ya Waafrika wenyewe kwa wenyewe yako matabaka. Wale wasiokubali hili daima wataishia katika vuguvugu la utaifa tu na kuhubiri 'udugu' wa watu wousi. Na hili ni tatizo la washairi wengi katika diwani zote mbili.

Mnyibwe (Mtu-Kitu) anaelekea kuutambua ukweli huu:

Na ubepari si rangi, nyekundu na kahawia
Wala si kupiga nyangi, wa mbali wakasikia
Ubepari ni misingi, ya haki kudhulumiwa

(J.M. Mnyibwe (Mtu-Kitu) uk. 24)

Ubepari si imani, si maneno wala utaifa, bali ni utaratibu wa jamii ambao unaruhusu dhuluma ya jasho la mfanyakazi au mkulima iwepo. Kutaifisha mabenki na majumba, japo ni hatua muhimu katika kupambana na ubepari, hakutoshi kuutangua ubepari, madhali mfumo wenyewe wa kibepari bado upo. Ujamaa wa domo unapozidi ubepari hujivika pazia la unafiki:

Matatizo yaliyopo, yaliyotuandamia
'Viongozi' kuwa popo, mumbo kujibadilia
Hapa wapo kule wapo, Azimio kukimbia.....

Na ghiliba ilo nzito, Taifa kughilibia
Analo jambo Lushoto, mapesa anabugia
Eti kajenga mtoto, dede hajasimamia ......

(M.Mnyibwe, uk. 25)

Ni hatua ndefu sana kutoka kwa Mtu-Chake, anayelaumu watu wa chini, hadi hapa kwa Mtu-Kitu, anayefichua ubovu wa uongozi, (Hata uchaguzi wa jina la kishairi hutegemea mtazamo wa fikira wa mshairi. Mathalani jambo muhimu katika ujamaa siyo Mtu-Kuwa-na-Chake (Mtu-Chake) bali ni Mtu-Kuwa-na-Kitu (Mtu-Kitu) -- yaani mgawano mzuri wa mali)

Mtu-Kitu anamalizia shairi lake kwa kushauri wasaliti wa ujamaa waadhibiwe:

Wale wanaopuuza, waonwa wana hatia
Majina kuwatangaza, bila ya kuwajutia.......(uk. 26)

Sawa: bali kuwatangaza tu kunatosha? Tangu hapo wanajulikana; siri yao ni siri ya wengi. Labda jibu bora tunalipata kwa Sullimar anayesema; "Tunoe visu kwa tupa."

Mshairi Sihiyana Swalehe Mandevu (Mtenda Mema) hakubaliani na utumiaji wa mabavu. Yeye, labda kwa kuwa anapenda 'mema' anaona njia bora ya kutatua matatizo yetu ni elimu: "Msichoke na mafunzo, watu kuwaelimisha" (uk. 53). Katika shairi lake jingine (Na. 23) mshairi huyo huyo asema njia ya kutatua matatizo yetu ni kuongeza 'makada' wa Chama, kuongeza jitihadi katika kazi ("Silaha ni jitihadi, kila kitu tutashika" (uk. 64) na kusali:

Ndugu tumuombe Mungu, sasa hivi tutacheka
Kwa rehemaze Rabuka, litukuza Azimio (uk. 65)

Ni vigumu kupendekeza ufumbuzi sahihi wa matatizo ya kijamii kama kiini cha matatizo hayo hukijui. Ndiyo maana kila mshairi katika diwani hii anapendekeza ufumbuzi wake binafsi. Wale ambao ni wdhahifu zaidi wanadiriki kusema kuwa Azimio limekwisha kusawazisha matatizo yote. O.A. Kasumba (Mroa) anasema:

Azimio ndiyo dawa, dawa ya penisilini
Unyonyaji lagenguwa, na ukupe lalaani (uk. 56)

Azimio ni penisilini inayotibu maradhi yote ya kijamii. Sasa maradhi yamepona, hivyo wajibu wetu ni kufanya kazi kwa bidii, tule tushibe, afya zetu zirejee. Anaongezea Kibao:

Yatupasa kuzidisha, bidii kila namna
Uvivu kujiepusha, na pia kutegeana
Kuchezewa kutakwisha, mtu hawezi tukana ..........
(Salim Ali Kibao, uk. 23).

Hii ingekuwa kuweli kama tatizo letu, ambalo ni ubepari, lingekuwa limesababishwa na uvivu wetu. Mpaka sasa haijathibitika kama nchi zilizoendelea zinafanya kazi kwa juhudi zaidi kuliko nchi zinazoendelea.

Ikiwa sala, juhudi ya kazi na mahada hawawezi kutatua matatizo yetu leo, vivyo hivyo taasisi ya sheria haiwezi kuibadilisha jamii. J.J. Komba, mshairi wa zamani na katibu mkuu wa UKUTA, anafikiri ufumbuzi wa matatizo ya utekelezaji yanayotukabili hivi leo ni kuweka sheria kali:

Ni juu ya serikali, na Chama kuthibitisha
Kuweka sheria kali, bungeni kuipitisha
kukomesha mbaya hali

Hali yao nayo mali, wanaotufedhehesha
Tuwatupilie mbali, shimoni kuwaangusha
Azimio la Arusha, hapa lilipofikia
(J.J. Komba, uk. 72)

Ingawa Komba anatuzindua kwa fani tofauti kidogo na ile ya wenzake (maana umbo moja tu la tarbia linachosha likitumika kwa muda mrefu) [11] lakini kwa fikra hatuzindui; anachokifanya, chambilecho Yesu Kristo, ni kumimina tu tembo kongwe katika vibuyu vipya. Maana sheria, kama taasisi nyinginezo, hubuniwa na tabaka linalotawala ili kuhalalisha na kulinda mfumo wa jamii na mahusiano ya kijamii yaliyopo. Sheria hazibadilishi mfumo. Mathalani sheria hazimpi chakula mwizi fukara bali humzuia asibomoe ghala la tajiri.

Kwa washairi wengi, katika diwani zote mbili, ufumbuzi kamili wa matatizo yetu, njia pekee ya kuondoa umaskini, ni kilimo. Kandoro anatuambia:

Na lingine tazamio kilimo kustawisha
Hayo ndiyo mapimio, kuzuwia mshawasha
Njaa na vingi vilio, vyote tutaporomosha
Uvivu tunaushosha, utukome marudio (uk. 87).

................/4

Washairi wengi, labda baada ya kusoma kijitabu cha Ujamaa Vijijini, wanakubaliana na kauli hiyo. Wanapendekeza wakazi wa mijini 'wasio na kazi' wahamie vijijini kulima. Si vibaya kulima, bali kuna maswali ya msingi ambayo ni vibaya kuyakwepa wakati tunawashauri watu kurudi vijijini. Baadhi ya maswali hayo ni haya: Je, ujamaa utajengwa vijijini tu na miji itaachwa nje kabisa ya mkondo wa mapinduzi? Kwa nini mpaka sasa bado wapo watu 'wasio na kazi'? Kwa nini watu hao hawapewi kazi huko huko mijini? Uchumi wa kijamaa uliopangwa vizuri hauwezi kukosa kazi, labda kupungukiwa na wafanyakazi. Je, Tanzania itajikomboa kwa kutegemea kilimo tu na kutojali kabisa kuanzisha viwanda vikubwa? Na swali la mwisho: Kwa nini vijana wengi wanakimbilia mijini?

Mshairi yoyote ambaye hajajibu maswali haya hawezi kupendekeza ufumbuzi wa kufaa wa tatizo la uzururaji. Uchambuzi wa kijuu juu wa matatizo si kosa la washairi tu, bali ni kosa la wapiga nadharia wengi katika nchi yetu - waandishi wa vitabu, wanasanaa, wanasiasa, n.k., Katika riwaya, tatizo hili limetia fora na kuifanya riwaya ya Kiswahili iwe chapwa na kuzidi kutopea katika udhanifu. Lipo tapo zima la waandishi wa riwaya ambalo linahubiri 'kurejea vijijini' kuwa ndio ufumbuzi wa matatizo ya mnyonge wa mjini.[12] Chanzo cha udhanifu wa tapo hili ni itikadi ya kikulima ambayo bado imeshika sana kutokana na maendeleo haba ya nguvu za kuzalisha mali yanayoitilia rutuba imani potofu kuwa kilimo ndicho 'uti wa mgongo' na kitaendelea kuwa 'uti wa mgongo' wa uchumi wetu. Udhanifu huu hautakwisha mpaka hali ya uchumi inayourutubisha itakapoondolewa.

Diwani zote mbili zina upungufu mkubwa wa kiuchambuzi, lakini Mashairi ya Miaka Kumi ya Azimio la Arusha kina upungufu mkubwa zaidi. Msisimko mkubwa wa harakati, uchungu na imani ya ushindi tunayoiona katika Mashairi ya Azimio la Arusha hatuioni tena katika Mashairi ya Miaka Kumi ya Azimio la Arusha. Ushairi huu wa sasa umevia, umepoa, ni gofu na kivuli tu cha ushairi wa miaka ya 1967 - 71. Hili ni jambo la kusikitisha, lakini linaeleweka.

Mhariri, Abdilatif Abdalla, ameuona upungufu huu, na anafikiri kuwa kiini chake ni unafiki na ukasuku. Anatuambia katika utangulizi:

> .....Haimfalii mshairi kutunga tungo ambazo hazina kazi nyingine zifanyazo ila kuwa ni kipaza sauti tu cha yatendekayo au yasemwayo nchini mwake, au kusifu tu na kuitikia kwa kila lisemwalo na lifanyikalo.
> .....Nchi haijengeki kwa unafiki bali huangamia kwa unafiki.
> (uk. 6)

.........15

Mashairi mengi katika diwani hii ni ya aina hiyo ya 'kusifu' na 'kuitikia' tu kila lisemwalo majukwaani. Na kwa vile hayana udhati mkubwa, hayafungamani na hisia halisi za waandishi, mashairi mengi yako chapwa kisanaa.

Ndiyo kusema basi diwani hii haina manufaa yoyote? Hata kidogo. Diwani hii ina manufaa kadha. Kwanza inatuonyesha kuwa washairi wetu bado wako nyuma kimwamko; kwamba bado tunayo safari ndefu hadi kufikia ile hatua ya kuwa na sanaa halisi ya umma.

Ni muhimu kujikumbusha kuwa washairi wengi wa Kiswahili ni watu wa kawaida-- yaani si wasomi, si mabepari au matajiri. Wengi wa wafanyakazi na wakulima halisi. Mtazamo wao wa maisha, fikira zao, na matamanio yao yamefungamana na mazingira yao ya maisham na yamewekewa mpaka na mazingira hayo. Mawazo yoyote mapya wayapatayo washairi hao hayatokani na kusoma vitabu vingi vya kigeni au kusafiri ugenini na kujifunza na kuona mambo mapya. Sanaa yao, lugha yao na hasa mawazo yao yanatokana na mapokezi ya utamaduni, mila na fikira waliyorithishwa na wahenga wao, na vile vile uzoefu wao wa maisha ya kila siku; yanatokana na harakati zao za kujikimu katika ulimwengu wenye uhasama, ubahili na ubaguzi dhidi ya wanyonge. Hivyo washairi hao kuwa wepesi kupokea wazo lolote jipya lenye welekeo wa kutetea wanyonge au lenye kuwaahidi maisha bora ya mbeleni, hata kama ahadi hizo hazitekelezeki au zingechukua muda mrefu sana kutekelezwa. Hivyo ahadi za dini, za pepo baada ya kufa aghalabu huwajadhubisha washairi wetu na kuwasukuma kutunga mashairi ya kiwango cha juu sana kisanaa.

Hawa ndio washairi tunaoshughulika nao katika tahakiki zetu; ndio tunaowasikia redioni na kuwasoma magazetini. Hali zao za maisha zinawafanya wayafahamu vizuri sana matatizo ya mtu wa kawaida. Kwa sababu hii, washairi hawa, kwa kukusudia au bila ya kukusudia, kujikuta wakiandika mambo yenye kutetea tabaka lao, tabaka la wakulima na wafanyakazi; hujikuta wanalitetea, wanalisemea, wanalipigania tabaka hilo. Ndiyo maana Abdilatif Abdalla anasema: "Si jambo geni, wala si kitushi, kwa mshairi wa Kiswahili kuitumia sanaa yake hii kwa ajili ya jamii au nchi yake." (utangulizi, uk. 2).

.......16

Kwa mwandishi, kuishi na kuzoea mazingira ya kikulima na kifanyakazi kuna uzuri na hatari zake pia. Uzuri ni ule tuliokwisha kuueleza-kwamba mshairi anayetokana na umma na anayeishi miongoni mwao, siyo kifikira tu, bali kihali, kimwili, kiuchumi, anaweza akayaeleza matatizo yao kwa dhati na uhakika kamili. Anaweza kuwa mwakilishi wao kisanaa.

Hatari iliyopo ni kwamba mipaka ya mazingira yake hayo ya kiuchumi, kielimu na kifikira huweza kumzuia mshairi huyo asipate mawazo mapya na mapana zaidi, kumfanya mtazamo wake na kumfanya awe kikaragosi tu cha kueneza mawazo na fikira za watawala wake bila ya kukusudia (na pengine kwa kukusudia, kwa kujipendekeza, ili apate riziki yake). Washairi wa aina hiyo, ambao leo twawaita 'wasaliti' walikuwepo enzi za ukoloni na mpaka leo bado wapo. Ndiyo maana ni muhimu kupambanua kati ya mtazamo wa fikira wa mwandishi na tabaka lake au nafasi yake katika jamii. Siyo kila mkulima aandikaye huandika fikira za tabaka lake, na siyo kila msomi au bwanyenye aandikaye huandika fikira za mabwanyenye.

Hata hivyo mara nyingi, hasa wakati wa harakati kali za kitabaka, washairi na waandishi wengi wa tabaka la chini hutoa mawazo ambayo kwa kiasi kikubwa yanaweza kusemwa kuwa ni ya tabaka lao. Itokeapo mawazo ya tabaka hilo la wangone yakagongana na itikadi inayotawala, basi waandishi wa tabaka hili hujikuta vizimbani, magerezani au vitanzini. Iwapo siasa inayotawala huelekeaelekea kutetea maslahi ya wangonge, basi fasihi ya kimapinduzi huchanua na fasihi huwa ni nyenzo mojawapo ya mapinduzi hayo.

Kwa kiasi kikubwa washairi wa Tanzania walijumuika kwa hiari katika harakati za TANU za kudai uhuru kwenye miaka ya 1950, kwani waliziona ya kuwa zilikuwa zikiyatetea maslahi yao ya kitaifa. Hali kadhalika, Azimio la Arusha lilipotangazwa mwaka 1967, lugha na mawazo yake yalikuwa mvuto mkubwa kwa mwananchi wa kawaida, ambaye alikuwa:

> Amenyonywa kiasi cha kutosha
> Amenyanyaswa kiasi cha kutosha na
> Amepuuzwa kiasi cha kutosha......

Nyundo ya Azimio, angalau kwa kauli kama si kwa vitendo, haikuelekezwa kwa mtu wa kawaida; ilielekezwa kwa bepari, kabaila, mirija ya kimataifa katika mabenki, makampuni ya bima, viwanda, n.k. Mshairi wa kawaida hakuwa na kitu cha kupoteza kutokana na pigo hilo, hivyo umma wa Watanzania uliliunga mkono Azimio hilo, na umma wa washairi hali kadhalika.

Bali diwani hii inadhihirisha jambo moja, nalo ni kuwa baadhi ya washairi waliounga mkono ujamaa hawakuuelewa sawa sawa. Wajibu wa washairi wetu hivi leo ni kujielimisha ili wakifahamu vizuri kila wanachokisifia na kukitetea kwa kalamu na sauti zao.

......./17

TANBIHI & MAREJEO . . .

1. Abdilatif Abdalla, Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa, Oxford University Press, Nairobi 1971.

2. Abdilatif Abdalla, Sauti ya Dhiki, Oxford University Press, Nairobi 1973.

3. Maandishi mengine ya Abdilatif Abdalla, hasa yahusuyo nadharia ya fasihi, hayajachapishwa katika kitabu kimoja, bali yametawanyika katika majarida na vitabu mbali mbali vya Kiswahili. Taz. madhalan makala yake ya "Wajibu wa Mshairi wa Kiswahili Katika Jamii Yake" (Uhuru tarehe 1 na 2 Novemba, 1976); "Utangulizi" wake katika Diwani ya Ustadh Nyeamaume Shungwaya Publishers, Nairobi, 1976; na utangulizi katika kitabu cha T.S.Y. Sengo, Shaaban Robert: Uhakiki wa Maandishi Yake, Longman, DSM, 1975.

4. G. Kamenju na F. Topan (wahariri) Mashairi ya Azimio la Arusha, Longman, Dar es Salaam, 1971.

5. Serikali ya TANU ilitarajia kwamba ingeweza kutekeleza mipango yake ya maendeleo kwa kutegemea misaada na mikopo na mitaji kutoka nchi za kigeni. Kutokupatikana kwa misaada na mitaji hiyo kulisababisha mpango wa Kwanza wa miaka mitano kutofaulu na hali ya uchumi kuzorota zaidi. Palikuwa na mvutano kati ya viongozi wa Serikali na Chama walioutumia uongozi wao kujilimbikizia mali na ambao haukufaidika sana kiuchumi kutokana na kujitawala. Wanafunzi wa Chuo Kikuu, mwaka 1966, waliandamana kupinga sheria iliyowataka wajiunge na jeshi la kujenga taifa baada ya masomo yao, wakidai kuwa viongozi wanawalazimisha vijana tu kujitoa mhanga kwa ajili ya taifa wakati viongozi wenyewe wanazidi kujinufaisha. Migomo ya wafanyakazi ilikuwa ikitokea mara kwa mara ingawa si sana kama wakati wa ukoloni, na bei za mazao mengi ya Tanganyika, hasa katani, zilikuwa zikishuka kila mwaka. Mambo yote haya, pamoja na kupevuka kwa harakati za ukombozi kusini mwa Afrika kulikoiwajibisha serikali ya Tanzania kuunga mkono mapambano ya silaha, pamoja na kushindwa kwa vibwanyenye wa ndani kustawisha ubepari wa kitaifa kwa njia ya 'mashindano huru' ni miongoni mwa sababu zilizoisukuma TANU kutangaza Azimio la Arusha.

6. Mpaka sasa hakuna tafsiri ya Kiswahili ya mashairi ya Vladimir Mayakovsky. Bali upo mkusanyo wa baadhi ya mashairi yake kwa Kiingereza katika kitabu kiitwacho Poems (Pregress Publishers, Moscow, 1972). Mashairi yake mengine yamo katika kitabu cha The Penguin Book of Socialist Verse (Mha. Alan Bold) London: Penguin Books, 1970) uk. 179-202.

.........

7. Nyerere, J.K. Freedom and Unity, Oxford University Press, Dar es Salaam 1966, uk. 209.

8. Mtazamo huu unapingana na mtazamo wa kinafsi wa kibwanyeye uidhaniao fasihi na fikira kwa jumla kuwa ni mambo yaliyo juu ya muundo wa jamii na mahusiano ya watu katika jamii, na kuwa dhana ndiyo huzua vitu yakini na kuumba ulimwengu badala ya ulimwengu na vitu yakini kuzua dhana.

9. Rai ya kuwa fasihi hutokana na ufumuo au 'buruhani' ya miungu ni muflisi kwani inatafuta kiini cha mambo na matendo ya watu nje ya dunia na ulimwengu. Fikira hii ya kidhanifu ni ya kale sana na ilitumiwa na waandishi wengi wa vitabu vya dini kuhalalishia mahubiri yao.

10. Utaifishaji ambao haubadilishi mahusiano ya watu katika uzalishaji mali hauleti ujamaa bali wakati mwingine hutumika kuimatisha ubepari unaotetereka. Mathalan baadhi ya mashirika ya ndege huko Uingereza yalitaifishwa baada ya wenye mashirika hayo kukaribia kufilisika. Utaifishaji wa kijamaa ni ule tu unaofanywa na dola ya kifanyakazi.

11. Fani ya Komba ni ya ushairi wa msisitizo aliouanzisha Marehemu Mathias Mnyampala. Mtindo wa aina moja tu unachosha, na kubadilisha mtindo ni alama ya usanifu bora usiokuwa uigaji tu. Isitoshe, fani aghalabu hutawaliwa na maudhui. Hata hivyo, tunapoamua kutumia mtindo fulani hatuna budi kuhakikisha kuwa tumezifahamu vizuri kunga za fani hiyo. Mathalani, ingawa Komba amejaribu kutumia fani ya msisitizo katika utunzi wake, lakini hakufaulu. Msisitizo wa Mnyampala una mistari sita kwa kila ubeti. Kila mstari una mizani kumi na sita isipokuwa mstari wa tatu ambao una mizani nane tu. Neno la mwisho la mstari wa tatu linarudiwa mwanzoni mwa mstari wa nne ili kusisitiza wazo muhimu katika ubeti huo. Kadhalika neno la mwisho katika nusu-kipande cha kwanza cha kila mstari wa tano huandikwa kwa msisitizo. (Taz. ubeti huu wa kwanza wa shairi la Mnyampala, "Natunga Msisitizo", ambalo alilitunga kuifafanua fani yake 'mpya'. Maneno yaliyosisitizwa yameandikwa kwa herufi za mlalo):

Nawapangia maneno, ya sifa na welekezo,
Na kuzitoa mifano, zinase nyoyo mawazo,
Usemi wa sisitizo;
Sisitizo mlingano, naioleta mivizo,
Maagizo yawe manono, nayatilia mkazo,
Natunga msisitizo, tungo zenye mwendo mpya.

(M.Mnyampala, Diwani ya Mnyampala, EALB, Nairobi, 1972, uk. 121.

12. Baadhi ya waandishi ambao kwa kiasi fulani wanaingia katika tapo hili linalohubiri "kurejea shambani" hi Shaban Robert, Utubora Mkulima; Nelson, Dar es Salaam, 196; Kezilahabi, E. (Dunia Uwanja wa Fujo EALB, Nairobi; 1974). Katika riwaya hii wazo la kurejea shamba linazingatiwa ndani ya wazo kubwa zaidi linalomtaka myonge apige moyo konde na kuvumilia dhiki zinazo-sababishwa na nafasi yake katika mahusiano ya jamii. Wahusika wawili; Moyokonde na Vumilia, wanatumiwa na mwandishi kuwa kielelezo cha wazo hili; N. Balisidya, (Shida Foundation Books ltd Nairobi 1975) na P. Muhando (Hatia EAPH, Nairobi, 1972).

## UNYONYAJI WA WAFANYAKAZI CHINI YA UBEBERU

### KISA CHA WAFANYAKAZI WA BANDARI

Kwa mfanyakazi wa muda mrefu katika bandari ya Dar es Salaam, jitihada za kutafuta suluhisho la matatizo yanayo-mkabili kutokana na ukandamizwaji na unyonywaji siyo kitu kigeni.

Mapambano ya wafanyakazi kaipinga mabepari wanaowaajiri ni ya muda mrefu. Misingi ya ufanyaji kazi iliyowekwa katika kipindi cha ukoloni ndiyo hasa inayotambulisha namna mapambano haya yalivyoendelea na sura yalizo-chukua. Katika hali ya utekelezaji wa kazi shughuli za bandari zime-gawanyika katika vijisehemu vingi. Kwa ajili ya kurahisisha ufafanuzi wa swala hili, tutaangalia wafanyakazi katika mafungu matatu ambapo karibu kila mfanyakazi anaingia na mwamko wao katika kupigania haki zao. Sehemu ya kwanza itakuwa ni ile ya wafanyakazi walioajiriwa moja kwa moja; sehemu ya pili ni ile ya vibarua walioandikishwa na kulipwa kwa mwezi na tatu ni wafanyakazi wanaoripoti kazini kama vibarua na ambao kulipwa kwao kunaweza kukawa kwa wiki au hata kwa siku. Katika sehemu ya kwanza ni lazima tupambanue kuwa warasimu mbali mbali waliopo katika utawala hawakujumlishwa kwani swala lao ni tofauti na tutalijadili baadaye.

Tukianza na historia fupi ya bandari hii, ni dhahiri kwamba umuhimu wake haukutokana na maendeleo ya viwanda hapa nchini. Ukuaji na upanu-kaji wa kiwanda hiki hasa ni matokeo ya utawala wa kikoloni uliokuwa na malengo muhimu yafuatayo : Kwanza ni kujipatia malishafi kwa ajili ya viwanda vilivyokuwepo huko ulaya, zaidi ikiwa ni viwanda vya mabepari wa Kiingereza. Hivyo bandari ilikuwa ni muhimu kama kipito cha bidhaa hizo za awali. Kama ilivyokuwa katika makoloni mengine, nchi yetu ili-kuwa ni soko ambapo bidhaa mbali mbali zilizotolewa na viwanda huko Ulaya ziliuzwa. Kwa hiyo, bandari ilikabiliwa na jukumu la kupokea, kuhifadhi na kutoa bidhaa hizo ambazo zilisambaa kote nchini. Na tatu ni kwamba, kutokana na shughuli tulizotaja ni wazi kuwa makoloni yalikuwa ni uwanja ambapo mitaji ya mabepari ilizalishwa.

Kwa hiyo basi, katika uchumi wa kikoloni, Bandari na njia za usafirishaji kama Reli na Barabara zilikuwa muhimu sana na zilitengenezwa kwa madhumuni maalum.

Dar es Salaam ilianza kukua kama bandari wakati wa utawala wa kikoloni wa Kijerumani. Utaratibu wa forodha ulianzishwa na shughuli za upokeaji, utunzaji mizigo na usafirishaji zilianza kufanyika.

Kitu muhimu cha kuzingatia katika swala hili ni sehemu ambayo bandari inachukua katika mambo ya uchumi tangu wakati huo hadi leo. Misingi ya uchumi iliyowekwa na wakoloni ni ile ambayo iliwawezesha wao kujinufaisha kutokana na makoloni kwa kadri iliyowezekana. Misingi hii ndiyo inayo-

fanya nchi zilizo makoloni na makoloni-mamboleo kuwa ni uchumi unaoangalia nje. Yaani uchumi usiowiana kindani. Katika nchi yetu bandari ni sehemu ambayo iliunganisha njia zote za usafiri na kuweza kutoa utajiri mkubwa nchini. Bidhaa kama katani, kahawa, pamba na madini zilisafirishwa hadi pwani ambapo zilipakiwa katika meli na kusafirishwa.

Kwa hiyo shughuli za bandari zilihitaji wafanyakazi na kadiri bandari ilivyo-zidi kupanuka ndiyo kadiri idadi ya wafanyakazi ilivyozidi. Shughuli za uendeshaji bandari zilianza na makampuni ya kibepari hadi Shirika la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki lilipoundwa. Misingi ya ufanyaji kazi ilibakia ile-ile iliyoundwa na mabepari iliyowafawa wafanyakazi katika vijisehemu vidogo vidogo na kuhakikisha kuwa Usalama wao kazini ni kidogo iwezekanavyo.

Uonevu na dhuluma walizokuwa wakitendewa ziliwafanya watafute njia mbalimbali za kupigania haki zao. Mnamo mwaka 1943 wafanyakazi kwa mara ya kwanza waliweza kusimama imara na kupinga nguvu za utawala wa kikoloni. Mgomo huu utasababishwa na mazingara ya kazi yaliyokuwa magumu kustahimili. Masaa ya kazi yalikuwa mengi na hali za kazi kwa afya ya wafanyakazi hazikuwa zina-tiliwa maonani. Ujira mabao wafanyakazi walipata haikuweza kutosheleza mahitaji yao muhimu na familia zao. Gavana aliamuru mara moja hatua kali zichukuliwe na wafanyakazi warudi kazini. Hii haikuwatisha wafanyakazi na walirejia kazini baada ya kuahidiwa kupata baadhi ya mahitaji yao. Mapambano haya hayakuwihia hapa tu. Katika miaka iliyofuata migomo ya wafanyakazi ilikuwa katika hali ya juu zaidi. Mnamo mwaka 1947 palitokea mgomo ulivenea katika sehemu nyingi zinazo husiana na bandari.

Hali hii baadaye iliwezesha kuundwa kwa chama cha TFL (Tanganyika Federation of Labour) kilichoanza kutetea maslahi ya wafanyakazi katika misingi ya kibwenyenye. Chama hiki kiliendelea kutetea na kueleza malalamiko ya wafanya-kazi nchini hadi mwaka 1962 kilipopingwa marufuku. Tangu chama hiki kilipo-pigwa marufuku wafanyakazi wa bandari ambao awali waliweza kugoma wakati wakidai haki zao. Sasa walijikuta kuwa kisheria kugoma ilikuwa ni makosa.

Kitendo cha mfanyakazi kugoma kufanyakazi kwa kweli haina maana kuwa anafurahia kitendo hicho. Hii huwa ni matokeo ya hali inayokuwepo mahala pa kazi. Kabla ya uhuru migomo ya wafanyakazi kisiasa ilisaidia sana katika kuondoa utawala wa kikoloni. Kwa vile kupata uhuru wa bendera haikuwa hatimaye ukombozi, swala la wafanyakazi ilibidi litafutiwe vikwazo.

Uendeshaji wa bandari hii umekuwa chini ya shirika la jumuiya ya Afrika mashariki hadi kuchangukana kwa shirika hili na sehemu ya shirika hilo upande wa Tanzania kutwaa utawala kamili. Bandari imeendelea kuwa ni moja-wapo ya sehemu zilizokuwa zinapanuka baada ya uhuru. Mategemeo ya kunufaika kwa wafanyakazi yamekuwa ni ndoto tu ambayo inazidi kuonyesha mtengano wa kihasama kati ya wafanyakazi na wale wanaochukua ziada inayopatikana. Ingawa mwaka hadi mwaka bandari inazidi kupata faida hali za wafanyakazi huzidi kuwa duni na maisha kuwa magumu zaidi.

Kuishi kwenye vibanda vilivyochakaa pembezoni mwa jiji la Dar es Salaam na kula kwenye magenge ni hali ambayo ni kielelezo cha mfanyakazi. Hali za kudai haki zinazidi kuwa ngumu siku hata siku na maisha ya mfanyakazi kuzidi kudidimia. Hebu sasa tuangalie jinsi ambavyo bandari hii imeweza kupanuka haraka na kuwa mojawapo ya bandari kubwa katika Afrika.

Mnamo mwaka 1965 Mlowezi Ian Smith huko Zimbabwe alijitangazia Uhuru kwa kujitenga na utawala wa Kiingereza. Utawala wa Smith umekuwa ni matatizo makubwa sana kiuchumi kwa nchi ya Zambia ambayo imezungukwa na nchi kavu. Kutokana na kwamba Msumbiji na Angola zilikuwa bado chini ya utawala wa wareno Zambia ililazimika kutafuta njia ambayo ingeiwezesha kusafirisha bidhaa zake. Njia pekee iliyokuwepo na yenye usalama ilikuwa ni kupitia Tanzania. Hivyo utandikaji reli toka Dar es Salaam hadi Kapiri Mposhi ilikuwa ni jambo muhimu. Mnamo Mwaka 1968 uwekaji bomba la mafuta toka Dar es Salaam hadi Ndola ulimalizika. Utengenezaji wa barabara vilevile ulianza na kufuatiwa na utandikaji wa Reli. Shughuli hizi zilifanya bandari kujikuta inafanya kazi nyingi na nzito mwaka hadi mwaka. Hii inadhihirishwa na uongezekaji wa bidhaa za Zambia. Yaani zilizoenda na kutoka Zambia. Kwa mfano, Tani za shaba iliyosafirishwa kupita bandari hii ziliongezeka kama ifuatavyo:

1965 - 30,000 Tani
1969 - 235,000 Tani

Na idadi ya bidhaa zilizopokelewa ziliongezeka toka tani 733,000 hadi tani 1,059,000.

Licha ya bidhaa za humuhumu nchini ambazo vilevile zimekuwa zikiongezeka, bandari hii hushughulikia bidhaa za Zaire, Burundi and Rwanda. Kipindi toka mwaka 1965 hadi 1974 ni kipindi ambapo wafanyakazi hukikumbuka kwa msingamano wa shughuli walizofanya na maisha ya wafanyakazi yaliyopotea au kulemaa kutokana na uhaba wa zana muhimu za kufanyia kazi. Ongezeko hili la kazi haliambatani na ongezeko la ujira waliopata.

Pengine swala muhimu sasa kuangalia ni nani anayenufaika na kazi hizi ngumu ambazo mfanyakazi hufanya. Kwa kweli, swala la wafanyakazi wa bandari huliwezi kutenganishwa na mapambano ya wafanyakazi wengine katika viwanda mbalimbali. Kama ilivyosehemu nyingine, mfanyakazi wa bandari hukabiliwa na ukosefu wa chombo ambacho anaweza akatumia kupigania haki zake. Kila chombo kilichopo kwake ni kitu kigeni ambacho kinajionyesha wazi kuwa hakiko pale kwa niaba yake. Zaidi ya hapo uandikishaji wa idadi kubwa kama vibarua huwaina lengo la kuwetenganisha na kujenga hali zinazoruhusu unyonyaji na ukandamizaji. Kwa kibarua kazi ni masaa ya kazi anayofanya na siku anazohudhuria kazini. Endapo kutokana na matatizo ya ugonjwa au matatizo mengine ya kifamilia akishindwa kufika kazini basi siku hiyo haihesabiwi. Hii haina maana kuwa wafanyakazi walioajiriwa chini ya sheria za kudumu wanapata ujira unaolingana na kazi wanazofanya.

Hali za ukandamizwaji na unyonyashwaji wa wafanyakazi hujionyesha tangu nyumbani hadi katika sehemu za kazi. Idadi kubwa ya wafanyakazi huishi pembeni mwa jiji la Dar es Salaam kwenye vibanda vya madebe, miti, makuti na vilivyotengenezwa kutokana na mwili ya magari mabovu. Kwa wale waliobahatika huweza kupangisha chumba kimoja kwa familia nzima. Hali za afya katika sehemu hizi ni chini sana na maradhi ya kila aina yanaweza kuifika familia ya kifanyakazi. Mirundikano ya takataka, mabaki ya mifupa, mizoga ya panya, mbwa, ndege na paka, mifereji ya maji machafu yanayojipenyeza toka nyumba hadi nyumba, mabwawa ya maji machafu yaliyosimama na visima vilivyomo mabarabarani mahali ambapo mabomba ya maji yamepasuka ni picha ya sehemu zote waishipo wafanyakazi. Familia za kifanyakazi kwa nadra sana huweza kupata chakula cha kutosha na chenye thamani ya kuweka mwili katika hali ya afya. Kando ya yote haya wafanyakazi huishi, kwa maisha ya upweke na lindi la ufukara. Siyo kwa vile hawafanyi kazi bali kwa vile wafanyakazi zaidi.

Licha tu ya kuwa mfanyakazi hunyanyaswa na nguvu za mtaji mabwenyenye humsakama waziwazi kwa kila atendacho katika hali ya fedhaeha isiyoelezeka. Kuwahi kazini ni jambo ambalo sheria za kibwenyenye husisitiza. Kuchelewa dakika kadhaa kwa mfanyakazi huwa na maana ya kupoteza sehemu fulani ya ujira wake ingawa amehudhuria kazini na sababu maalum. Kwa mfanyakazi wa bandari asipopunguziwa ujira basi hupangiwa kazi ngumu zaidi kama adhabu. Kubeloa shaba, kupakua mizigo ya hatari kama ya madawa ambayo mengine huwa yamepasuka bila kinga n.k. Kwa hiyo kwa mfanyakazi kuamka saa kumi na saa kumi na moja usiku ni kitu cha kawaida usafiri huwa ni shida na ifikapo saa moja king'ora hupigwa na wafanyakazi hugawiwa sehemu za kazi chini ya maserange. Kazi hizi zinazofanywa kwa pamoja huwezesha bandari kupata faida na limbikizo kubwa.

Ujira anaopata mfanyakazi ni kima cha chini yaani Shs. 466.00. Fedha hizi kwa mtu mwenye familia hapa mjini ni sawa na hakuna. Kwa kweli hata akizitumia kununulia chakula tu hakitatosheleza mahitaji hayo. Kwa hiyo kufanya kazi zaidi ya masaa ya kazi (overtime) ni kitu kisichoepukika. Hii ndiyo njia pekee ambayo husalia kwa kumwezesha mfanyakazi ajipatie ingalai mahitaji ya lazima. Baada ya kufanya kazi zaidi ya masaa kumi na mbili mfanyakazi huweza kujipatia kiasi cha Shilingi 600.00 hadi Shs. 800.00 Endapo mfanyakazi huyu hataendelea kufanya kazi palepale basi huenda kujitafutia kibarua katika sehemu nyingine baada ya kazi. Kwa hiyo siyo ajabu kukuta kuwa shughuli zinazoendeka katika makampuni mbalimbali ya ujenzi na utengenezaji mabarabara baada ya saa tisa mchana hufanywa na wafanyakazi wa mashirika au makampuni mengine waliotoka shifti ya kwanza. Hayo ndiyo maisha ya kazi na ujira kwa mfanyakazi hivi leo chini ya ubeberu.

Kwa upande mwingine ni wazi kuwa kuna wale wanaonufaika na hali hii ya unyonyaji damu ya mfanyakazi. Utaifishaji njia za uzalishaji mali haikuwa hatimaye ujengaji wa uchumi unaowiona kindani na kujitegemea. Hali hii

imewezesha mabwenyenye wa kirasimu kwa kutumia nguvu za dola kujipatia msingi wa kiuchumi na kuwa na uwezo zaidi juu ya ziada inayozalishwa na wafanyakazi. Kwa kushirikiana na makampuni makubwa ya ulimwengu na vyombo vya mabeberu kama Bnki ya Ulimwengu, Mabwenyenye wa Kirasimu wamezidi kuweka uchumi wa nchi chini ya mwavuli wa ubeberu badala ya kujitoa katika mfumo huo.

Kwa hivyo hatuwezi kueleza kwa namna nyingine yoyote juu ya suluhisho la utesekaji wa tabaka la wafanyakazi kama siyo kwa Harakati za kitabaka ambazo zinaweza kuleta ufumbuzi wa kimsingi. Tabaka la wafanyakazi siyo tabaka la watu wanaokandamizwa na kunyanyaswa tu, bali vilevile ni tabaka lenye nguvu uwezo na hamasa kuu katika kubadilisha hali yake na jumuiya nzima. Ni kutokana na jinsi ambavyo tabaka hili litafanya ushirikiano na matabaka mengine yanayoumia ndipo suluhisho la kweli kwa matatizo haya linaweza kupatikana.

***************************

Ifuatayo ni tafsiri ya makala yaliyoandikwa na Kiongozi maarufu na shupavu, mtetezi mkubwa wa maslahi ya tabaka la wafanyakazi, V.L.Lenin hapo mwaka 1905. Makala haya yaliandikwa ili kukosoa fikra za kibwanyenye ambazo zilikuwa zikionezwa na wajamaa fulani fulani wa bandia. Ili mapinduzi yaweze kusonga mbele, ilipasa fikra zote za kupotosha ambazo zilienea kana kwamba ni za kijamaa kweli zifutiliwe mbali katika jumuia ya Urusi. Tunachapisha tafsiri hii kwani tunafikiri Afrika leo hii inakabiliwa na tatizo hili kubwa la kuenea kwa fikra za ujamaa wa bandia, yaani ujamaa wa kinjozi Kama Waafrika tunataka kufaulu katika jukumu letu, itapasa tuondoe fikra zote hizi na badala yake tuzingatie ujamaa wa kisanyansi.

WAHARIRI

## UJAMAA WA KINJOZI NA UJAMAA WA KISAYANSI

NA

V.I. Lenin

Kati ya fikra mbali mbali za ujamaa, ujamaa wa kisayansi ndio ulioenea zaidi pote katika Ulaya na harakati za kutaka kujenga jamii kwa misingi ya ujamaa wa kisayansi zinaendeshwa hasa na tabaka la wafanya kazi chini ya uongozi wa vyama vya Wafanya kazi. Kuenea huku kwa ujamaa wa kisayansi hakukuwa jambo la mara moja, bali ni matokeo ya mapambano marefu dhidi ya fikra duni za kila aina, ujamaa wa kinjozi, mauaji na maasi, n.k. Miaka thelasini hivi iliyopita, ujamaa wa kisayansi haukuwa umeenea hata Ujerumani, mahali ambapo kwa wakati huo fikra zilizokuwepo zilikuwa mchanganyika wa ujamaa wa kinjozi na ujamaa wa kisayansi. Fikra zilizokuwa zimetapakaa na kushikwa na wafanyakazi nchini Ufaransa, Hispania na Ubelgiji ni zile za wafuasi wa Proudhon, Blanqui na za waasi - fikra ambazo ziliwakilisha mtazamo wa kibwanyenye na sio wa kifanyakazi.

Ni kitu gani hasa kilichosababisha ushindi mkuu huu wa ujamaa wa kisanyansi katika miaka kadhaa iliyopita? Usahihi wa ujamaa wa kisayansi umethibitishwa na mwenendo na mabadiliko katika jamii - kisiasa hata kiuchumi, na vile vile harakati za matabaka yanayokandamizwa. Kufifia kwa tabaka la vibwanyenye kuliletelza kutokomezwa kwa fikra potofu za aina mbali mbali za vibwanyenye, ambapo kustawi kwa mfumo wa kibepari na kupevuka kwa harakati za Kitabaka katika jamii ya kibepari ndiko kulikozusha fikra za ujamaa wa kisayansi.

......./2

Hali duni iliyopo nchini Urusi imekomaza fikra mbali mbali za ujamaa zilizo potofu. Historia nzima ya fikra za kimapinduzi nchini Urusi katika miaka ishirini na tano iliyopita ni historia ya mapambano ya ujamaa wa kisayansi dhidi ya ujamaa wa kinjozi wa Manaraduik. Ingawa kustawi kwa vuguvugu la tabaka la wafanyakazi kumeleta ushindi wa ujamaa wa kisayansi nchini Urusi, kuibuka kwa vuguvugu la wakulima - hasa baada ya maasi maarufu ya Ukraina ya mwaka 1902 - kwa upande mwingine kumeleteleza kuibuka kwa fikra potovu za Ma-narodnik, fikra za Ma - Narodnik ambazo ni za unafiki mtupu ndiyo ngao ya Ma - Socralist - Revolutionaries. Ni kwa sababu hii ndiyo maana suala la wakulima ni suala muhimu katika mabishano yaliyopo kati ya wajamaa wa kisayansi na Ma - Narodnik pamoja na Ma - Socialist - Revolutionaries.

Kwa kiasi fulani, fikra za ma- Narodnik zilikuwa ni fikra zenye msimamo na uzito wa kipekee. Fikra hizo zilikanusha kuwa ubepari umeenea nchini Urusi, zilikataa wazo kuwa wafanyakazi viwandani ndio askari shupavu na walio mstari wa mbele kuliko wafanyakazi wengineo; zilikataa kukubali umuhimu wa mapinduzi ya kisiasa na kupatikana kwa uhuru wa kisiasa wa kibwanyenye; zilihubiri mapinduzi ya kijamaa ya mara moja ambayo misingi yake ni vijiji vya wakulima vikiwa vimebaki vile vile na zana zake duni za kazi. Kilichobakia sasa kutoka kwenye fikra hizi ni chembe chembe ya mawazo tu. Hata hivyo ili kuweza kuelewa kwa undani maswala yaliyopo na ili kuweza kuzuia tofauti za kifikra kuhusu maswala haya kuwa mabishano yasiyo na maana, ni muhimu kila wakati kukumbuka misingi ya fikra potovu za ma - Socralist - Revolutionaries - misingi ambayo mizizi yake iko katika fikra za ma - Narodnik.

Ma - Narodnik waliamini kuwa mkulima ndiye ngao na nuru ya jamii mpya nchini Urusi; na imani kama hii ilitokana kwanza na muundo wenyewe wa maisha huko vijijini ambao ni wa "kijamaa", na pili imani hiyo ilitokana na kutokuwa na imani katika mfumo wa kibepari. Wajamaa wa kisayansi, kwa upande mwingine, wanaamini kuwa mfanyakazi tu ndiye anayeweza kuleta ujamaa halisi nchini Urusi na kwamba kustawi kwa mfumo wa kibepari nchini Urusi katika kilimo na viwandani kunadhibitisha ukweli wa mawazo hayo siku hadi siku. Vuguvugu la tabaka la wafanyakazi nchini Urusi limetambulika mahali pote na kila mtu; lakini, kwa upande wa vuguvugu la wakulima, suala hili bado linatatanisha na tofauti zilizopo kuhusu suala hili zinatokana na tofauti zilizopo katika kulitafsiri baina ya Wajamaa wa kisayansi na ma - Norodnik. Kwa upande wa ma-Norodnik, vuguvugu la wakulima wanaliona kama ndilo linalothibitisha ujamaa wa kisayansi kutofaa nchini Urusi; kwamba ni vuguvugu ambalo litaleta ujamaa moja kwa moja; vuguvugu ambalo halijishughulishi na ukombozi wa kisiasa wa kibwanyenye; vuguvugu linalotokana na uzalishaji-mali unaotumia zana za kazi ndogo ndogo na sio kubwa na za kisasa. Kwa ujumla, kufuatana na mawazo ya ma-Narodnik, vuguvugu la wakulima ndilo hasa la kijamaa na ambalo litajenga ujamaa moja kwa moja. Imani ya ma-Narodnik katika vijiji vya wakulima na aina ya fujo inayoambatana na utekelezaji wa mipango yao- vyote kwa pamoja

ndiyo inayotufanya tuseme hivyo.

Kwa mjamaa wa kisayansi, yeye analiona vuguvugu la wakulima kama ni vuguvugu la kutaka demokrasi tu na wala si vuguvugu la kuleta ujamaa wa kisayansi. Nchini Urusi, kama jinsi ilivyo katika nchi nyingine, vuguvugu la wakulima linaambatana na mapinduzi ya kuleta demokrasi ambayo bado ni ya kibwanyenye tu- kijamii hata kiuchumi. Vuguvugu hilo si vuguvugu ambalo madhumuni yake ni kuvunjilia mbali misingi ya mfumo wa kibepari, yaani si vuguvugu dhidi ya uzalishaji wa bidhaa - mtaji. Bali ni vuguvugu ambalo madhumuni yake ni kuondoa mabaki ya mahusiano ya kiuchumi yanayoambatana na mfumo wa kikabaila - umilikaji wa ardhi na wa watwana. Kwa hiyo basi, ushindi wa vuguvugu hili la wakulima kwamwe haliwezi kuondoa mfumo wa kiuchumi wa kibepari; badala yake, litawezesha tu kuweka mazingara au misingi ambayo itawezesha ubepari kustawi vizuri zaidi. Ushindi wa vuguvugu hili utasaidia ujenzi wa dola la kibepari ambamo harakati za wafanyakazi dhidi ya mabepari zitaendeshwa kwa nguvu na mwamko zaidi.

Kwa hiyo basi, hii ndiyo misimamo miwili iliyo tofauti na ambayo inapashwa kueleweka na yeyote yule anayotaka kuchunguza tofauti kuu zilizopo kati ya ma-Socialist Revolutinaries na wajamaa wa kisayansi. Kwa upande wa ma - Socialist-Revolutionaries, vuguvugu la wakulima ndilo litakaloleta ujamaa, ambapo wajamaa wakisayansi wanaliona tu kama ni vuguvugu la kudai kuondolewa kwa mfumo wa kikabaila. Kwa hiyo, yeyote yule anaweza akaona ujinga wa hawa ma-Socralist-Revolutionaries, hasa wanapokuwa wakirudia rudia mara elfu kwa kudai kwamba eti wajamaa wa kisayansi wanapuuza suala la wakulima. Kuna njia moja tu ya kuweza kuondoa ujinga kama huo nao ni kwa kuanza kuwafundisha toka mwanzo kabisa msimamo wa ma-Narodnik na kwa kuwaelezea kuwa tofauti kuu iliyopo baina yetu haitokani na kukubali au kutokubali umuhimu wa suala la wakulima, wala haitokani na kulitambua au kutolitambua suala hilo bali inatokana na mitazamo yetu tofauti kuhusu vuguvugu la wakulima nyakati hizi na suala la wakulima nchini Urusi wakati huu. Yeyote yule anayethubutu kusema kwamba wajamaa wa kisayansi wanapuuza suala la wakulima nchini Urusi, kwanza ni mjinga mno kwani maandishi yote makuu ya wajamaa wa kisayansi wa Urusi - tukianzia na kijitabu cha Plakhanov kiitwacho "Tofauti zetu" (kilicho chapishwa miaka ishirini iliyopita) - kwa ujumla yanakuwa yakizungumzia upotovu wa fikra za ma-Narodnik kuhusu suala la wakulima nchini Urusi. Pili, yoyote yule anayesema kwamba wajamaa wa kisayansi wanalipuuza suala la wakulima anadhihirisha tu nia yake ya kutaka kuepa kutoa tofauti kuu zilizopo - tofauti ambazo ndizo tu zinatuwezesha kutoa jibu kwa swali kama kweli vuguvugu la wakulima la sasa ni la kudai tu demokrasi ya kibwanyenye au hapana; kama kweli vuguvugu hilo lina lengo la kuondoa kabisa mfumo wa kikabaila au hapana.



.......

Ma-Socialist-Revolutionaries kamwe hawajatoa na hawataweza kutoa jibu lililo fupi na sahihi kuhusu suala hili kwani hawana msimamo thabiti usipokuwa ule tu wa kuyumbayumba kati ya ma-Narodnik na wajamaa wa kisayansi. Wajamaa wa kisayansi wanadai kwamba Ma-Socialist - Revolutionaries wanawakilisha msimamo wa vibwanyenye (kwamba ni watetezi wa itikadi ya vibwanyenye) kwa vile hawawezi kujitoa kutoka fikra na ndoto za vibwanyenye na pia ndoto za ma-Narodnik katika kulitazama suala zima la vuguvugu la wakulima.

Ni kwa sababu hii ndiyo maana ni lazima tuanze kujifunza upya tangu mwanzo suala zima. Kwa wakati huu, vuguvugu la wakulima nchini Urusi lina madhumuni yapi hasa? Jibu ni ardhi na uhuru. Ushindi wa vuguvugu hili utakuwa na umuhimu gani? Baada ya kuleta uhuru wa watwana litakuwa limetokomeza utawala wa makabaila na warasimu katika utawala wa dola la kikabaila. Baada ya kunyang'anya ardhi, vuguvugu hili litaigawa ardhi hiyo kwa wakulima. Je, uhuru wa watwana na unyakuaji wa ardhi kutoka kwa makabaila kutafutilia mbali uzalishaji wa bidhaa? La hasha. Je, uhuru na ugawaji wa ardhi kwa wakulima pamoja na kuwakusanya wakulima katika vijiji vya "ujamaa" kutaondoa ukulima wa kibinafsi? La hasha, hauwezi. Je, uhuru na unyang'anyi wa ardhi kutoka kwa makabaila kunaweza kukapunguza tofauti iliyopo kati ya mkulima tajiri anayemilki msululu wa farasi na ng'ombe na mfanyakazi wa shambani, yaani tofauti inayotenganisha mkulima bepari na mfanyakazi wa shambani? Pia, jibu ni hapana. Badala yake, jinsi ukabaila unavyofutiliwa mbali ndiyo kadiri hiyo hiyo tofauti za kitabaka zinavyozidi kukua na kupanuka baina ya mabepari na wafanyakazi. Sasa basi, ni kitu gani hasa kitakachokuwa cha maana katika vuguvugu hili la wakulima pindi litakaposhinda? Ushindi wa vuguvugu hili lina umuhimu ufuatao: ni kwamba litaondoa mabaki ya ukabaila; lakini kamwe haliwezi kuvunjilia mbali mfumo wa kiuchumi wa kibepari na wala haliwezi kuondoa mgawanyiko wa watu katika matabaka (matajiri na maskini; mabepari na wafanyakazi) Ni kwa nini vuguvugu la wakulima hivi sasa ni vuguvugu tu la kudai demokrasia ya kibwanyenye? Ni kwa sababu, baada ya kuvunjilia mbali hatamu za warasimu na makabaila, jamii itaongozwa kwa mtindo wa demokrasi ya kibwanyenye - bila ya kubadilisha misingi ya ubepari iliyomo, katika jamii hiyo - yaani bila ya kubadilisha utawala wa mtaji. Ni namna gani basi mfanyakazi mwenye mwamko wa kisiasa anapashwa kulitazama suala hili? Ni dhahiri kabisa kwamba ni lazima aliunge mkono vuguvugu hili la wakulima, atoe msaada wa aina yoyote ile na kusaidia kuvunjilia mbali ngome ya utawala wa urasimu na makabaila. Papo hapo ni lazima awaeleze wakulima kuwa haitoshi kuvunjilia mbali utawala wa makabaila. Baada ya kuondoa utawala huo, ni muhimu kuanza papo hapo matayarisho ya kuondoa mfumo wa kibepari - utawala wa mabepari; na kwamba kwa madhumuni hayo ujamaa wa kisayansi unahitajika na fikra zake zianze kutawanywa mara moja; na kwamba wafanyakazi mashambani sharti waungane dhidi ya wakulima wa kibepari na

......./4

mabepari wa Urusi kwa ujumla. Ili wafanyakazi kwenye msimamo wa juu kisiasa achapushwe kupunza harakati za kuleta demokrasi na badala yake kutilia mkazo harakati za kuleta ujamaa, au la, [illegible] na kuzingatia za kwanza? Jibu ni hapana. Wafanyakazi kwenye msimamo wa juu kisiasa [illegible], anajiita 'Socialist-Democrat' [illegible] uhusiano uliopo kati ya aina mbili hizo za harakati. Anafahamu kwamba hakuna njia nyingine ya kujenga ujamaa wa kisayansi isipokuwa kwa kupitia kwanza uhuru wa kisiasa. Kwa sababu hiyo atajitahidi kupigania demokrasi kwanza ili baadaye aweze kufikia lengo kamili- ujamaa wa kisayansi. Ni kwa nini msisitizo wa kupigania demokrasi ni tofauti na yale ya kupigania ujamaa wa kisayansi? Sababu yenyewe ni kwamba tabaka la wafanyakazi litaungana na matabaka tofauti katika aina mbili hizo za mapambano. Harakati za kudai demokrasi zitaendeshwa na tabaka la wafanyakazi pamoja na makundi fulani fulani ya mabwanyenye - na hata vibwanyenye. Lakini harakati za kuleta ujamaa wa kisayansi zitaendeshwa na tabaka la wafanya-kazi dhidi ya mabepari wote. Harakati dhidi ya warasimu na makabaila zinaweza pia ni lazima ziendeshwa kwa kuungana na wakulima wote - hata pamoja na wakulima wa hali ya juu na wakulima wa hali ya kati. Lakini inapokuja kwenye harakati dhidi ya mabepari ni wafanyakazi masikini tu ndio wanaoweza kuziendesha harakati hizo mpaka kufikia ushindi.

Iwapo tutazingatia fikra hizi za ujamaa wa kisayansi- fikra ambazo zinaepwa na ma-Socialist-Revolutionaries- hatuwezi kupata shida katika kupima makanusho ya ma-Socialist-Revolutionaries kuhusu ujamaa wa kisayansi, kama; "Kwa nini ilikuwa ni lazima kwanza kuunga mkono wakulima dhidi ya makabaila, halafu papo hapo kuunga mkono wafanyakazi dhidi ya wakulima kwa ujumla badala ya kuwaunga mkono wafanyakazi mara moja dhidi ya makabaila; ni namna gani ujamaa wa kisayansi unahusika katika suala hili, Mungu peke yake ndiye anaelewa."

Mawazo kama haya ni ya kipuuzi sana- na ya kitoto. Kwa karne nyingi si ajabu hata kwa maelfu ya miaka iliyopita, binadamu amekuwa akiwaza namna gani angeondoa kwa mara moja unyonyaji wa aina yoyote ile. Mawazo haya yaliendelea kubaki njozi tu hadi hapo mamilioni ya wananchi wanaonyonywa pote ulimwenguni walipoanza kuungana na kuanza kuendesha harakati kali na ngumu za kutaka kubadilisha na kuiweka jamii ya kibepari katika mwelekeo ambao kila jamii ya aina hiyo itabidi ifuate. Ujamaa wa kinjozi ulibadilika na kuwa ujamaa wa kweli wakati ujamaa wa kisayansi ulipounganisha lile shauku la wananchi la kutaka mabadiliko na harakati za tabaka maalumu. Bila ya mapambano ya kitabaka ujamaa unabakia kuwa tamshi tupu au ndoto tu. Nchini Urusi aina mbili tofauti za mapambano ya kitabaka zinaendeshwa. Wafanyakazi wanapambana dhidi ya mabepari popote pale palipo na mahusiano ya kiuchumi ya kibepari (na kweli mahusiano haya yapo - na hii inapashwa ieleweke na ma-Socialist-Revolutionaries- Mahusiano haya ya kibepari yapo hata katika vijiji ambavyo ma-Socialist-

Revolutionaries hudai kuwa eti sasa ni vya "ujamaa". Wakulima kmz sehemu ya kundi la watu wanaomilki ardhi kidogo-yaani kama sehemu ya tabaka la vibwanyenye, nao pia wanapambana dhidi ya mabaki ya ukabaila, dhidi ya warasimu na makabaila. Ni wale tu wasioelewa siasa-uchumi na historia ya mapinduzi ulimwenguni ndio wanaoshindwa kuelewa kwamba hivi ni vita viwili vya kitabaka na vilivyo tofauti kabisa. Kule kufumba macho ili mtu usione tofuati kati ya aina hizi mbili za vita na kuendelea kudai kuwa ujamaa ujengwe "mara moja", ni sawa na mtu kuficha kichwa chake kwenye bawa na kukataa kufanya uchambuzi halisi wa mambo.

Ma-Socialist-Revolutionaries ambao hawafuati tena ile nadharia ya ma-Narodnik, sasa wamekwishasahau hata mafunzo ya ma-Narodnik wenyewe. Kama gazeti la Revolutsionnaya Rossiya lilipochapisha makala moja lilisema yafuatayo, "kwa kuwasaidia wakulima kuwanyang'anya ardhi makabaila Bw. Bw. Lenin, bila ya yeye mwenyewe kujua, anasaidia kujenga uchumi wa vibwanyenye kwa kutmia misingi ya mfumo wa kibepari unaostawi huko vijijini. Je, kulingana na nadharia ya ujamaa wa kisayansi, kufanya hivyo sio sawa na kurudi nyuma hatua moja?"

Ni aibu iliyoje, jamaa zangu!!! Je, umekwishasahau mpenzi wako Bw. V.V.!! Soma kitabu chake kiitwacho Destiny of Capitalism na pia kitabu kiitwacho The Sketches kilichoandikwa na Bw. Nikolai-on pamoja na vitabu vingine. Hapo ndipo utakumbuka kwamba ukulima wa kikabaila nchini Urusi umekuwa ukiingiliwa na mfumo wa Kibepari. Ndipo mtafahamu kuwa upo mtindo wa uchumi unaotegemea ukusanyaji wa kodi kutoka kwa watwana na ambao ni mabaki ya mtindo wa kikabaila wa kufanyishwa kazi kwa nguvu. Iwapo utajaribu kusoma kitabu MTAJI (Capital) kilichoandikwa na Karl Marx, utaona kwamba hakuna mahali ambapo mtindo wa watwana kufanyishwa kazi na makabaila ungeweza ukastawi, kwa kweli-hakuna mahali ambapo mtindo huo ulikua ukastawi na halafu ukabadilika na kuwa mtindo wa uchumi wa kibepari bila kwanza kupitia mtindo wa kilimo ambao mkulima ana ardhi yake na zana zake za kazi. Katika jitihada zako za kuvuruga fikra za ujamaa wa kisayansi, njia unazotumia ni njia za kishenzi ambazo zinatambulika tangu siku nyingi; unasingizia ujamaa wa kisayansi kuwa eti ndio unaodai kwamba ukulima wa kibepari unaotumia mtaji mkubwa utatokana na ukulima wa kikabaila unaotegemea watwana. Unaendelea kusema kuwa kwa vile mazao yapatikanayo kwenye mashamba ya kikabaila ni mengi zaidi kuliko yale yanayopatikana kutoka kwenye mashamba madogo madogo ya wakulima, kule kuwanyang'anya ardhi makabaila ni hatua moja nyuma. Mawazo kama hayo yanamfaa tu mwanafunzi wa darasa la nne. Hebu fikirieni jamani hili lifuatalo: eti ilikuwa ni "hatua moja nyuma" kule kutenganisha mashamba hafifu ya wakulima wadogo wadogo kutoka kwenye mashamba yenye rutuba ya makabaila wakati ukabaila ulipovunjiliwa mbali!!!

Sasa hivi nchini Urusi, kilimo ni mchanganyiko wa mifumu miwili ya kiuchumi nayo ni: mfumo wa kibepari na mfumo wa kikabaila. Hasa hasa,

..........6

leo hii, harakati za wakulima dhidi ya makabaila ni harakati dhidi ya mabaki ya mfumo wa kikabaila. Hata hivyo, kule kujaribu kuorodhesha mambo yote na kupima kila jambo kwa ustadi kama daktari anavyofanya na kujaribu kuweka mipaka - wapi ukabaila unapoishia na wapi ubepari unapoanza,kufanya hivyo ni sawa na mtu kuwasingizia wajamaa wa kisayansi kama eti ndio wanaosababisha ujinga wake. Tunaweza kushindwa kupima ile sehemu ya bei ya vitu vilivyonunuliwa kutoka kwa mfanya biashara na ambayo inawakilisha thamani - kazi; na pia tunaweza tukashindwa kupima ile sehemu nyingine ambayo ni wizi tu. Lakini, je hii ina maana kwamba nadharia ya thamani-kazi haina manufaa tena?

Kilimo cha siku hizi ni muungano wa mitindo miwili ya kiuchumi-ubepari na ukabaila. Lakini ni wajinga tu ndio wanaoweza kudai kwamba ni jukumu letu kupima, kuhesabu na kunakiri kila sifa iliyomo katika mitindo hiyo miwili na halafu kuchambua jamii. Ni wale waliomo ndotoni tu ndio wanaoweza kusema kwamba "hakuna haja" kwetu sisi kutofautisha kati ya vita hivi viwili vya kitabaka-kwa kweli tunaweza kumalizia kwa kutamka kuwa katika mipango na mbinu zetu ni lazima kuunganisha harakati zilizo za wafanyakazi tu - harakati dhidi ya mabepari na harakati za wakulima wote za kudai demokrasi-ambazo ni harakati dhidi ya makabaila.

Kadiri ubepari unavyoingia huko mashambani ndiyo kadiri hiyo hiyo ilivyo umuhimu wa kuteganisha wafanyakazi wa mashambani, kwa sababu hii itasaidia kukuza uhasama wa wafanyakazi dhidi ya mabepari mara tu makabaila wanapo pokonywa ardhi yao. Na kadiri ubepari unavyoingia mashambani ndivyo hivyo hivyo kunyang'anywa kwa ardhi ya makabaila kutatia moto harakati za wa ujamaa wa kisayansi - na vivyo hivyo ndivyo ilivyo ile hatari ya kuchukulia mapambano ya kuleta demokrasi kama kwamba ndiyo ujenzi wa ujamaa wenyewe.

Kwa hivyo basi ni muhimu kuunganisha harakati zilizo tu za kifanyakazi na harakati za wakulima kwa ujumla- lakini kamwe, tusije tukazichanganya aina mbili hizi za harakati. Ni lazima tuunga mkono harakati za wakulima za kudai demokrasi, lakini tusije tukapumbazwa na harakati hizo ambazo si za kitabaka; tusije tukashangilia harakati hizo kama kwamba ndizo harakati katika ujenzi wa ujamaa; aidha tusije tukasahau ule umuhimu wa kuunganisha wafanyakazi walioko mijini na wafanyakazi wa mashambani katika chama cha kisiasa cha wafanyakazi. Ingawa chama cha kisiasa cha wafanyakazi kitaunga mkono jitihada zote za kudai demokrasi, hata hivyo chama hakiwezi kukubali kutolewa kwenye mkondo wa kimapinduzi na njozi na majaribio ya kipinga-mapinduzi ya kutaka kuleta "usawa" wakati mfumo wa kiuchumi bado ni ule wa uzalishaji bidhaa. Kwa wakati huu, harakati za wakulima dhidi ya makabaila ni harakati za kimapinduzi; kunyakuwa kwa ardhi ya makabaila wakati huu wa mabadiliko ya kiuchumi na siasa - ni kitendo cha ki-mapinduzi kwa kila hali, na tunaunga mkono kitendo hiki

ambacho ni cha ki-mapinduzi na cha kudai demokrasi. Lakini kulo kuita kitendo hiki kama ni kitendo cha "kijamaa" na kujidanganya na pia kuwa danganya wananchi kuhusu uwezekano wa kuleta "usawa" katika umilkaji wa ardhi ambapo mfumo wa kiuchumi bado ni ule wa uzalishaji wa bidhaa, hii ni njozi za vibwanyenye wapinga-mapinduzi-njozi ambazo zinawafaa tu wao wenyewe.